

ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

- | | |
|---------------------------------------|--|
| 1. Mhe. Ali Abdalla Ali | Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini. |
| 2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa | Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni. |
| 3. Mhe. Mgeni Hassan Juma | Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake. |
| 4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi | MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais. |
| 5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani. |
| 6. Mhe. Omar Yussuf Mzee | MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais. |
| 7. Mhe. Haji Omar Kheri | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/JimbolaTumbatu |
| 8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais. |
| 9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed | MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais. |
| 10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary | MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni. |
| 11. Mhe. Rashid Seif Suleiman | MBM/ Waziri wa Afya/Jimbo la Ziwanii. |
| 12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban | MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais. |

13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvumi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.

25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26. Mhe. Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
27. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28. Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29. Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvubi/Jimbo la Mpandae.
31. Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
32. Mhe. Said Hassan Said	Mwanasheria Mkuu.
33. Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34. Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35. Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais
37. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40. Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41. Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake

43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo

65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
74.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
75.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
76.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
77.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	Jimbo la Jang'ombe
78.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
79.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
80.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad

Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Ishirini na Nane - Tarehe 23 Juni, 2015

(Kikao kilianza saa 3.00 asubuhi)

DUA

Mhe. Spika (Pandu Ameir Kificho) alisoma Dua

TAARIFA YA RAIS

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Taarifa ya Mhe. Rais ya leo inahusu ujio wake hapa katika ukumbi huu wa Baraza la Wawakilishi, taarifa hiyo nimeipata baada ya kupokea barua inayotoka Ofisini kwake barua ya tarehe 19 Juni, 2015 yenye kumbukumbu No. IKL/PS/BLW-41/Vol. IV/14 ya tarehe 19 Juni, 2015. Barua inaeleza kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anakusudia kuja kulihutubia Baraza la Wawakilishi mnamo tarehe 26 Juni, 2015 saa 9.30 za Alasiri na kwa kuwa ujio wake ni maalum kwa ajili ya kumalizika kwa muhula wa miaka 5 ya chombo hiki cha Baraza, Baraza la Nane baada ya kulitumia Baraza hatimaye atatoa tamko rasmi la kulivunja Baraza na litavunjika rasmi kunako tarehe 13 Agosti, 2015. Lakini ye ye atatoa tamshi hilo hapo tarehe 26 Juni, 2015 mnamo saa 9.30 za Alasiri, hiyo ndio taarifa ya Mhe. ya Mhe. Rais ambayo amenituma nije niitoe kwenu ili mambo mengine baada ya hapo yafuate. Ninashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe kwa kupokea taarifa hiyo ya Mhe. Rais. (*Makofii*)

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Shilingi Bilioni Mia Nane na Thalathini Mia Tatu na Sitini Milioni na Laki Tatu kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2016 na kuruhusu Utoaji na Uhaulishaji wa Fedha hizo pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo

(Kusomwa mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena naomba nitimiza wajibu wa Kikatiba chini ya Kifungu 106 kinachomtaka Waziri mwenye dhamana ya Fedha kuwasilisha katika Baraza la Wawakilishi Mswada wa Sheria kwa ajili ya kuidhinisha Matumizi ya Serikali kila mwaka unapoanza. Kwa heshima kubwa naomba sasa na kwa ruhusa yako niwasilishe mapendekezo ya Mswada wa Sheria wa Kuidhinisha Makisio ya Matumizi...

Mhe. Spika: Mhe. Waziri, unawasilisha kwanza kwa kusomwa kwa mara ya kwanza, kwa kusoma *long title* ya mswada huo. Katibu anakusaidia juu ya utaratibu huo.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, naomba niwasilishe Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Shilingi Bilioni Mia Nane na Thalathini Mia Tatoo na Sitini Milioni na Laki Tatoo kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha unaoishia siku ya tarehe 30 Juni, 2016 na kuruhusu Utoaji na Uhaulishaji wa Fedha hizo pamoja na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mhe. Spika: Na kwamba mswada huo sasa ndio umesomwa mara ya kwanza. Kama tunavyoolewa taratibu zinahitaji kwamba mswada wa aina kama hii zile mara tatu zote zile ya kwanza ikiwa ndio hii basi zifanyike katika mkutano huu huu.

Baada ya uwasilishaji huo wa mswada huo kusomwa kwa mara ya kwanza, naomba sasa nimkaribishe tena Mhe. Waziri ili awasilishe mswada kusomwa kwa mara ya pili. Sasa unatoa maelezo yako yale na mwisho utoe hiyo hoja.

TAARIFA

Mhe. Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, naomba kukushukuru sana na pengine si kawaida katika utaratibu kwa hali tuliyofikia nikaomba ruhusa yako. Naomba ruhusa yako kwa masikitiko sana kwamba mimi kwa niaba ya mawaziri wenzangu waliomo Serikalini upande wa CUF, kwa niaba ya Wawakilishi wenzangu waliomo ndani ya CUF na kwa niaba ya chama changu kukushukuru sana kwamba tumeshirikiana miaka 5 pamoja na kufanya kazi pamoja.

Lakini kwa masikitiko sana naomba kukwambia kwamba sisi kuanzia sasa tunatoka humu Barazani sote tuliokuwa watu wa CUF na sababu yetu kubwa Mheshimiwa, haturidhiki na hatukutegemea kwamba utaratibu na uendeshaji wa kuandikisha wapiga kura utakuwa na vurugu kama unavyofanywa. Hatujawahi kuona maisha yetu askari akavaa ninja akaingia mitaani anapiga raia waliokuwa hawana hatia, magari ya jeshi yanapita yamechukua na marisasi kama vile kuna vita. Mheshimiwa, haturidhiki utaratibu huu unaoendeshwa na Wizara ya Tawala za Mikoa na SMZ katika mfumo uliokuwa haujawahi kutokeea.

Kwa hivyo, kwa masikitiko makubwa hatukuwa na njia nyengine, tumejitahidi kulieleza hili katika vikao mbali mbali, lakini hali inayotokea huko nje ni vurugu, watu wanapigwa, wanatiwa ndani bila ya kosa. Kwa hivyo, sisi hili limetushinda

kustahmili Mheshimiwa na tunaomba tutoke tuendelee nyinyi kuwaachia muendelee na Baraza hili ili tupate nufaa inayostahiki. Ahsante Mheshimiwa. Kwa hivyo, nawaomba Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kutoka CUF...(Makofî)

(*Hapa Wajumbe wa CUF walitoka nje ya Ukumbi*)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Mhe. Spika, kwa masikitiko makubwa sana kitendo ambacho amekielezea Mhe. Juma Duni Haji, ambaye ni Waziri wa Miundombinu na Mawasiliiano, alichokieleza hapa imbele ya Baraza lako Tukufu sisi kwa upande wetu Mawaziri kutoka CCM na Wawakilishi wanaotokana na Chama cha CCM jambo hilo limetusikitisha sana.

Mhe. Spika, uandikishaji upo kwa mujibu wa Katiba na Sheria ya nchi yetu na hata siku moja Baraza la Wawakilishi wajibu wake siku zote ni kusimamia sheria. Kunapotokea tendo lolote la kinyume na sheria utaratibu unaotumika ni kufuata mkono wa sheria katika kufatilia haki ya msingi inayohusu sheria hiyo. Ni kinyume na sheria kabisa kuchanganya sheria na mambo ya kisiasa, ama kulitumia Baraza lako hili tukufu na mambo ya kisiasa.

Mhe. Spika, tumefanya kazi na wenzetu kwa kipindi cha miaka 5 hakukuwa na kauli ya namna hii, lakini sasa kwa sababu tunamalizia Baraza hili na kutokana na kauli ulioionesha sasa hivi hapa ya kwamba tunategemea kulivunja Baraza hili tarehe 26 Juni, 2015 kwa sasa yanatokea matokeo ambayo kwa vyovyote vile kwa watu na wananchi wa kawaida watajua kabisa kama wenzetu hawa wana jambo ambalo lina undani na si la dhamira njema kwa nchi hii. Nia na madhumuni ya Serikali yetu ni kuendesha uchaguzi huru na wa haki na kila mwenye haki aweze kupaa nafasi hiyo ya kutumia fursa yake kwa mujibu wa Katiba na Sheria ili aweze kuchagua kiongozi anayemtaka bila ya kuingiliwa kufuata utaratibu wa sheria.

Kitendo ambacho wenzetu wamekionesha nadhani si tu kitakitia aibu Chama cha CUF, lakini kinasikitisha sana sana kwetu sote wananchi wa Zanzibar kwa namna tulivyojitolea kutafuta amani, utulivu na umoja wa nchi yetu, ikawa wenzetu ikiwa ni chanzo cha kuhakikisha wanaharibu utaratibu huo. Kwa hivyo, Mhe. Spika, sisi Wawakilishi wako tunaotokana na CCM na Mawaziri wanaotokana na CCM tutaendelea kushiriki katika kikao hiki cha Baraza hili Tukufu na kwa kuwa *quorum* inatimia Mhe. Spika, tuendelee na shughuli zetu. Ahsante sana.(Makofî)

Mhe. Spika: Mnadhim wa Serikali ameshazungumza na bila shaka anazungumza hayo kwa niaba ya Mkuu wa Shughuli za Serikali katika chombo hiki, kwa hivyo, kwa leo amepata dharura yuko kwenye shughuli za aina kama hii pale Dodoma.

Waheshimiwa Wajumbe, jambo hili limetokea vijana wa kileo husema *by surprise*, ikiwa nimelielewa, sikuwahi kulisikia na hata mnong'ono nadhani kati yetu pia ilikuwa hatukuwahi kupata, sisi tulio baki humu ndani. Sasa kazi hii inaweza ikaenda ila na hii ndio katika yale mambo ambayo ni muhimu sana kuhakikisha wakati wote tunakuwa na wajumbe wa kutosha, leo mfano halisi ndio huu. Ingekuwa ni Katiba hatuna namna kwa sababu *quorum* ya kuweza kubadilisha Katiba haipo, lakini kwa hili inawezekana.

Sasa niwaambie wale tulio wakabidhi kazi kukaimu kazi ya unadhimu waifanye kazi hiyo, Mnadhim wa Serikali na wewe fanya kazi hiyo kwa upande wa Serikali wenzio ili tunafanya mjadala wa jambo hili lakini hatimaye tuwe na *quorum* ya kutosha ya kuitisha rasmi jambo hili. Kwa hivyo, mimi limenisikitisha, bahati nzuri mfumo huu wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa makusudia yake ilikuwa ni kujaribu kupunguza mivutano, mivutano katika chombo hiki, lakini mivutano hata kwa wananchi ili kama tatizo ni suala zima la kushirikiana katika kugawana nafasi ndani ya Serikali basi mfumo huu tukaupitisha rasmi pale 2010 na wananchi wenyewe waliupigia kura za maoni na ikafika kwenye 66 na *point* kama 4 hivi asilimia ya wananchi waliosema kwamba mfumo huu uendelee na uwepo. Kitendo hiki kwa kiasi fulani kinateteresa hata kauli ya wananchi waliosema na tukakubaliana kwamba turekebishe Katiba yetu pale mwaka 2010 ili kuruhusu rasmi mfumo huu kwa mujibu wa Katiba.

Tumerekebisha hivyo kutokana na kauli ya wananchi, kwa sababu wananchi wakishasema maana yake wananchi ndio wenye nchi hii, wakishaamua maana yake sisi sasa turekebishe iendane kwa mujibu ya wale wananchi wanavyohitaji na tumefanya hivyo. Niwashukuru wajumbe wa Baraza lile la Saba kwa kufanya kazi hiyo vizuri na tukawa tumefanya kazi hii tukiwa chini ya mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Kwa kiasi kikubwa tumeshirikiana, changamoto haziishi na hasa kwa jambo jipya, lakini jambo hili mpaka nilipokuwa safarini pale *European Union* nimelizungumza. Bahati nzuri nadhani nilifanya kitu si kizuri kukwambieni kwamba Spika wenu alipata nafasi akahutubia Bunge la *European Union* na ajenda moja niliyopeleka ni mfumo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa *GNU*, nikaulizwa maswali mengi sana tukayajibu hatimae wakafurahi, wakasema huu ni mfumo mpya, lakini kwa kuwa unakusaidieni ni jambo jema mkauendeze, *European Union*.

Sasa jambo hili linaleweka kimataifa, baada ya jambo hili kueleweka nakumbuka viongozi wakuu wetu walipata nafasi wakenda nchi mbali mbali pamoja na Marekani kuzungumza suala la mfumo huu na makubaliano yetu ambayo ni maamuzi ya wananchi na hatimae yakawekwa rasmi Kikatiba na tukafikia pahala sasa tumekwenda vizuri kwa kiasi tulivyokwenda. Narudia kusema kwamba changamoto haziishi na kwa vyovyyote itakavyokuwa changamoto za aina hii

zitakuwepo, lakini usuluhishi wake au ufanuzi wake au uamuzi wake ni kujaribu kukabiliana na hizi changamoto ili hatimae mkaweza kwenda vizuri.

Waheshimiwa Wajumbe, kitendo hiki si tu kimetupa aibu humu ndani ya chombo hiki, lakini kitendo hiki kinawapa maswali wananchi kwa sababu ndio waliosema kwamba tuje na mfumo huu. Kama utakumbuka tarehe 31 Julai, 2010 ndio kura ya maoni ilipigwa siwezi kuisahau na hii inatokana na tukio muhimu la wananchi, ilikuwa tarehe 31/07/2010. Na hoja yake ilianzia na hoja ya mwenzetu Mhe. Abubakar Khamis Bakary ndiye aliyeanza hoja hii, ni mmoja katika Wawakilishi wa upande wa *CUF*. Wengine tukachangia hatimae tukarekebisha mpaka tukarekebisha mpaka tukafikia muafaka na hatimae suala la Mswada wa Kura ya Maoni ukapitishwa ili jambo hili liende kwa wananchi.

Mazungumzo yake yalikuwa marefu yameanzia kwenye vyama, sasa Waheshimiwa Wajumbe, muliobaki wa Chama cha Mapinduzi nataka tuelewe na tujikumbushe kwamba kumbe ni wakati wowote tuwe askari na kawaida ya askari kunapotokea jambo anahami nchi yake. Sasa sisi tuliobakia humu ndani ndio wa kuhami nchi yetu hii. Nakuombeni sana tuwe wamoja, tushirikiane na tunasihiiane zaidi ili kuona nchi hii tunaihami kwa faida ya wananchi wote. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe, hili lilihusu tuwe na hotuba rasmi ndefu, lakini kwa kuwa jambo lenyewe ilikuwa ni *surprise* basi kwa sasa na kwa leo hii itoshe maneno haya, kwamba sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wananchi wajue hii ndio wa kuihami nchi hii ya Zanzibar kutoka muda mwangi uliopita huko nyuma, hivi sasa na siku nydingi zijazo. Tuna wajibu huo na nakuombeni sana tuifanye kazi hiyo kwa mashirikiano makubwa sana ili tuhakikishe kwamba hatimae wananchi wa nchi hii watapata maendeleo ambayo wanayahitaji kutoka kwetu. Sisi ni viongozi ndio viongozi, wenzetu wale pia nao ni viongozi wamechaguliwa na wananchi hao, lakini bahati mbaya sana leo wamekana maamuzi ya wananchi kufanya kazi kwa pamoja chini ya Mfumo wa Serikali ya *GNU*. Sisi tuliobaki tuendelee kufanya kazi kwa nguvu zote, kwa moyo wote ili kuwatetea wananchi wetu na kutetea maendeleo yao. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wajumbe, nakushukuruni sana na sasa tuendelee isipokuwa ile kazi ya kutafuta wajumbe ifanyike haraka sana. Tunaendelea. (*Makofi*)

Mheshimiwa, taratibu, Spika akishasema, kaa kitako. Mhe. Waziri, endelea.

(*Hapa Mhe. Spika, alitamka kwa ukali kumwambia
Mhe. Hamza Hassan Juma kukaa chini*)

Mswada wa Sheria ya Makisio na Matumizi ya Mwaka 2015

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, wahenga wanasema “mtoto umleavyo ndivyo akuavyo”. Nataka niwahakikishie wenzangu wa Chama cha Mapinduzi tutaendelea kuwa pamoja na kutekeleza majukumu ya wananchi, na hii ni ishara inayotupa nguvu wanachama wa Chama cha Mapinduzi kuyachukua majimbo yote. Tutaifanya kazi hiyo ili Baraza lijalo tuwemo wingi zaidi humu ndani, ili kuweza kutekeleza shughuli za wananchi waliotutuma.

Mhe. Spika, niliona na mimi niongezee kwa sababu sikufurahishwa hata kidogo na vitendo vya wenzetu, Sheha mmoja anawahangaisha tuna Masheha zaidi ya mia tatu. (*Makofifi*)

Mhe. Spika, kwa mara nyengine tena naomba nitimize wajibu wa Kikatiba chini ya Kifungu 106 kinachomtaka Waziri mwenye dhamana ya Fedha kuwasilisha katika Baraza la Wawakilishi Mswada wa Sheria kwa ajili ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali kila mwaka unapoanza, kwa heshima kubwa naomba sasa na kwa ruhusa yako niwasilishe mapendekezo ya Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio ya Matumizi ya Bilioni Mia Nane na Thalathini, Milioni Mia tatu na Sitini na Laki Tatu kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha unoishia siku ya tarehe 30 June, 2016 na kuruhusu utoaji na uhaulishaji wa fedha hizo pamoja na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, baada ya kuelezea wajibu huo wa Kikatiba napenda nianze kwa kukushukuru kwa dhati wewe mwenyewe binafsi pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza lako tukufu kwa mashirikiano makubwa ambayo kwanza yaliniwezesha mimi na watendaji wangu wa Wizara ya Fedha kuandaa na kuiwasilisha Bajeti ya Serikali ambayo ilipitishwa na Baraza lako tukufu. Pili, katika kuchangia bajeti za wizara zote za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na hatimae kumalizia na Bajeti ya Wizara ya Fedha, nawashukuru sana kwa mapenzi yenu kwa serikali na wananchi wa Zanzibar bila ya nyinyi kukubali bajeti, watendaji ndani ya serikali hawatoweza kutekeleza majukumu yao.

Mhe. Spika, kuidhinishwa kwa bajeti za wizara zote hizo kunapelekea Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi kutoa uwezo kwa serikali kutumia kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina shilingi bilioni mia nane na thalathini, milioni mia tatu na sitini na laki tatu, kati ya fedha hizo shilingi bilioni mia nne na thalathini na moja, milioni mia nne na nne na laki mbili kutumika kwa ajili ya kazi za kawaida na shilingi bilioni mia tatu na tisiini na nane, milioni mia tisa na hamsini na sita na laki moja kwa ajili ya kazi za maendeleo.

Mhe. Spika, kupitishwa kwa mswada huu utaiwezesha pia serikali kukopa fedha ndani na nje kwa ajili ya matumizi ya ndani kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 June, 2016. Kiasi cha fedha kilichoainishwa kwa ajili hiyo ni kama kinavyoongozwa na masharti ya kifungu cha 5 (1) cha mswada huu.

Mhe. Spika, mswada huu una vifungu 9; kifungu cha 1 kinazungumzia jina fupi, kifungu cha 2 kinazungumzia tafsiri, ambacho kifungu cha 3 kinazungumzia utoaji wa shilingi bilioni mia nane na thalathini, milioni mia tatu na sitini na laki tatu kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali.

Mhe. Spika, kifungu cha 4 kinazungumzia makisio ya fedha zilizokubalika, kifungu cha 5 chenye vifungu vidogo (4) kinazungumzia uwezo wa waziri mwenye dhamana ya fedha wa kukopa, kifungu cha 6 chenye vifungu vidogo (3) kinazungumzia uwezo wa waziri katika maombi ya ziada kwa lengo la kukabili matumizi mengine ya dharura pale haja itakapo jitokezea.

Mhe. Spika, kifungu cha 7 kinazungumzia marejesho ya mkopo na riba, kifungu cha 8 kinazungumzia kukubaliwa kwa mpango wa maendeleo na kifungu cha 9 ambacho ni cha mwisho kinazungumzia kukubaliwa kwa fedha zilizopitishwa kwa matumizi ya maendeleo.

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo mafupi ya mswada huu kwa idhini yako sasa niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako tukufu kuujadili na hatimae kuupitisha mswada huu ili uwe ni Sheria ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka fedha 2015/2016. Mhe. Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Spika: Ahsante sana hoja imetolewa na imeungwa mkono, kwa hivyo, sasa iko wazi kwa mjadala, nafasi ya kwanza basi nimpe Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti.

Mhe. Mahamoud Mohammed Mussa (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti): Mhe. Spika, ahsante kwa kunipa fursa hii kwa niaba ya Mwenyekiti kusoma ripoti ya Wenyeviti katika kupitisha hii *bill* ambayo Mhe. Wazir ameizungumza hapa. Lakini kabla sijaanza Mhe. Spika, naomba uniruhusu nitoa masikitiko yangu juu ya kitendo ambacho kimetokea hapa na wenzetu, sisi sote ni watumishi wa wananchi na jukumu letu ni kuwatumikia wananchi wa nchi hii ili kwa lengo la kuleta maendeleo.

Mhe. Spika, vile vile, Waswahili wana msemo wanasesma kwamba; “Lisemwalo lipo na kama halipo laja” lakini leo hatimae limedhihirika. Sisi kwa niaba ya wenzangu na wananchi wa Jimbo la Kikwajuni tunalaani sana kitendo hiki cha viongozi wenzetu kupewa jukumu na hatimae kuweza kufanya kama ambavyo

wamefanya, lakini wananchi ndio watahukumu na serikali hii inaongozwa katika misingi ya utawala bora na utawala wa sheria. Kwa hiyo, ni imani yangu sheria itachukua mkondo wake na pale ambapo panakidhi neno la msingi na neno la muhimu litafanya kazi na wanaohusika watayasimamia ipasavyo. Baada ya maelekezo hayo sasa Mhe. Spika, nielekee katika hotuba ambayo nimekuja kusimama hapa kuisoma kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Wenyeviti. (*Makofî*)

Mhe. Spika, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutujaalia uzima na afya njema kukutana hapa kwa ajili ya kuwatumikia wananchi wa Zanzibar. Lakini pia tumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kuufikia mwezi mtukufu wa Ramadhani tukiwa hai na wazima. Tunamuomba Mwenyezi Mungu azikubali funga zetu na ibada zetu katika mwezi huu mtukufu wa Ramadhani na tunawatachia wananchi wote wa Zanzibar Ramadhan *Kareem*.

Mhe. Spika, aidha, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii ya kuwasilisha mbele ya Baraza lako tukufu maoni ya Kamati ya Wenyeviti wa Kamati ya Kudumu ya Baraza hili, kuhusu Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Shilingi Bilioni Mia Nane na Thalathini, Mia Tatu na Sitini Milioni na Laki Tatu Kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali Kwa Mwaka wa Fedha Unaoishia Siku ya Tarehe 30 June, 2016 na kuruhusu utoaji na haulishaji wa fedha hizo pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, kwa upekee kabisa napenda kumshukuru na kumpongeza sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dk. Ali Mohammed Shein kwa busara zake, hekima zake anazozitumia katika kuiongoza nchi hii kwa kushirikiana na wasaidizi wake Makamu wa Kwanza wa Rais na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais katika Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar Mhe. Balozi Seif Ali Iddi.

Mhe. Spika, pia, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wote wa Baraza hili kwa kuichangia na kutoa maoni yao kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2015/2016 na mashirikiano makubwa waliota ili kufanikisha kukamilisha kwa kazi za kamati hii.

Mhe. Spika, napenda pia kuwashukuru Waziri wa Fedha Mhe. Omar Yussuf Mzee, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha Nd. Khamis Mussa Omar, Naibu Katibu Mkuu Nd. Juma Ameir Hafidh na Kamishna wa Bajeti Nd. Mwita Mgeni Mwita pamoja na Wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa mashirikiano yao makubwa waliota katika kufanikisha kumalizika kwa kazi za kamati yangu.

Mhe. Spika, kama inavyofahamika kuwa dhumuni la kuletwa mswaada huu ni kuidhinisha Makadirio na Matumizi ya Fedha zote zilizopitishwa katika Baraza hili tukufu katika Bajeti ya Mwaka huu wa Fedha 2015/2016 ili kuruhusu utoaji na uhaulishaji wa fedha hizo kwa ajili ya matumizi yaliyopangwa katika programu mbali mbali.

Mhe. Spika, tunaiomba sana serikali kupitia Wizara ya Fedha baada ya Rais kusaini mswada huu na sheria itakapoanza kutumika katika bajeti ya mwaka huu inayozingatia mfumo mpya wa *Programme Based Budget (PBB)*, ihakikishe kuwa matumizi ya fedha yanafanyika kama yaliyoidhinishwa na kupitishwa katika chombo hiki ili kuhakikisha kuwa fedha za umma zinatumika kama zilivyoidhinishwa na Baraza lako tukufu kwa maslahi ya wananchi.

Mhe. Spika, naomba nitumie fursa hii kuwakumbusha wale wote waliopewa dhamana ya kusimamia mafungu ya fedha katika bajeti ya mwaka huu kuwa mfumo tulioanzisha sasa hivi wa bajeti upo wazi sana kwani kila fedha imeoneshwani kwa namna gani itatumika katika bajeti ya mwaka huu. Kwa hivyo, basi, matumizi ya fedha hizo yawepo wazi kama yaliyyooneshwa katika vitabu nya bajeti ili kuweka matumizi mazuri ya fedha za umma.

Mhe. Spika, kamati yangu inaanini kuwa licha ya ufinyu huu wa bajeti tulionao, lakini kama matumizi ya fedha yatafanyika kwa kuzingatia sheria zinazohusiana na masuala ya fedha, basi mabadiliko makubwa yataonekana. Lakini pamoja na kuhimiza matumizi mazuri ya fedha za umma kwa kuzingatia sheria, pia ipo haja ya kuangalia thamani ya fedha (*value for money*) katika matumizi ya fedha zetu ili tuone kwamba fedha za walipa kodi zinatumika kwa mujibu wa thamani ya kilichofanyika.

Mhe. Spika, ni imani yetu kwamba kwa kuwa serikali imekuwa na nia njema ya kuanzisha mfumo huu mpya wa bajeti, kutakuwa na mabadiliko makubwa sana katika matumizi ya fedha za umma kwani kutakuwa na uwazi wa matumizi, lakini pia utawasaidia sana Wajumbe wa Baraza hili urahisi wa kuihoji serikali juu ya matumizi ya kila fedha iliyoidhinishwa katika chombo hiki na matokeo yanayotegemewa katika kila programu yaonekane.

Mhe. Spika, kwa kumalizia hotuba hii naomba sana kutoa pongezi kwa Wajumbe wote wa Kamati ya Wenyevitii kwa mashirikiano makubwa tunayofanya kwa umoja wetu kwa kipindi chote cha miaka mitano ambacho Mwenyekiti wetu Mhe. Hamza Hassan Juma alikuwa akituongoza.

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba vile vile niwatambue Wajumbe wa kamati hii kama hivi ifuatavyo:

1. Mhe. Hamza Hassan Juma	-Mwenyekiti
2. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-Mjumbe
3. Mhe. Mahmoud Mohammed Mussa	-Mjumbe
4. Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	-Mjumbe
5. Mhe. Omar Ali Shehe	-Mjumbe
6. Mhe. Hija Hassan Hija	-Mjumbe
7. Ndg. Khamis Hamad Haji	-Katibu
8. Ndg. Salum Khamis Rashid	-Katibu

Mhe. Spika, baada ya maelekezo hayo nawaomba Wajumbe wenzangu tuipokee ripoti hii ambayo ni ya mswada huu wa mwisho, tuijadili na hatimae tupitishe ili tuweze kumpa uhalali Mhe. Waziri wa kwenda kufanya kazi ambayo tunaitarajia iweze kufanyika kwa ajili ya kuwaleta maendeleo wananchi wetu wa Zanzibar. Wajumbe nyinyi mliobakia hapa ndio wenye dhamana na wenye uhakika wa kuendeleza maendeleo ya nchi hii, naomba nyote kwa umoja wenu kwa kushirikiana na mimi tuhakikishe kwamba bajeti hii inapita na hatimae tunafanya yale ambayo tumeyalenga. Wale wananchi wenzangu naomba kwa ujumla wao na wao washirikiane nasi na kuunga mkono bajeti hii. Kwa niaba yangu Mhe. Spika, na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni tunaunga mkono asilimia mia kwa mia ili tumalize kazi hii tumkabidhi Mhe. Waziri wa Fedha, akafanye kazi kwa niaba ya wananchi. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofit*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Mahamoud, tunakushukuru sana kwa kutoa maoni ya Kamati ya Wenyeviti kwa niaba ya Mwenyekiti. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Hamza Hassan Juma.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Spika, kwanza nakushukuru kunipa nafasi hii ya mwanzo kuweza kuchangia hotuba ya Mhe. Waziri, kuhusu Mswada wa Fedha ambaao ametuomba tumuidhinishe kiasi cha Shilingi Bilionti Mia Nane na Thalathini, Laki Tatu na Sitini na Mia Tatu ili serikali iende ikatoe huduma kwa wananchi.

Mhe. Spika, mimi kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura na nitawaomba sana Waheshimiwa wenzangu wa majimbo mengine ambaao wameletwa hapa kwa kupigwa kura ili serikali iweze kutoa huduma kwa wananchi, basi nawashawishi tukubali maombi haya ya Mhe. Waziri, ili fedha hizi ziende zikatoe huduma kwa wananchi.

Mhe. Spika, kwanza kabla sijaingia katika mchango wangu nilikuwa nataka niseme jambo dogo sana. Katika Baraza letu hili tumeshudua Katiba ya Zanzibar ikikiukwa karibu mara tatu, kwa kweli jambo hili si jambo zuri sana hasa katika nchi ambayo inafuata utawala bora.

Mhe. Spika, Katiba ya Zanzibar kifungu cha 43(5) kiko wazi sana kinazungumzia suala la uajibikaji wa mawaziri ndani ya Baraza la Wawakilishi. Namuomba sana Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, najua pamoja na kwamba ye ye hayupo lakini yupo kwa sababu *Hansard* itaendelea kuwepo na Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, yupo tunaomba kilio chetu hiki akipeleke kwa Mhe. Rais.

Mhe. Spika, Katiba ya Zanzibar Ibara ya 43(5) inasema;

"Mawaziri watawajibika kwa pamoja mbele ya Baraza la Wawakilishi chini ya Makamu wa Pili wa Rais."

Mhe. Spika, mimi nilitegemea kauli ile aliyoitoa Mhe. Juma Duni Hajji, ambaye kwa sasa hivi eti anaitwa Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano kauli ile angeliitoa *back bencher* kutoka Chama cha *CUF*, lakini wewe leo umo ndani ya serikali, mipango inayopangwa ndani ya serikali umo, kwenye Baraza la Mapinduzi Ikulu unaingia, unapiga chapati, unapiga sambusa, unapiga kuku na posho, halafu unafanya unafiki unapotoka Ikulu ukija huku unawadanganya wananchi.

Mhe. Spika, namuomba sana Mhe. Rais ameshawastahamilia sana kama kula washakula, naomba kwa kitendo kilichofanywa leo mawaziri kuikana serikali ndani ya Baraza la Wawakilishi, wamekiuka Katiba ya Zanzibar kifungu 43(5). (*Makofi*)

Mhe. Spika, mawaziri wote pamoja na manaibu mawaziri kutoka Chama cha *CUF* wafukuzwe kazi na viti viwe wazi. Sisi tulipoingia kwenye Baraza hili ultupa vitu vitatu, ultupa Katiba ya Zanzibar, Katiba ya Jamhuri ya Muungano na Kanuni za Baraza la Wawakilishi. Sasa leo haiwezekani nondo zile ulizotupa leo zinakiukwa hapa hapa hadharani mchana kila mtu anaona halafu suala hili linafumbiwa macho, haiwezekani. (*Makofi*)

Mhe. Spika, hata kama Mhe. Rais hajatamka kuwafukuza kazi Katiba ya Zanzibar wale wameshajiondoa kwenye nafasi za uwaziri. Kwa hiyo, naomba sana serikali, namuomba sana Mhe. Rasi leo funguo zetu tuletewe za SMZ, wapande gari zao wende wakafanye kampeni.

Mhe. Spika, mimi najua ulipokuwa *European Union* na kwa bahati mbaya safari hii hukunichukua, maana yake na mimi leo ile *speech* uliyoitoa kule na mimi ningeitafsiri hapa. Mhe. Spika, najua uliulizwa sana mfumo huu nyinyi mnaendeshaje, mnaongoza halafu watu wanakupingeni mmo humo humo ndani?

Mhe. Spika, siku zote tunasema mfumo tuliokuwanao Zanzibar wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa haupo dunia nzima, matokeo yake ndio haya. Hawa watu ambaio unawapanga kuja kuleta hoja zako ndio wale wale wanaokuja kuvunja hoja zako, hatuwezi tena kustahamili masuala kama haya.

Mhe. Spika, nikiondoka hapo nataka niende katika mchango wangu. Mimi nawaomba Waheshimiwa Wajumbe leo hoja hii tuichangie sote, tuichangie sote kwa sababu gani? Kwa sababu hapa kila mmoja kapewa kilio kutoka jimboni kwake wananchi wangu hawana maji, wananchi wangu hawana umeme, wananchi wangu hawana madawa, wananchi wangu hawana barabara.

Mhe. Spika, kama hatujaidhinisha matumizi haya hayo maji atahudumia nani, barabara atajenga nani, fedha zenyewe ndio hizi, hiyo mishahara pamoja na hawa jamaa waliotoka humu ndani mishahara yao imo katika bejeti hii katika fedha tutakazoozidhinisha. Sasa leo unataka kama *quorum*, kwa sababu wao walitegemea wakitoka wao *quorum* haitimii wamechelewa, wamechemsha, imekula kwao. Sisi tutapitisha na fedha tutaziruhusu kwa serikali iende ikahudumie mambo ya maji, mambo ya afya, mambo ya kilimo na kila kitu.

Kwa hiyo, naomba Waheshimiwa Wajumbe, kila mmoja ni Mjumbe wa Kamati katika wizara aangalie katika mambo ya msingi achangie na amuombe waziri aruhusu fedha zile ile wananchi ziende zikawahudumie.

Mhe. Spika, nitaanza mimi, katika jimbo langu la Kwamtipura nina mradi wa mtaro siku nyingi, miaka mingi wananchi wangu kila zikija mvua wanazama. Namshukuru sana Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, Mtumbatu wa juu na mimi Mtumbatu wa chini, Mchaani.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri, ameshakubali kwamba kuanzia mwezi huu wa sita na mwanzoni mwa mwezi wa saba mtaro ule utaanza kujengwa. Sasa leo kama fedha hizi hatukuziruhusu ule mtaro utajengwa kule? Mtaro ule nataka niseme wanaozama na *CUF* wamo. Hivi juzi ilipotokea ghariki ya mvua katika watu tuliokwenda kuwapa misaada na *CUF* wamo. Sasa leo hao Wawakilishi wao waliowaleta humu wameshakimbia, sasa ile dhahama atawaokoa nani, dhahama ile nitaiokoa mimi Mwakilishi wa jimbo la Kwamtipura kutoka tiketi ya CCM ili fedha ziidhinishwe tukajengewe mtaro. Na mimi naomba Mhe. Waziri uwe na ari, tunataka sasa hivi muwaoneshe ari wananchi kwamba wao wametoka sisi baada ya kuidhinisha fedha hizi majimbo yote shughuli zianze kufanywa, tena Mhe. Waziri, katuomba hapa akakope shilingi 30 bilioni.

Mhe. Waziri, tukimaliza tu ile tarehe 31 Julai ikiingia tarehe mosi nenda kakope zote, kakope usisubiri za kukusanya tupate kuhudumiwa. Kuna barabara nyingi hazijajengwa, mimi nina kibarabara changu siku zote cha Kwa Abasi

Hussein/Mboriborini fedha ziko Mfuko wa Barabara kama sikuidhinisha fedha hizi barabara ile itamalizwa, haiwezekani. Sasa hao wenzetu kama wametufanya usanii leo, usanii huu utawarejea wao.

Mimi nashangaa sana. Mhe. Subait Khamis Faki, katika hao watu sikutegemea angelitoka humu ndani ya Baraza ni Mhe. Subeit Khamis Faki. Mhe. Subeit, ye ye ndiye anayelalamika wananchi wangu wa Micheweni masikini, sijui hawana kitu gani, kuna fedha nydingi ambao zimeidhinishwa kwa ajili ya kwenda kuhudumia Micheweni, ni vitu vya kushangaza, yaani hawa jamaa, tena mimi nawaomba sana wananchi hawa *CUF* hawafai na mfano ndio huu.

Mhe. Spika, leo wanatudhihirishia udhaifu wao waroho. Mimi huwa sipendi sana kumsema lakini leo itabidi nimseme maana kawatuma hawa, Maalim Seif Sharif Hamad mwaka 1995 aliranda dunia nzima kwenda kuomba Zanzibar isipewe misaada, tena mimi nashangaa watu wanakwenda nje kuomba misaada kwa nchi zao, ye ye alikwenda dunia nzima kuizua misaada Zanzibar, watoto wetu wengi walikosa chanjo katika kipindi kile, hawa watoto ambao wenye miaka 15, 16 wenye ulemavu chanzo kikubwa ni Maalim Seif Sharif Hamad, kwa sababu ye ye ndiye aliyekwenda kuomba Zanzibar isipewe misaada, leo Zanzibar uchumi wenywewe hakuna halafu unakwenda kuzuulia misaada.

Mhe. Spika, unajua hawa leo wangelifanya vituko hivi pale mwanzo mwanzo pangekuwa patamu sana hapa, maana tungkuwa kila bajeti tunawatolea mifano.

Mhe. Spika, barabara zinazojengwa sasa hiviu Pemba, barabara ya Gando, barabara ya Mtambwe, barabara zile zilikuwa zijengwe kwenye mwaka 1996/1997 na fedha tayari Benki ya Dunia ilikwisha idhinisha. Baada ya Zanzibar kuzuwiwa misaa zile zililala, leo hapa wawakilishi wao ooo, sijui barabara ya pi. Leo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar baada ya miaka 10 kwenda kupiga magoti kuwabembeleza wakubwa wafadhili duniani fedha zile tumezipata sasa hivi angalau barabara ya Gando mtu unakwenda bila ya matatizo, barabara ya Mtambwe unakwenda bila ya matatizo na barabara nyengine. Leo baada ya kuona kwamba kumbe Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kila kukiwa na amani na utulivu ndio inapiga hatua kubwa za maendeleo, wameamua sasa kuanzisha vurugu ili wafadhili warudi tena watuzuwie misaada ili tukwame.

Mhe. Spika, hapa hatukwami, lakini kuna siri imefichika nyinyi hamujui. Waswahili wanasema; "Ukimuona nyani kapea ujue amekwepa mikuki mingi", katika nyani waliopea na mimi nimo. Hawa sisi tunawasikiliza sana.

Mhe. Spika, tunaposema Dokta Ali Mohammed Shein alipoingia serikali ilikuwa inakusanya shilingi 13 bilioni kwa mwezi walifurahi sana, wakasema aa pesa hizi, sasa kila mwaka Mhe. Waziri wa Fedha, akija anasema mapato yanaongezeka,

kutoka shilingi 13 bilioni sasa hivi Dokta Ali Mohammed Shein anakusanya shilingi 35 bilioni, tumbo linawauma. Hapa hatujachimba gesi na Mhe. Rais keshasema keshokutwa Katiba mpya ikipita kitu cha mwanzo anaanza kufunga mikataba ya gesi na mafuta watu waje wachimbe.

Mhe. Spika, shilingi 830 bilioni hatujachimba gesi, hatujachimba mafuta, hatujaanza kuza vitalu nya mafuta na gesi; leo kabla ya kuanza kuchimba tukianza kuza vitalu, zile *blocks*, wakija tu fedha nyingi zitapatikana kila kisima hatutokosa Trilioni moja.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar tangu Mapinduzi bajeti yetu haijawahi kufika Trilioni moja, lakini leo tukianza kuchimba gesi na mafuta bajeti ya mwanzo inayokuja mwaka 2016/2017 tutaanza kuzungumzia bajeti ya Zanzibar Trilioni moja na kuendelea mbele. Maana yake nini, mishahara itaongezeka, madawa yataongezeka, hospitali zitaongezeka, huduma za afya zitaongezeka kila kitu kitaboreka. Sasa haya wameshayaona na Mhe. Waziri wa Fedha na yeze siri nyengine azifiche.

Jana baada ya kuwaambia utatupeleka maeneo huru kwenda kuona mipango ya maendeleo jamaa wameona choyo hawa, yaani wanaona kumbe hii Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ndio mambo yake haya, kumbe tukimaliza uchaguzi wanaleta mambo makubwa zaidi. Mhe. Waziri wa Fedha jana alimaliza kila kitu, Dokta Shein hana kazi kwenye kampeni, tena naomba bora wewe ndio uwe *campaign manager* safari hii.(Makof)

Mhe. Spika, kutia saini bandari ya Mpigaduri ni ukombozi mkubwa kwa Afrika, kwa Afrika Mashariki lakini zaidi kwa Zanzibar. Haya yanawauma, hawa wanavyokusudia watoke wende wakaanzishe vurugu wakishaanzisha ina maana tugombane fedha tusizipate na wahisani waje kuzuua misaada ili hayo mambo tuliyotia saini yasipatikane.

Sasa la mwisho kabla hujaniambia kwa sababu nishaanza kukuona unaangalia dakika zangu tano. Mwisho kabisa ninaloliomba unajua sina amri ya Kamishna wa Jeshi la Polisi, lakini ningelimwambia gari za wanaojiita mawaziri wa CUF kuanzia leo zisiingie Ikulu, kama wametoka humu ina maana wameikimbia serikali na serikali imo wamemkimbia Makamu wa Pili wa Rais, Ikulu wanakwenda kufanya nini. Hawa wameshazowea kupiga debe kule Darajani, waache wakakusanyike Darajani, Mtendeni wakapige debe, serikali watuachie wenywewe tumalize shughuli.

Mhe. Spika, mimi nimefurahi sana kwa sababu tulipopitisha Katiba mpya wewe ulikuwa shahidi, sio Katiba mpya ila marekebisho ya kumi ya Katiba, kipindi kile Dokta Amani Abeid Karume alipokuwa anatushawishi tukubali marekebisho ya

kumi ya Katiba kuanzisha Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Alisema kutakuwa na amani na utulivu, mambo ya ugomvi kutakuwa hakuna, tutaendesha serikali kwa pamoja na mambo yetu yatakwenda vizuri. Sasa hii leo kuanza kutususa dakika za mwisho ndio uzuri wenyewe huu? Kwa hiyo, ina maana wamemdanganya mpaka Dokta Karume, walikwenda kule kina Mhe. Ismail Jussa na wenzake kamati yao ile pamoja na wengine wakenda wakamshawishi Dokta Amani Abeid Karume akakubali Serikali ya Umoja wa Kitaifa, leo matokeo yake ndio kama hivi wanansasa.

Mhe. Spika, naomba sana wao wenyewe wameshatangaza kwamba wameshindwa kuimaliza Serikali ya Umoja wa Kitaifa, wamejimaliza wenyewe sasa kazi iliyobakia kama tulivyokubaliana kwenye Katiba baada ya miaka mitano wananchi waulizwe tena. Haya sitoi mimi, haya ndio tulivoambiwa jamani hebu tujaribuni twende kwa majoribio, baada ya miaka mitano twende tukawaulize wananchi. Sasa wananchi kwa muda wa miaka minne hii ilikuwa inakwenda vizuri kila unapopita wanapongeza, lakini ulipoingia huu mwaka wa tano mambo yameharibika na sasa hivi hawa jamaa wameshindwa, hii Serikali ya Umoja wa Kitaifa ina joto jamaa wameshatoka.

Sasa kama wameshatoka watarudi kwa njia gani? Sisi kazi yetu tukafunge mlango na kufunga mlango ni kufanya marekebisho ya Katiba, laiti ingelikuwa muda unatosha ningelileta hoja binafsi ya kufanya marekebisho makubwa ya Katiba ya Zanzibar na ninaomba Mwanasheria Mkuu aje anisaidie hapa kwa muda tuliokuwanao. Dokta Jakaya Mrisho Kikwete ameliongezea Bunge siku 10 kwa ajili ya kupeleka ile miswada muhimu. Sasa je, leo Zanzibar Mwanasheria Mkuu serikali yetu haiwezi kutuongezea japo siku tano? Siku tano tu, tunarekebisha Katiba. Mhe. Spika, tunamuomba Mhe. Waziri wa Fedha kwa sababu bajeti hii sasa hivi ndio tunamaliza, anakunuta hana kitu tutamkopesha au tutapiga bure sadaka, ili tuweze kuweka mambo sawa, wananchi wameshachoka kubabaishwa.

nakushukuru baada ya kunipa hiyo nafasi, kwa hayo machache kwa niaba ya wananchi wangu wa jimbo la Kwamtipura naomba sana, sisi tunaiunga mkono bajeti hii iende ikawahudumie wananchi, lakini kama nilivyowaomba wenzangu wachangie kila mmoja katika jimbo lake lenye matatizo aruhusu fedha hizi ili aende akatatte matatizo yake katika jimbo la Kwamtipura. Laiti kama ingelikuwa fedha za Mfuko wa Jimbo hawajazichukua wale Mhe. Spika, wala usingewapelekea, kwa sababu wanakataa sasa mtu anakataa bajeti tena anataka nini.

Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii naunga mkoo hoja. Ahsante sana.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Spika, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia kukutana hapa leo, lakini pili nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii ili na mimi kuchangia Mswada huu wa Mhe. Waziri wa Fedha kwa kuupitisha zile pesa ambazo alizoomba wakafanye matumizi.

Mhe. Spika, kwa kuanzia naomba nimpongeze Mhe. Waziri kwa kazi nzuri anayoifanya, lakini shukurani za pekee ziende kwa Katibu Mkuu na watendaji wengine kwa kumsaidia Mhe. Waziri kwa kufanikisha kazi zake.

Mhe. Spika, kwa ujumla niwapongeze sana Mawaziri kwa upande wa CCM ambao wamesimama hadi leo kuona kwamba wanatetea maslahi ya wananchi na wananchi wanapata yale ambayo yanastahiki kuyapata. (*Makofii*)

Mhe. Spika, maneno uliyozungumza, kwanza niseme sina sikitiko kwa sababu kitendo ambacho kimefanywa kwa makusudi, mimi sina haja ya kusikitika ninawashangaa wenzangu wanaosikitika. Mhe. Spika, lakini maneno uliyozungumza baada ya tokeo lile lililotokea ni mazima sana kwa mtu ye yote ambaye ana akili timamu, kukaa kitako na kuyatafakari na kutambua nani ana nia njema na nchi hii na nani hana nia njema na nchi hii. (*Makofii*)

Mhe. Hamza Hassan Juma, naye amezungumza maneno mazima zaidi na Wazungu wanasema Mhe. Spika; "*spare the road, spoil the child*". Mhe. Spika, tumekuwa tunalea vitendo hivi si mara moja wala si mara ya pili na sasa mtoto ameharibika.

Mhe. Spika, Mhe. Hamza, amependekezo mapendekezo mengi sana na mimi naomba wale ambao wanaohusika wakae chini watafakari mapendekezo yale na wayafanyie kazi, maana siyo kutafakari tu lakini pia yafanyiwe kazi. (*Makofii*)

Mhe. Spika, Waswahili wanasema; "Ukicheka na nyani atakufuata mpaka Msikitini". Wamezoea kufanya haya na Serikali bado inawanyamazia kimya wanatazamwa na ndiyo maana wanaendelea kuyafanya haya, kwa sababu wanaona hamna watakalofanywa, lakini niseme tu Mhe. Hamza, amezungumza vizuri sina haja ya kuyarudia. Ni vyema yale ambayo ameyazungumza ninarudia kwa mara nyengine tena yafanyiwe kazi. (*Makofii*)

Mhe. Spika, walitaka tuvunje Katiba hapa na Mhe. Hamza, amesema leo wamevunja Katiba, lakini siyo mara ya kwanza kama nilivyosema, mara ya kwanza walileta hoja binafsi kututaka tuvunje Katiba hapa katika Baraza lako. Lakini kwa nguvu tuliyokuwa nayo Wawakilishi wa CCM tulikataa na hoja ile Mhe. Spika, haikupita. Sasa Mhe. Spika, niwaombe Wawakilishi wenzangu wa CCM tumezoea kuchezeshwa ngoma ambayo sio yetu na sisi tunaingia tunafunga vibwebwe tunacheza. (*Makofii*)

Mhe. Spika, tuvve vibwebwe vyao na ngoma yao waicheze wenyewe. Hili la Katiba halikuwa la kwanza lakini pia hili la *GNU* lilikuwa lao wenyewe. Sasa Mhe. Spika, Mhe. Hamza, alisema kwamba kule *AU* wanatushangaa tunaendeshaje Serikali hii. Mimi ninashukuru nilipata nafasi ya kwenda pamoja na Mhe. Spika na niliona jinsi gani wanavyoshangaa. Lakini sikushangaa wao kutushangaa kwa sababu *United Kingdom* wenyewe limewashinda, wanashangaa sisi Waswahili tunaliwazaje. Sasa kama Mzungu limemshinda Mhe. Spika, ujue Mswahili hatuliwezi, tulivueni. (*Makofî*)

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo niwaombe Wawakilishi wenzangu wa CCM na niiombe Serikali kwa ujumla tukae chini tufikirie na tena tufikirie mara mbili, Mzungu anasema, "*Think twice*", haina haja ya kulinda Serikali hii kama haina maana na kama hii mbili imeshindwa basi turudi kule kule kwenye moja; kama hii Serikali ya Umoja wa Kitaifa imeshindwa ya kutunganisha, turudi kwenye ule ule mfumo wa kwanza tuendelee nao. Maana hili ndiyo limeshashinda tupo peke yetu, wao wameshatoka. Kwa hivyo, haina haja na kama nilivyosema tukae chini tufikirie mara mbili, tuone kwamba lile ambalo lina maslahi na nchi hii na tumechoka kucheza ngoma si zetu na sasa tushavua vibwebwe, tunataka tuchaze ngoma ambazo ni zile zetu wenyewe. (*Makofî*)

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo niunge mkono yale yote ambayo Mhe. Hamza, amezungumza na yale ambayo amependekeza katika Mswada huu yafanyiwe marekebisho na ninayaunga mkono. (*Makofî*)

Mhe. Spika, mimi nikiingia kwenye Mswada huu nina maeneo machache tu ya kuchangia.

Kwanza katika ukurasa wa 13 kwenye Fungu H02, neno "Hospitali ya Mnazo Mmoja", lisomeke "Hospitali ya Mnazi Mmoja".

Lakini pia Mhe. Spika, katika ukurasa wa 14 kwenye jadueli *column* ya pili, neno "Huduma za ustwawi wa jamii", lisomeke "Huduma za ustawi wa jamii".

Baada ya kusema hayo Mhe. Spika, ninaunga mkono Mswada hu na ninawaomba Wawakilishi wenzangu waunge mkono ili Serikali yetu hii ikafanye matumizi ya fedha hizi kama vile ambavyo Mhe. Hamza Hassan Juma, amependekeza.

Mhe. Spika, ninaunga mkono. (*Makofî*)

Mhe. Spika: Ahsante sana. Ninakushukuru sana Mhe. Wanu Hafidh Ameir, kwa mchango huo na kuunga mkono hoja.

Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Mussa Ali Hassan, wakati wengine bado wanajitayarisha. (*Makofî*)

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Spika, kuweza kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia bajeti hii ya Waziri wa Fedha.

Kwanza sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha hapa tukiwa wazima wa afya, tukiendelea na shughuli zetu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sisi Wawakilishi wa Majimbo wa Chama cha Mapinduzi tunaiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia juu ya mia, kuhakikisha kwamba tunakwenda majimboni kufanya kazi zile ambazo zinawasumbua na zinawapa matatizo wananchi ili wapate maendeleo ambayo tumeyataraja. (*Makofî*)

Mhe. Spika, pindi tukiwa hatukuweza kuitishaa bajeti hii, hao watakuwa ni wasaliti wa wananchi, kwa sababu wananchi wetu ndiyo wanategemea kwamba bajeti hii itawaokoa katika maisha yao ili kuhakikisha kwamba maendeleo tuliyokuwa tumeyazungumza kwa muda wa miaka mitano, hivi sasa yanafikia kikomo ili wahakikishe kwamba maendeleo tuliyochangia hivi sasa yanarudi kwa wananchi ili kupatiwa huduma ambazo walizitegemea.

Hivi sasa majimboni kuna matatizo makubwa sana ambayo tuliyategemea kumaliza pindi tukiunga mkono bajeti hii hasa kutokana na hali ya barabara zetu zilivyokuwa chakavu pamoja na skuli zetu ambazo chakavu, maendeleo ya maji ambayo tunapiga kelele kila siku ambayo sehemu nyngi za majimbo yetu zina matatizo ya maji.

Mhe. Spika, kweli ni kwamba tukiwa hatukiunga hii bajeti ni sawa kuwa sisi ni wachochezi wa wananchi ili wafanye ghasia kwa sababu hawana maendeleo ya nchi hii.

Mhe. Spika, mimi na wananchi wangu wa Jimbo la Koani ninahakikisha kwamba bajeti tunaiunga mkono ili kuhakikisha yote ambayo tuliyazungumza kwenye Baraza hili yanapita na kuweza kuhakikisha tunayafanyia kazi kwa wakati. (*Makofî*)

Mhe. Spika, ninawashangaa wenzetu wa Chama cha Upinzani *CUF* kwamba kila siku wao ndiyo wa kwanza kutaka maendeleo, kuwa nchi yetu iwe na maendeleo na kusema kwamba nchi hii ina matatizo kwani haina maendeleo, leo tunatengeneza maendeleo ni wa kwanza kutoka nje ya jengo ili kuona maendeleo yale yasipatikane kwenye nchi yetu. Sijui Mhe. Spika, watu hawa tuwaeleweje ama tuwaiteje. Mimi ninawaita hawa watu ni muhangi wa Chama cha Mapinduzi. (*Makofî*)

Mhe. Spika, kwa kweli hawaitakii mema Serikali yetu inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi. Ninamuomba Mhe. Rais avunje mara moja Serikali ya Muungano ili tuhakikishe Serikali inayoshinda ndiyo inayoongoza dola ili iweze kuipangia maendeleo yake kwa wakati. Hii Serikali ya Umoja wa Kitaifa imeturejesha nyuma sana, tulitegemea kwamba tutafika katika maendeleo ya kuwa tunahakikisha tunapata maendeleo. Lakini yote ambayo tuliyategemea Mhe. Spika, yamerudi nyuma, tumeshuhudia vifo vingi vya wananchi vimetokea kiholela, kuripua masuala mengi baada ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa kuwepo.

Mhe. Spika, kwa kweli Serikali ya Umoja wa Kitaifa haitusaidii lolote na hatimaye yake ivunjwe mara moja, Serikali inayoshinda iweze kuongoza dola ya nchi hii ya Tanzania Zanzibar. (*Makofî*)

Mhe. Spika, sisi Wawakilishi wa Majimbo tunaitetea bajeti hii ili ihakikishe kwamba leo hii inapitishwa ili tarehe 1 Julai kuwa tunaweza kufika katika maendeleo kwenye majimbo yetu na kuhakikisha majimbo yote ya Zanzibar yanapata maendeleo kutokana na bajeti hii ambayo tunaipitisha hivi sasa. (*Makofî*)

Mhe. Spika, kwa kweli mimi sitokuwa na mchango mwangi isipokuwa tu namuomba Mhe. Rais kwa mara ya tatu akae na Serikali yake ili kuona kwamba Serikali ya Umoja wa Kitaifa hakuna maendeleo yaliyopatikana isipokuwa Serikali iliyopita kwamba ni wale ambao wanapata Serikali ndiyo waongoze dola hii na waweze kupanga maendeleo yetu.

Mhe. Spika, ninaiunga mkono bajeti hii kwa asilimia mia kwa mia pamoja na wananchi wangu wa Jimbo la Koani.

Mhe. Spika, ahsante sana. (*Makofî*)

Mhe. Spika: Ninakushukuru Mhe. Mussa Ali Hassan. Tumkaribishe basi Mhe. Panya Ali Abdalla, afuate baadae Mhe. Shadya Mohamed Suleiman, wakati Mhe. Nassor Salim Ali, anajitayarisha.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Spika, ahsante sana, awali ya yote sina budi na mimi kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subuhana Wataalla* ambaye ametujaalia asubuhi hii tukaweza kufika hapa katika Baraza lako Tukufu na kuendelea na majukumu yetu. Lakini pia nichukue fursa hii kwa wewe Mhe. Spika, kunipa na mimi nafasi hii ili niweze kuchangia machache na kuunga mkono hoja hii ilio mbele yetu. Pia, nichukue fursa hii kumshukuru sana Waziri wa Fedha na watendaji wake wote kwa kazi ngumu na kubwa, lakini wameweza

kuiwasilisha kwetu na inaonekana matumaini mazuri ambayo yataweza kujenga nchi yetu katika misingi mizuri. (*Makofî*)

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein ambaye ni Rais wetu wa Zanzibar. Mhe. Spika, ninampongeza Dkt. Shein kwanza kwa ukomavu wake wa kisiasa; Dkt. Shein amekomaa kisiasa na amekuwa ni ngome kwetu sasa na inaonekana anayekwenda na ngumu anaumia yeze mwenyewe mkono wake. (*Makofî*)

Mhe. Spika, ninataka niungane na Mhe. Hamza Hassan Juma, kwa utangulizi wake wa maneno aliyojasema, kwa kweli amemaliza kila kitu katika michango yetu, amesema mengi na ni kweli. Baada tu ya kitendo kile wewe mwenyewe maneno uliyoyasema ni ya hekima na busara kubwa na siku zote tumeshuhudia busara hii ukiitumia katika kutuongoza, lakini walionekana wenzetu walivyo kwa kweli ilikuwa hawana nia safi, iliyochokuwa kinatusaidia ni busara yako na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu akuzidishie busara hizo na hekima uweze kuendelea kutuongoza, tunakuamini sana. (*Makofî*)

Mhe. Spika, wenzangu hapa wamesema na wakashangaa na mimi ninashangaa, na ushangaa nilianza kuushangaa tangu kwenye Bunge la Katiba. Kwa sababu wao kwenye Bunge la Katiba walikuwa wakilalamika sana hapa, tunataka mafuta, gesi lakini sasa tunakwenda kuitafuta hiyo gesi ituhalalikie, wao ndiyo waliotoka katika Bunge lile. Nilishangazwa sana na nilijua mimi wangelitoka *back beachers*, lakini kutoka Mawaziri ni kitendo ambacho mimi kimenishangaza zaidi. (*Makofî*)

Kwa sababu wao ni Serikali, wao wana sehemu kubwa kabisa kuliko hawa Wawakilishi. Leo kitendo kile cha wao, mimi nilijua kule wanaweza wakatoka *back benchers* lakini Mawaziri kwa kuwa wamechukua viapo viwili, wao wangelibaki. Lakini leo pia tunashuhudia mfano mwengine Waziri ndiye aliyesimama hapa na kutoa hoja ile kuwashawishi wenzake watoke, hatuwezi kuwa na viongozi wasioaminika. Kuwa na kiongozi usioaminika na hatuwezi na viongozi ambao si waaminifu, wewe umeshabeba jukumu la kuwaongoza wananchi wako na hapa umepewaa jukumu jengine la kuongoza Serikali. Sasa wewe mwenyewe unapokuwa ndiyo kinara, ni vitu ambavyo vinatusaabisha na vinataka vifikirie kama wenzangu walivyotoa michango yao.

Mhe. Spika, hii yote inatokana na nyimbo ya kufundishwa, siku zote nyimbo ya kufundishwa haikeshezi ngoma, lazima katikati ama ubeti utasahau, hao ndivyo walivyo, haya yote wanapandikiziwa, leo kafanyeni hivi, kesho kafanyeni hivi, matokeo yake ndiyo haya tunayaona. (*Makofî*)

Mhe. Spika, akili za kuambiwa siku zote lazima na wewe uchanganye na zako, na busara inahitajiwa sana, ukishaitwa kiongozi vitu hivi vya busara na hekima, si kila unalopewa ulichukulie uamuzi tu, lazima ufikirie kama hili ninalolifanya ni hakika.

Mhe. Spika, leo tupo katika Wizara hii ya Fedha ambayo ndiyo tunayoitegemea kwamba wizara zote ili yaweze kufanya kazi ambazo Wawakilishi wote hapa tulipokuwa tunapitisha bajeti moja moja, tulikuwa tumeomba mambo yetu tofauti kwenye majimbo yetu na mikoa yetu ambapo sasa tunataka tumwambie Mhe. Waziri, tunakuruhusu fedha hizi ifikapo muda uruhusiwe kuzitumia, leo tunatoka halafu tunasema sisi ndiyo tunawapenda wananchi wetu. Hili linatuonesha sahihi kama watu hawapo tayari kuwasaidia wananchi na watu wapo zaidi kimaslahi yao. (*Makofî*)

Mhe. Spika, mimi niiombe sana Serikali kwa haya ambayo wametueleza na sisi maombi yetu ambayo tulyapeleka katika Mawizara mbali mbali ambayo tulikuwa tukichangia michangio yetu yaweze kufanyiwa kazi kwa maslahi ya wananchi, yaweze kufanyiwa kazi kwa vizazi vyetu vijavyo.

Mhe. Spika, vilio vingi viro mitaani kwetu; kuna kilio cha maji na umeme kwa sehemu ambazo hazijafika na ili viweze kufika basi lazima tumruhusu Mhe. Waziri wa Fedha, tumuidhinishie fedha hizi ili Wizara zote ziweze kufanya kazi ya kuwafikishia huduma mule ambamo bado hazijakamilia kufika.

Mhe. Spika, mimi kwa upande wangu nilikuwa na ombi dogo na wala siyo dogo, maana yake linaleta athari sana katika Mkoa wangu, niiombe Serikali sana iwe makini na naomba ikaangalie hasa yale madaraja yetu ambayo yamevunjawna vunjwa vibaya na sasa ajali za gari ikitokea inakuwa si ndogo tena. Kwa sababu gari inaingia moja kwa moja kwenye daraja. Sasa niiombe Serikali ikae chini juu ya hili ifikirie utaratibu gani itaweza angalau inapotokea ajali basi isiweze kuwa kubwa kiasi hicho cha kuweza kuumiza watu vibaya sana.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo kwa imani yangu na kwa imani ya wanawake wote wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, ninasema ninaunga mkono Mswada huu wa kuidhinishwa makisio ya matumizi ya Shilingi Bilioni Mia Nane na Thalathini, Mia Tatu na Sitini Milioni na Laki Tatu kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina, tunamruhusu Mhe. Waziri wa Fedha aweze kutumia fedha hizo muda utakapofika ili wananchi wetu waweze kupata mahitaji mbali mbali ambayo tumeeleza katika bajeti mbali mbali zilizopita. (*Makofî*)

Mhe. Spika, ninakushukuru. (*Makofî*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Panya Ali Abdalla, kwa mchango huo na hatimaye kuunga mkono hoja. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Shadya Mohamed Suleiman, afuate baadae Mhe. Nassor Salim Ali na Mhe. Mlinde Mbarouk Juma, anajitayarisha.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Ahsante sana Mhe. Spika, na mimi kunipatia nafasi hii ya kuweza kuchangia mswada huu uliokuwa mbele yetu. Awali ya yote Mhe. Spika, naomba nichukuwe nafsi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu aliye niwezesha kuwa na afya njema na asubuhi hii kuweza kusimama katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Spika, kwanza na mimi nianze na masikitiko yangu makubwa kwa kitendo walichokifanya wenzetu wale, ambao wanajiita wao ni watetezi wa wananchi. Mhe. Spika, naomba uniruhusu nitumie chombo hiki kuwaambia ndugu zangu wa Pemba, natumai wanaangalia hili Baraza letu tukufu, waone hao wanaowaita viongozi wao hivi watakwendwa kuwatetea vipi na kuwaeleza nini wanachi wao. (*Makofi*)

Mhe. Spika, hapa kila siku kwenye bajeti zilizopita tunakaa, tunasimama na kusema kwamba majimboni kwetu kuna matatizo ya maji na barabara. Sasa leo ikiwa serikali haitoidhinisha pesa hizi na kuweza kutawanya kwenye wizara mbali mbali, hizo huduma tunazozitaka zitakwenda kufanyiwa nini. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nakumbuka kwenye bajeti ya Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano Mhe. Farida Amour, alisimama hapa na kuwa mkali kweli, na kutoa mfano wa Uwanja wa Ndege wa Pemba, alisema kwamba tunabaguliwa baina ya Wapemba na Waunguja. (*Makofi*)

Mhe. Spika, hili linanisikitisha sana na sio kweli, laiti kama serikali yetu ingekuwa inabagua Mhe. Spika, basi natumai Pemba kungekuwa hakuna maendeleo yoyote, serikali wangkaa wakasema tufanye maendeleo huku Unguja, Pemba kusiende kitu, tungkuwa wapi na tukiangalia maendeleo yote kule Pemba yanaletwa na Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mhe. Spika, ukienda kwenye barabara, maji na wawakilishi wapo wanasaidia nini, hakuna. Kwa hivyo, nawaomba wananchi wa kisiwani Pemba mubadilike, natumai munafuatilia hoja hizi. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mimi naomba niunge mkono mswada huu wa kuidhinisha makisio ya shilingi bilioni 830,360,300,000/- kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali kwa mwaka wa fedha 2015/2016, ili wananchi wetu waepukane na matatizo mbali mbali yanayowakabili hivi sasa.

Mhe. Spika, sasa hivi tuna matatizo mbali mbali katika mahospitali. Kina mama wanapoteza maisha kutokana na ukosefu wa damu, matumizi mbali mbali ya vitu vya hospitali hakuna. Leo Mhe. Spika, tukisema tunasusa kama walivyofanya wenzetu, mambo haya yatafika vipi. Mhe. Spika, tuna uwanja wetu wa ndege ule pale wa Pemba leo umeshaanza kutiwa taa, *Alhamdulillah* mambo yanaendelea. Leo bila ya kuidhinisha pesa hizi ule uwanja utafikia wapi na tunakaa hapa kila siku tunapiga kelele uwanja wa ndege wa Pemba, leo wametoka watakuja kusema nini kuhusu uwanja wa ndege huo, watawaambia nini wananchi ili wasikie. (*Makofi*)

Mhe. Spika, walisema hapa tutiliwe japo vibatari. Leo *Alhamdulillah*, miundombinu ya taa imeanza kuwekwa. Leo tunatoka humu ndani, hivi kweli tunawatendea haki wananchi, tunawapenda kweli wananchi wetu au tunajitakia sisi tu raha. Vile vile, Mhe. Spika, pesa hizi kama hazikuingizwa hizo barabara zetu tatu za Pemba tunazozipigia kelele Wete Konde, Wete Gando na Wete Chake Chake zitatengenezewa nini bila pesa hizi serikali kuidhinisha wakaenda kutumia.

Mhe. Spika, pia, tuna suala zima la meli, kila siku tunapiga kelele hapa ee! Wananchi wa Pemba wanakuwa. Meli *Alhadulillah* karibu itaingia tunategemea, bila ya kuidhinishwa pesa hizi tukamalizia kule ikaletwa meli yetu ili wananchi wetu na wao wakasafiri kwa salama, itakuwa vipi.

Mhe. Spika, bado kuna sehemu nyengine katika vijiji vyetu kuna matatizo ya maji, bila ya kumuidhinishia pesa hizi Mhe. Waziri, akampelekea Mhe. Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati pale, ili wananchi hao nao wakaepukana na hili tatatizo la maji, pesa zitapatikana wapi.

Mhe. Spika, baada ya hayo machache mimi naunga mkono kwa asilimia mia mswada huu kwa niaba ya wanawake wa Mkoa wa Kusini Pemba. Nakushukuru Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, kwanza nichukuwe fursa hii kukushukuru sana na mimi kunipa nafasi ya kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya mwaka huu wa 2015/2016.

Mhe. Spika, kwanza. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Makofi yote hayo ni ya Mhe. Othman Nyanga. Nakushukuru sana kuhudhuria kwenye mkutano huu. Endelea.

Mhe. Nassor Salim Ali: Mhe. Spika, Waswahili wanasesma; "Ngoma ya kitoto haikeshi". Kwa sababu wenzetu leo wametia tena mpira kwapani na haya ni

mazowea tumeshayazowe. Lakini leo ndio lile dimba linafungwa kabisa, kwa sababu maneno ambayo aliyoazungumza Mhe. Hamza Hassan Juma, ninayaunga mkono na niseme kwamba huu ndio mwisho wa safari ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. (*Makofî*)

Mhe. Spika, Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, siku zote wakati akihutubia hotuba zake, amekuwa akihutubia amani na utulivu wa nchi yetu na siku zote amekuwa akihutubia na kusema kwamba anatekeleza na kuisimamia Serikali ya Umoja wa Kitaifa ambayo imo ndani ya Katiba ya Zanzibar. Lakini leo nadhani hata Mhe. Rais ameyaona haya na leo nadhani atakoho, kama sio leo, ni kesho. (*Makofî*)

Mhe. Spika, Waswahili wanasema; "Mwenda tezi na omo, huishia ngamani" na ngamani leo imefika. Wazanzibari leo wameona vioja na vioja hivi vimetendeka ndani ya Baraza lako tukufu, nina imani kubwa kwamba wananchi wa Zanzibar wataamua maamuzi ambayo ni ya kuiondoa kabisa Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa wakati utakapofika. Kwa sababu serikali hii imepitishwa na Wazanzibari kwa dhamira njema, kwa malengo mazuri kwa sababu ya kuleta umoja na mshikamano na amani ya nchi yetu, lakini wenzetu hawana mapenzi, imani na wala dhamira njema na nchi yetu. (*Makofî*)

Mhe. Spika, mimi nina imani kubwa wananchi wa Zanzibar ifikapo mwezi wa Oktoba, wataamua maamuzi ambayo ni makubwa na yenye hadhi ya kuichagua CCM kwa ngazi zote. Kuanzia ngazi ya Urais, Wabunge, Wawakilishi wa CCM kwa sababu ndio wenye imani na nchi hii. (*Makofî*)

Mhe. Spika, asubuhi wakati wanatoka Wajumbe wenzetu uliona hali, lakini angalia Baraza lako tukufu linavyo meremeta hivi sasa. Nichukuwe fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wawakilishi wote wa CCM, kwa kuja kwa wingi. Kwa yule ambaye hata alikuwa Dar es Salaam. Kwa taarifa yako Mhe. Spika, kuna wengine wamekodi ndege maalum na wamefika hapa, kwa mapenzi na imani ya nchi yao. (*Makofî*)

Mhe. Spika, kwa sababu laiti kama isingepitishwa sheria hii ya mswada huu, basi yale yote mazuri ambayo serikali yetu ilidhamiria kuyatekeleza ndani ya majimbo yetu na ndani ya nchi yetu basi yasingewenza kufanyika. Lakini kutokana na imani na uchungu wa nchi yetu Wawakilishi wa CCM wako ndani na tutaupitisha mswada huu wa matumizi kwa asilimia mia moja. (*Makofî*)

Mhe. Spika, leo ni siku ya aibu, lakini ni siku ya mafanikio. Aibu itawapata wenzetu, lakini mafanikio kwa wale ambao wana imani na mapenzi na nchi yetu itakuwa ni mafanikio makubwa sana, kwa sababu sisi leo hapa tatafanya maamuzi

ya matumizi haya kwa maslahi ya nchi yetu, majimboni kwetu na maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Spika, nikushukuru sana kwa hotuba yako nzuri ambayo uliitoa hivi punde. Ni hotuba ambayo ilitufanya hata sisi Wawakilishi wa CCM tuwe na ari ya kuchangia mswada huu kwa nguvu zetu zote na niwapongeze sana. Leo nimeona Waswahili wanasesma; "Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu". Lakini leo nimeona umoja wa wana-CCM au wawakilishi wa CCM ndani ya Baraza lako tukufu; sio mawaziri wala sio sisi huku *back benchers*. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mimi nimalizie kwa kusema kwamba niwaombe Wazanzibari wote wanaoitakia mema na maendeleo Zanzibar tuungane kwa pamoja kumchagua tena Dk. Ali Mohammed Shein na wale wote ambao tunamalizia kipindi hiki. Nimuombe sana Mhe. Rais, ingawa haya ni maamuzi yake, lakini unajua siku zote Mhe. Spika, timu ya ushindi haibadilishwi. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Rais, mawaziri wake wa CCM wamefanya kazi kubwa wote. Wale wa kuchaguliwa majimboni na wale ambao kawateuwa yeye, wamefanyakazi kubwa mno. Nina imani kwamba sisi huku *back benchers* wa majimbo tatarudi na mawaziri wetu ambao mumeteuliwa kupitia Ikulu Mhe. Rais atawarejesha tutafanyakazi hii kwa mwaka 2015/2020. (*Makofi*)

Mhe. Spika, nakuhakikisha Mwenyezi Mungu akitujaalia uhai na uzima tutakuchagua tena kuwa Spika wetu kwa mwaka 2015/2020. Mhe. Spika, baada ya kusema haya naunga mkono kwa asilimia mia moja.

Mhe. Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mhe. Mlinde Mabrouk Juma: Mhe. Spika, na mimi napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu, lakini kukushukuru na wewe pia kwa kunipatia nafasi hii asubuhi ya leo, kuchangia mswada huu wa matumizi.

Mhe. Spika, kwanza nikupongeze kwa nasaha ambazo ulizitoa leo asubuhi, baada ya tukio ambalo lilitokea, wengi sisi hatukutarajia kwamba tukio lile lingetokea siku ya leo. Lakini maneno haya yalikuwa yakizungumzwa siku nyngi, kwamba hawa wenzetu hawako na nia ya dhati. Ilionekana kwamba kuna siku watafanya vitendo hivi. Lakini leo tumefika dakika ya mwisho, kama ni mpira dakika 90 tunasubiri zile za *referee* tu za watu ambao wameumia umia kidogo nje ya dakika zile, leo ndio wanatoka uwanjani.

Sasa Mhe. Spika, niwaombe sana wananchi wa Zanzibar wawaone viongozi wenye style ya aina hii, kwamba sisi hawatufai. Sisi wengine kabla ya uchaguzi tulikuwa tuko kwenye shughuli zetu za kawaida. Ulipokuja mfumo huu wa Serikali ya

Umoja wa Kitaifa, tulikuwa na maswali mengi tunajiuliza, lakini Waheshimiwa Wawakilishi wakati ule tulipoona wanajenga zile hoja, zilitushawishi na sisi kuukubali mfumo huu baada ya kuja kwetu, basi tuliamua tupige kura ya ndio ili Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa iweze kuwepo katika nchi yetu. Lakini matokeo yake tunaona sasa tunapata mashaka kwamba serikali hii, tunaona kama ule msemo wa Marehemu Mzee Karume aliposema; "Koti likikubana livuwe". Kwa maana serikali hii sasa tunaona haina maana yoyote.

Mhe. Spika, Marehemu Mhe. Salmin Awadh Salmin, alikuwa ana mawazo hapa ya kuja na hoja binafsi. Lakini Mhe. Hamza Hassan Juma, amesema muda kwa kweli utaangalia kama upo, lakini kwa kweli hakuna haja tena ya kuwa na mfumo huu, kwa sababu hatuoni faida ya kuwepo mfumo huu, kama leo viongozi wa serikali mawaziri ndio wanawashawishi wajumbe kwamba watoke, aah! Hii inatupa mashaka sana, matarajio ya wananchi sivyo alivyo. Kwa hivyo, Mhe. Spika, kama muda upo tupo ili wananchi wakaulizwe muundo huu wa serikali kama wanautaka au hawautaki halafu ndipo twende kwenye uchaguzi.

Mhe. Spika, mimi leo nimemshangaa sana mzee wangu huyu namuheshimu sana kwa jinsi walivyojipanga kuja kuvuruga zoezi zima la kupitisha mswada huu ili serikali ishindwe kutumia katika mwaka unaokuja wa 2015/2016.

Mhe. Spika, kama nimemfahamu vizuri alizungumzia kuhusu watu jinsi wanavyoandikishwa wanateswa, sijui wanapigwa na askari wanavaa ninja. Hapa tuna swalii la kujiuliza hivi uandishi huu ulipokuwa katika kisiwa cha Pemba hawa askari walikuwa hawapo, mbona Pemba wameandika wanavyojisikia na wamemaliza kwa salama. Leo tunaandika Unguja hapa sasa tunaambwiwa ooh! Askari wanavaa ninja na wanazuwia wananchi. Kama wanataka kufanya siasa na sisi siasa tunazijua na tunaziweza, lakini kwa *style* hii ambayo wanakuja nayo wananchi wamewaona, wamewasikia na nina imani kwamba wananchi watawakataa.

Mhe. Spika, kitendo hiki cha leo kinatupa picha moja kwamba ule msemo wa CUF, kwamba Pemba ni yetu lakini Unguja ni yetu sote. Kwa sababu Pemba wameandika salama Unguja watufanyie rafu, hiyo wanaamini kwamba Unguja ni ngome ya CCM, lakini wananchi tuko macho, hatutokubali kufanyiwa vitendo vyengine vyovyote ili wananchi wetu wasiweze kuandika. Tutapambana hadi dakika ya mwisho. Lakini wananchi wataendelea kuandika kwa salama na amani na vyombo vyaya dola naamini viro tayari kukabiliana na tukio lolote lile litakalojitokeza.

Mhe. Spika, nikije kwenye huu mswada kifungu cha 5 kinampa uwezo waziri wa kukopa. Mimi nimwambie Mhe. Waziri, kwamba tunamruhusu aende akakope ili aweze kutekeleza majukumu. Lakini mwakani ajipange vizuri, kwa sababu hawa

leo wanaotupinga ni wafanyabiashara wakubwa na wengi ndio hao CUF ndio wanaokaa wakatupinga. Lakini mnawaachia huko, mnawasamehe kodi na kuwapa vichwa leo ndio haya yanatufika. Pahala pa kuwa wasifanye biashara wao wanafanya. Serikali ichukuwe bidii kusimamia kodi hizi na kama wanafanyabiashara mahala sipo waondoshwe, sio kwa sababu sasa hivi tunasema mwezi wa Ramadhan, hawa ndio hao wanaotuangamiza sasa hivi.

Kwa hivyo, Mhe. Spika, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia juu ya mia. Ahsante.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Spika, na mimi kunipa nafasi ya kuchangia Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya shilingi bilioni 830,360,300,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia siku ya tarehe 30 Juni, 2016.

Mhe. Spika, kwanza namomba nitoe masikitiko yangu kwa kweli kitendo cha wenzetu kutoka nje ya Baraza lako tukufu kimenisikitisha sana na si kitendo cha kiungwana kwa kweli, lakini tuwaachie wananchi wenyewe wanaona na watapima ni nani kiongozi bora.

Mhe. Spika, napenda kuunga mkono Mswada huu kwa sababu kwa kiwango kikubwa ilani ya Chama cha Mapinduzi imefikiwa karibu asilimia 90, pato la Taifa katika mwaka 2010 ilikuwa ni bilioni 13.5 na mwaka 2015 tunaomalizia sasa umefikia bilioni 39 hii ni hatua kubwa iliyopiga Serikali. Na ukiangalia katika kipato cha mtu binafsi ninachokiangalia mwaka 2010 ilikuwa 500 na mwaka huu 2015 kimefikia 900 na hivi sasa nchi yetu inaelekea katika uchumi wa kati, hiyo ni hatua kubwa tuipongeze Serikali yetu ya Mapinduzi chini ya uongozi wa Dk. Ali Mohammed Shein.

Mhe. Spika, naunga mkono Mswada huu kwa sababu kuna masuala mengi ambayo katika kila Wizara kuna changamoto nyingi ambazo changamoto hizo zinahitaji kutatuliwa, malengo ambayo wamepanga wizara mbali mbali yanahitaji kufanyiwa kazi na bila kupitisha Mswada huo, mambo hayo yote hayatofanyika; ukiangalia sekta ya uvuvi kwenda kutengeneza michoro ya ujenzi wa kitengo cha utafiti baharini, kuna suala la sekta ya elimu, suala zima la ununuzi wa madawati, vifaa vya maabara, ujenzi wa barabara na mikopo kwa wanafunzi. Hayo yote kama hatujapitisha Mswada huu hayatoweza kufanyika. Kwa hivyo, mimi nimesimama hapa kuunga mkono Mswada huu ili yale ambayo Serikali imejjipangia kwa kipindi hichi 2015/2016 yaweze kutekelezeka kwa asilimia 90.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo naunga mkono Mswada huu ili tuipe nafasi Serikali itekeleze majukumu yake ipasavyo ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, Mungu akitujaalia Mswada huu tutapitisha leo hii na kwa hivyo, niwaombe wenzangu mnaonisaidia kuwaarifu Waheshimiwa mbali mbali wafuatao, ili waweze kuhudhuria punde tu katika kikao hichi na kuwaomba wale wengine wote ambao tuko humu ndani kama tunatoka nje kwa dharura basi tukumbuke kurudi kwa sababu shughuli hii imalizike leo hii. Kwa hivyo, naomba Mhe. Zainab Omar Mohammed, Mhe. Machano Othman Said, Mhe. Mwanasheria Mkuu, Mhe. Ali Mzee Ali, waarifiwe waje tushirikiane hapa kufanya kazi hii, Mhe. Asha Bakari Makame, kama hali yake inaruhusu pia aarifiwe aje hapa naelewa kwamba hali yake kidogo sio nzuri, lakini kama anajimudu basi aje kwenye kikao hichi ili tuweze kuifanya kazi hii kwa pamoja.

Mhe. Mohammedraza Hassanali, Mhe. Mtando, alikuwa na dharura ya kuumwa, lakini kama nae anajimudu basi aje, aarifiwe, ajiangalie kama anajimudu aweze kuja katika kikao hiki, Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa, najua anafanya kazi ya kuwachunga wengine, lakini nae awahi, aje kwenye kikao hichi, Mhe. Shamsi Vuai Nahodha, kwa wiki nzima tulikuwa nae, sina hakika kama amewahidi Bungeni, maana kuna kazi kama hii vile vile, lakini kama yupo hapa Zanzibar basi tumuarifu ili nae aje kushirikiana nasi hapa.

Nadhani wengine wote wana dharura na taarifa zao ninazo, kwa hivyo, tukiwapata wajumbe hao kazi yetu itakuwa imekamilika vizuri sana na tujitahidi basi tunaendelea kuchangia lakini wajumbe hawa Mhe. Ali Salum, tujitahidi tuwatafute na Mhe. Mnadhim wa Serikali pia tujitahidi kufanya hiyo kazi, ili kazi hii imalizike kwa ufanisi mkubwa, tunao uwezo huo kwa wajumbe waliopo kufanya kazi ikaenda vizuri, hili si jambo jipya, huko nyuma limewahi kutokea na tumekwenda na kazi hii na imefanyika vizuri. Waheshimiwa wajumbe, tuifanye kazi hiyo kwa mashirikiano makubwa ili tumalize hii kazi ambayo tunakusudia kuifanya kwa niaba ya Serikali, lakini kwa manufaa ya wananchi wote.

Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Fatma Mbarouk Said, afuate baadae Mhe. Hussein Ibrahi Makungu, wakati Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, ajitayarische.

Mhe. Fatma Mbrouk Said: Ahsante Mhe. Spika, kwa kunipa fursa hii ya kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Makisio na Matumizi ya mwaka 2015/2016 Awali ya yote na mimi nitoe masikitiko yangu kwa leo humu ndani niseme sijui kama wenzetu au sio wenzetu kwa sababu kama walikuwa ni wenzetu basi walikuwa leo wabakie katika Baraza hili na kuitisha jambo hili muhimu.

Mhe. Spika, Mswada huu ni muhimu kwa sababu haziwezi hizo pesa zikatumika bila ya kumaliza kazi hii ya Mswada huu, mimi mbali na hayo lakini kwa kitendo ambacho wamekifanya na kwa Ramadhani hii basi ni kitendo ambacho hata Mwenyezi Mungu hayuko pamoja na wao, kwa sababu sisi kama wawakilishi

humu tunawatumikia wananchi wetu ambao wametuchagua, lakini baada ya kusema kwamba wao wameamua kutoka leo humu basi mimi najisikia raha kweli, kuna usemi wa kiswahili unaosema kwamba; "Ukisusa wenzio wala" na sisi humu tutakula tena kwa matonge.

Mhe. Spika, mimi ndani ya Mswada huu ukenda kifungu cha tatu ambacho kinasema;

"Idara ya Hazina Wizara ya Fedha inaweza kutoa katika Mfuko Mkuu wa Serikali wa Hazina kiasi cha shilingi bilioni mia nane thamani na mia tatu, na sitini milioni laki tatu kwa matumizi ya huduma kumalizikia mwaka tarehe 30 Juni, 2016".

Mhe. Spika, mimi naunga mkono kwa sababu bila ya kuunga mkono fedha hizi hatutoweza kuzipata. kwa hivyo. ni lazima tuidhinishe na tupitishe, na mimi yale yote aliyosema Mhe.Hamza, zile fedha Mhe. Waziri, akazikope na ile mitaro ambayo inamsumbu Mhe. Hamza, basi na mimi naomba fedha hizo zikopwe na tupewe sisi tuliokuwa tuna haja nazo, kwa sababu wenzetu leo wametoka humu. lakini wengine ni Mawaziri. sina haja ya kuyasema mengi, wao ni Mawaziri na wametoka huku na walismama pale mbele na kujilabu na kutoa matatizo yao mengi. Lakini leo hii baada ya kukamilisha hii ng'we wao wametoka na mna mambo mengi ya msingi; Kwanza elimu tumeona namna gani bajeti hizi mambo mengi ambayo yametakiwa na wao kama Naibu Waziri au Mawaziri lakini leo wametoka.

Mhe. Spika, kwa kweli hawajijui wao wenyewe wala hawajitambui, kwa sababu leo ilikuwa kwanza tumalize hili na baada ya kwisha kufanya kazi hii wao ndio waamue kutoka humu, lakini nasema leo na mwezi huu mtukufu wa Ramadhani basi naona kama wamejimaliza na niwaambie ndugu zangu kule Pemba, kwa kweli wamechagua watu ambao hawaonei imani, kwa sababu kama haya kuna mambo chungu nzima humu mahospitali, wagonjwa, lazima pesa hizi zikubalike halafu wao wapate hizo huduma mbali mbali, sasa leo kama wametoka humu hii kazi ataiifanya nani, sasa nasema kwamba wamejimaliza.

Mhe. Spika, kuna kisa cha Nabii Yunus, watu wengi watakuwa wanakijua baada ya kukimbia umma wake na akaingia kwenye jahazi lakini baadae Mwenyezi Mungu kwa kutaka kumuonyesha kwamba kile kitendo alichokifanya kilikuwa sio cha kiungwana na kwa sababu Mitume na wao walikuwa ni wanadamu na walikuwa na kasoro zao, lakini walikuwa wanapewa wakhyi, basi Nabii Yunus alipokuwepo tumboni kwa yule chewa aliomba na alisema; "*Subhanallah walhamdulillah walailahailallah allahuakbar walahaula walakuwata ilabilah laliyu lghadhim hasbiyallah waneemal wakil lailahailla subhanaka inni kuntum*

minadhalimin fastajabna lahu walajaynahum minalghani kadhalika mujin muumini".

Mhe. Spika, malaika kwa kweli walimtafuta wakenda dunia nzima, hii dua ni kubwa na leo mimi naiomba hapa na usiku tuiombeni, tuisomeni hii. Walitafuta ulimwengu mzima wakatafuta baharini na mwisho wakarudi kwa *Allah Subhanahu wata'ala* kwenda kumwambia ili waje wamuokoe, kwa hivyo, leo hawa hawana uokovu, hawa wenzetu leo na Ramadhani hii basi naomba dua kwamba wananchi wawaone kwamba hawa watu ni madhalimu kwao na wasiwapo hizo kura zao, nawaomba sana ndugu zangu wa kisiwani kule Pemba.

Kama alivyosema mwenzangu hapa wao wanasema Pemba ni yao na Unguja ni yetu sote lakini leo wanadhihirisha watawadhalilisha wale wananchi ambao wako kule, kwa nini leo tusimalize kazi hii, kwa nini wasija humu ndani wanaonekana kwamba ni wadhalimu na wala hawana uzalendo wa nchi hii.

Mhe. Spika, mimi ninachokiomba tu fedha hizi ziwe na usimamizi mzuri, tuzipitishe, tuukubali mswada huu kwa sababu ni mswada muhimu wa kumalizia kazi yetu ile ambayo tumeianza karibuni mwezi mzima tumekula maposh. Leo kweli ile thamani iko wapi, hili ni jambo la mwisho, ilikuwa hili tulifanye, yaani ni la mwisho lakini ni kubwa. Kwa hivyo, kitendo kilichofanyika hapa leo nawaomba na Mwenyezi Mungu kwa leo hii hatokuwa pamoja nao.

Mhe. Spika, baada ya maneno hayo nashukuru na naunga mkono mswada huu. Ahsante sana. (*Makofī*)

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa sote tukiwa katika hali ya afya njema asubuhi hii, pia, nikushukuru wewe Mhe. Spika, kunipa nafasi hii kuchangia mswada wa Sheria hii ya kuidhinisha Makisio ya Matumizi ya shilingi bilioni 830, 360,300,000 kutoka mfuko mkuu wa Hazina wa Serikali wa mwaka wafedha.

Mhe. Spika, mimi naunga mkono asilimia mia kwa mia bajeti hii, sina shaka nayo wala sina matatizo nayo kabisa, na pia namuunga mkono Mhe. Hamza, kwa mchango wake asubuhi, kwa sababu pale asubuhi, nilikuwa namuangalia kwenye TV Mhe. Hamza, kwa kweli nampongeza kwa mchango wake mkubwa na mzuri sana, umeweza kuelimisha sana jinsi Serikali yetu inavyofanya kazi vipi na alivyoiona na ye ye mwenye, kwa hivyo, nampongeza Mhe. Hamza, kwa mchango wake. Lakini Mhe. Spika, pia, nimpongeze Mhe. Waziri wa Fedha, kwa juhudhi zake kubwa na jana alipokuwa anatoa hotuba yake nilimsikiliza kwa makini sana, kwa kweli Mhe. Waziri wa Fedha, mimi nampongeza na naamini ana imani kubwa na nchi hii na anajitahidi sana kutafuta fedha kila kona.

Mhe. Spika, mimi nimpongeze Waziri wa Fedha, kwanza kwa jengine kuna kipindi cha mwaka mmoja nyuma hapo mwaka jana tulikwenda China kwa jitihada zake kubwa na Mhe. Spika, wewe ni shahidi tulitoka hapa mimi, wewe Mhe. Spika, Mhe. Asaa Othman Hamad, Mhe. Abubakar Khamis Bakary, Mhe. Bikame Yussuf Hamad na wajumbe wengine, tulikwenda China, tulianza Beijing, Shanghai tukafika Makao na sehemu nyengine kwa kupata misaada mbali mbali ya kuweza kuendesha nchi yetu kwa ajili ya matatizo muhimu tuliyokuwa nayo na kuwaokoa wananchi wetu katika matatizo mbali mbali ya kijamii.

Lakini Mhe. Spika, mimi ninachoshangaa kwa hawa wenzetu sijui hili wanalionaje, naomba wananchi wafahamu kwa mambo muhimu ambayo tunajitahidi kuitia misaada kwa wafadhili wetu. Mswada huu ni muhimu tena muhimu kweli kweli kwa sababu una fedha nyingi sana hapa za kuondosha matatizo yetu hasa katika sekta mbali mbali, lakini kwanza nianzie kwenye sekta hii kwenye Wizara ya Elimu, kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Elimu, kwa kupanga kuniwekeea skuli ya kisasa moja pale katika Jimbo langu la Bububu, ile skuli ya Bububu ishakuwa ndogo, na wanafunzi sasa hivi washakuwa wanasoma mpaka chini ya miti na nilisema katika bajeti hapa.

Lakini namshukuru Mhe. Shamhuna, kwa juhudi zake kubwa kunambia ndani ya Baraza lako tukufu atanijengea skuli, hii ni nia njema ya Serikali na kuwaondoshea matatizo wananchi wetu. Mimi naomba wananchi pia wafahamu kazi tunayoifanya kama mimi binafsi kuchukua wanafunzi Bububu mpaka mjini kila siku kwa *trips* tatu kwa siku, hii kazi sio ndogo lakini tunafanya hivi kwa ajili ya wananchi wetu ni masikini, hawawezi kufika skuli watoto wetu wale, lakini nimefanya juhudi hizi ili kuwaondoshea matatizo na usafiri ule mimi niseme hawapandi watoto wa CCM peke yao, ila wanapanda kama wa CHADEMA, wa CUF, wa CCM na pia waliokuwa hawana chama wanapanda, lengo na madhumuni usafiri ule watoto wetu wasome kwa nia njema ili kuondosha tatizo la usafiri, sasa leo hawa wenzetu wanakuwa na nia gani kufanya hivi. Mhe. Spika, mimi siwafahamu kabisa.

Mhe. Spika, kwa kweli hii kazi wanayoifanya sio ya kuendesha nchi hii, tunahitaji maendeleo mengi ukitizama katika sekta ya afya tuna matatizo mengi lakini tunawashukuru wafadhili wetu wametusaidia sana, ukiangalia kwa sasa hivi Mnazi Mmoja kuna vyombo mbali mbali vizuri vinafungwa, Rais wetu kasema juzi mpaka uti wa mgongo na ubongo unafanyiwa uperesheni hapo, Dk. Ali Mohammed Shein alisema kwenye vyombo vyaya habari juzi juzi alijisifu kabisa, hayo ni maendeleo, lakini bila ya kutegemea wafadhili ili kutusaidia hatuwezi kufika pahali.

Mhe. Spika, kuna siku nilikaa na Naibu Waziri wa Afya Mhe. Mahamoud, nampongeza sana kwa juhudzi zake, aliniambia sasa hivi India inadai Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar karibu dola laki saba kwa kupeleka wagonjwa kule India, lakini sasa hivi tunapeleka wagonjwa China. Waziri wa Fedha, hizi pesa nyingi hazijalipwa bado, tunapeleka wagonjwa wengine China kwa jitihada za Serikali yetu kwa kuona wananchi wake wanapata tabu, ijapokuwa tuna madeni, lakini tunajitahidi kupeleka wagonjwa nje ili kuwatibusi.

Mhe. Spika, mimi niipongeze sana hii hospitali mpya iliyojengwa juzi juzi ya Mhe. Turki Mwenyekiti wa Hospitali ile *Vigo Company*, kwa sababu hospitali ile ni nzuri na bila ya amani na utulivu, hata wawekezaji hawa hawatoweza kuja, sasa hawa wenzetu wamefanya hivyo, mimi nadhani wanarudisha nyuma maendeleo yetu, sijui lengo lao liko wapi, ukitizama Wizara ya Ardhi, Maji na Nishati, kuna matatizo mengi hasa suala la maji na umeme, ukitizama sasa hivi Serikali yetu imeamua kuondosha mita kwenye vianzio vya maji vyote ili wananchi wapate maji *times* zote. Hili ni jambo la kupigiwa mfano.

Wizara ya Fedha imeagizwa wapewe *ZECO* milioni 500 kwa mwezi ili kuondosha kuwakatia umeme. Rais wetu katoa agizo hili, hili ni jambo la kupigiwa mfano. Mhe. Spika, serikali yetu ina nia njema katika kuongoza na kuwatumikia wananchi wake, si jambo dogo hili.

Mhe. Spika, tulikwenda Arusha kipindi fulani tukamkuta mwananchi masikini lakini analipa maji Sh. 30,000/= kwa mwezi, sio 4,000/= hapo Arusha tuliiyona hali hii. Lakini Rais wetu kasema ondosha mita Wizara ya Fedha itoe milioni 500 iwapo *ZECO*, hili ni jambo la kupigiwa mfano, na mimi nampongeza sana Rais wa Zanzibar kwa juhudzi zake. Kwa sababu mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi naona shida ya maji kwa wananchi wetu, lakini jitihada ya serikali ni kubwa sana.

Tukija kwenye Wizara ya Miundombinu ukisema serikali yetu imepiga hatua kubwa ya maendeleo. Tumeweza kununua meli mpya ya kisasa inakuja Julai kesho kutwa. Tumeweza kujenga *Airport, Terminal 2* ni kubwa na ya kisasa. Hii ni jitihada ya serikali na mikopo ya wafadhili. Sasa hawa wenzetu wakifanya hivi sidhani kama wafadhili watatusaidia tena, lakini naona hawana nia njema kabisa na serikali yao na wala wananchi wa nchi yao.

Pia, niipongeze Serikali kwa juhudzi yake kubwa *Qatar Air Ways* kutua hapa mwezi wa saba ndege mpya, *Airline* ya kisasa kabisa inatua mwezi wa saba. Hili jambo la kupigiwa mfano, na haya ndiyo maendeleo yanayotafutwa ya kuongeza ajira, maendeleo na biashara katika nchi yetu.

Ndege hii ikitua hapa itaingiza mabilioni ya fedha kwa kuleta wafanyabiashara na mambo ya watalii na kila kitu. Mimi naipongeza sana serikali kwa jitihada kubwa hasa Wizara hii ya Miundombinu na Mawasiliano. Pia kujenga barabara kuititia wafadhili pia nawapongeza serikali kwa kutoa fedha zake na wafadhili pia.

Mhe. Spika, nije katika Sekta ya Utalii. Mimi juzi nilisema kuwa Sekta ya Utalii ni uti wa mgongo wa nchi hii, kwa sababu bila ya amani na utulivu, na hawa wenzetu kama wanaanza mambo kama haya hata hao wawekezaji watakimbia.

Juzi nilitoa mfano mzuri hapa, kuna hoteli moja imejengwa hapa Serena pembeni inaitwa Hyatt. Ile ni hoteli ya kisasa, ile hoteli mimi niliingia ndani nilisema juzi. Ile hoteli imepita viwango ilivyojengwa, imejengwa vizuri sana. Ukiingia ndani huwezi kusema kama upo Zanzibar, wametumia mabilioni ya fedha wale wawekezaji. Leo wakianza fujo hawa ndugu zetu wale wawekezaji tumewatia hasara kubwa.

Mimi naomba sana wananchi waelewe suala hili wasije wakawafuata kwa sera zao hizi. Hizi sio sera, hayo ni matakwa kwa ajili ya maslahi yao. Wawaangalie vizuri, sera ipo kwenye Chama cha Mapinduzi, hiyo nasema wazi bila ya matatizo, kwa ajili ina nia njema kwa wananchi wake.

Sasa hivi kuna hoteli karibu 16 za nyota 5 za kimataifa Zanzibar, hili ni jambo la kupigwa mfano zinaingiza pesa katika serikali yetu na pia wageni wanakuwa wenye hadhi kwenye hoteli hizi. Niwashukuru wawekezaji waendelee kubaki.

Mhe. Spika, nasema bila ya amani na utulivu hakuna mfadhili atakayekuja hapa na wala maendeleo tutayoyapata. Mimi niseme tu bila ya Mapinduzi ya mwaka 1964 mimi nisingezaliwa na leo nisingekuwa hapa. Nayashukuru sana Mapinduzi ya 1964 ndiyo nimezaliwa na leo nimekuwa hapa.

Mimi naipenda sana nchi hii, najitolea kwa hali na mali kwa ajili ya nchi hii kupata amani na utulivu na maendeleo, naipenda kwa dhati kabisa. Kwa sababu mimi sina pa kwenda pengine baada ya hapa, nimezaliwa hapa na nitaishi hapa, sina pa kwenda ndio maana nchi yetu hii naipenda sana kwa dhati na kwa nia njema kabisa.

Mhe. Spika, juzi hapa katika vyombo vyaya habari (ZBC) nimemuona Mhe. Rais yupo Ujerumanu anaongea na Watanzania na Wazanzibari, kule aliulizwa baada ya uchaguzi huu 2015 Serikali ya Umoja wa Kitaifa itaendelea? Mimi nikatulia kwanza kumsikiliza Mhe. Rais atasema nini hapa. Namsikia Mhe. Rais anasema Serikali ya Umoja wa Kitaifa itaendelea kwa sababu hii imepigwa kura na

wananchi, kwa hivyo itaendelea. Mimi nikasema dah! Mhe. Rais ana moyo kweli kweli, anasema hivi kwenye vyombo nya habari.

Mhe. Spika, kwa kweli nasema na mimi nimefunga nilishangaa sana, kwa ujasiri wake Dkt. Shein akasema maneno yale mbele ya Wazanzibari na kwenye vyombo nya habari.

Anasema kwamba itaendelea Serikali ya Umoja wa Kitaifa kwa nia njema, kwa sababu anataka kushirikiana na wao hawa ndugu zetu. Lakini mimi nashangaa haya matatizo yametokea juzi juzi kwenye Mkutano mwengine wa Mhe. Makamu wa Kwanza wa Rais, Kibanda Maiti alikuwa anawahutubia wananchi, anasema safari hii wakitaka wasitake tutachukua kwa nguvu.

Mimi hapa nikapima, nikaja nikamwambia Waziri wa Utalii, hii *ZBC* ioneshe mikutano ya hapa ya viongozi ioneokane wanavyosema wanavyohubiri.

Rais juzi alisema Ujerumani tumemsikia, lakini leo Makamu wa Kwanza wa Rais kazungumza lakini kwenye *ZBC* hazungumzi, kwenye *Star TV* wananchi wanyonge hawaoni.

Kuna watu *Star TV* hawapati wanakwenda *ZBC* lakini wanasisikia viongozi kauli zao. Dkt. Shein mimi nampongeza kwa kauli yake kwa ajili ya kudumisha amani na utulivu. Lakini Makamu wa Rais alivyosema pale pale mimi nikamjua kwamba huyu anataka madaraka tu, utasemaje kwamba utachukua kwa nguvu, wananchi kama hawajakuchagua je? Kama hawajakupigia kura wananchi vipi utachukua nchi hii. Kwanza wape sera wananchi, wakukubali, wakuelewe una sera gani. Usiseme kwamba mimi nitachukua tu, kama kura zako hazijatosha utachukua vipi. (*Makofi*)

Mhe. Spika mimi niseme kitu kimoja tu, juzi juzi pia nilisema hapa, mambo ya vitambulisho hawa wanashirikisha Jeshi. Wasishirikishe Jeshi, Jeshi halitaki kabisa mchezo.

Mimi Jeshi la JWTZ naliogopa, halitaki mchezo jamani. Wakipita usiku mimi nakuwa naogopa, hata nikiwaona wale majeshi, wale si watu wa masihara.

Tusiwashirikishe kabisa wale jamaa, wale jamaa hawana hata ule ubinadamu wa kukaa kuzungumza nao. Wale watu wapo kwenye ulinzi tu, kwa hivyo tusiwashirikishe hawa ndugu zetu. Yale magari ya Jeshi ni yao wenyewe, wana haki nayo; yakipakia raia wakipakia nani, tusiwaingilie, yale ni magari yao wenyewe, nilisema lakini naendelea kusema tena.

Mhe. Spika, jana hapa nilikuwa natoka kwenye Baraza nilikutana na Mhe. Waziri wa Mawasiliano Juma Duni. Mimi yeye kama baba yangu, namuheshimu. Na mimi ninavyojuu mimi ni mdogo, kwa hivyo yeye nimuamkie, hilo baba yangu kanifundisha.

Yeye wakati anatoka hapa Mhe. Juma Duni nikakutana naye nikampa mkono namsalimia kama Waziri wangu, mimi ni Mjumbe wake wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi wakati nampa mkono akanambia mimi sitaki mkono wako. Nikamuheshimia nikampa kwa mara ya pili, nikamuuliza kwani Mheshimiwa kwani kuna nini mbona unanifanyia hivyo. Akanambia mimi sitaki mkono wako, usinialisimie tena kuanzia leo!

Ilikuwa ni jana Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mhe. Mohammed Said Mohammed (Dimwa) shahidi, na Mhe. Ali Salum shahidi, Mhe. Shadya nikamwambia.

Mimi nafikiri yeye kwa kuwa ni mgombea wangu anagombea, sasa sijui tatizo lake nini. Nikamwambia mimi sawa sikusalimii, lakini nikasema moyoni kuanzia leo mimi nikikusalimia wewe tena mimi si mtoto wa Ibrahim Makungu.

Mimi sina shida ya kumsalimia mzee yule, sina haja, kwa kuwa nilikuwa namuheshimu tu. Leo inakuwaje ananambia nisimsalimie? Mimi nanunua salamu yake au mimi napata faida gani kwa salamu yake?

Mhe. Spika, kwa nini ananidhalilisha kama vile, kanidhalilisha kabisa. Mimi nikasema basi mimi naondoka, lakini huyu mzee mimi na yeye basi, na salamu hizi naomba kama ananisikia basi anielewe, nasema kwa nia safi sitaki tena salamu yake, na wala tuisalimiane tena, kuanzia leo sitaki tena!

Mhe. Spika, suala hili limekuja kutokana na ushindi wa kule. Wananchi ndio watakaopima, siyo yeye wala sio mimi. Kama yeye ananichukia mimi wale wananchi wetu ndio watakaopima kule, huyu anafaa kuwa kiongozi au hafai.

Halafu ukitizama mimi naona ajabu sana wana sera gani za kusema kule. Kazi inayofanyika sasa hivi kule wana sera za kuwaambia wananchi kuwandanganya wale wananchi. Wale wananchi wameshashtuka, wameshaelewa kwamba hawa waongo. Sasa anachochukia nini?

Juzi wamefungua kesi hapa, imekwenda kesi miaka miwili kunishtaki mimi uchaguzi nimewaibia kura. Imekwenda kesi nimeshinda Mahakamani. Sasa hawa watu wanataka nini. Leo wanakuja hapa wanatoka Barazani. Mimi nimesema wananchi wafahamu na wawapime hawa watu kwa makini. Bila ya amani na

utulivu nchi hii maendeleo yetu haya yote tutakuwa hatuyapati. Mhe. Spika. hawa watu sio watu wa kweli na sio watu wenye nia njema na nchi hii.

Mimi nampongeza Rais wa Zanzibar kwa nia yake njema, na kama alivyosema Ujerumani kasema kuwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa itaendelea lakini kwa hali hii Rais mwenyewe itampa mashaka. Wakae hawa viongozi wawaangalie viongozi wa Chama cha Upinzani hii hali, ndio watakaotuulishia ndugu zetu, watawaulisha wanawake na watoto, wanataka kuishi katika nchi hii sasa kama hali ikiwa hivi siyo ya amani na utulivu hatutoendelea.

Mhe. Spika, mimi nashukuru sana katika Baraza lako Tukufu naelewana na Wajumbe wote; wa *CUF*, wa CCM lakini jana tumemalizana na Mhe. Juma Duni itakuwa tena hamna kabisa stori baina yangu mimi na yeze. Kwa hivyo mimi naomba sana wananchi waelewe ukweli uko wapi.

Mhe. Spika, Mhe. Waziri wa Fedha anajitahidi anatutafutia fedha kila kona masikini, anakwenda kuomba, tumekwenda mpaka China Mhe. Spika, shahidi ni wewe. *ZTE* tumekwenda tumeoneshwa mitandao sijui *CCTV Cameras*, mitaani leo zimeshafungwa kamera kwa jitihada ya Mhe. Waziri wa Fedha.

Mimi nampongeza sana na namshukuru. Tumekwenda kuomba karibu dola milioni 30 mradi wetu tunakopa kule, leo hizi pesa tutazilipa vipi. Lazima tuangalie na hili suala liko vipi na wanachi wapime kabisa. Mimi nimeshapima na nimeshajua wala sitaki kuambiwa kitu. Nimeshapima nimeshaona, lakini na wananchi wapime suala hili nani mwenye nia njema ya nchi hii.

Mhe. Spika, baada ya hayo naunga mkono asilimia mia Mswada huu sina mashaka nao mimi na wananchi wangu wa Bububu. Ahsante sana nakushukuru kwa kunipa muda wako. (*Makofit*)

Mhe. Spika: Tunakushukuru sana Mhe. Hussein Ibrahim Makungu. Namkaribisha Mhe. Makame Mshimba Mbarouk, afuate Mhe. Abdi Mosi Kombo na Mhesimiwa...

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, na mimi kwanza nakushukuru.

Mhe. Spika: Ngoja kwanza, na Mhe. Ali Salum Haji, tumempa kazi lakini akija na yeze atakuwa anachangia, basi tayari ajitayarlishe Mhe. Viwe kabla ya Mhe. Ali Salum ambaye tumempa kazi ya kuwaarifu Wajumbe wengine wahudhurie hapa kwa muda mfupi ili tuweze kumaliza kazi hii. Mhe. Makame Mshimba.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Spika, nikushukuru sana na mimi kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia Mswada huu wa Mhe. Waziri, lakini kwanza kabla sijaanza kuingia kwenye kuchangia ningependa niseme machache. Kwa mfumo huu ambao tunakwenda nao wa Serikali ya Kitaifa, "*Innaa lillaahi wainnaa ilayhi raajiuu*". (*Makofî*)

Baada ya hilo na jengine Kifungu cha 43(5). Mhe. Spika, hapa ndipo panapotungwa Sheria, nataka niseme jambo moja.

Mimi mara nyingi sana nilikuwa nasema *backbencher* ndiyo inayotoa hoja. Leo nimepata maajabu makubwa sana Mhe. Waziri kutoa hoja na Wajumbe wakamfuata wakaenda huko. Sasa leo Mheshimiwa nataka nikwambie ndiyo ile nyimbo inayosema;

"Mguu mbele mguu nyuma, mguu mbele mguu nyuma, mguu mbele mguu nyuma". (*Makofî*)

Mhe. Spika, kuna mambo mawili unapotaka kutunga nyimbo iangalie tafsiri yake. Unapotoa madua mengi ukalaani jambo jiangalie nafsi yako imekosheka. Sasa naingia kwenye tafsiri. Wenzangu walianza kwenye Bunge la Katiba, "mguu mbele mguu nyuma", ulianza kule.

Mhe. Spika, tumeingia hapa leo inaonesha dhahiri ndio ule mguu mbele mguu nyuma, kwa maana hiyo hii nyimbo haifai, kwa sababu haifikishi lile lengo lilokusudiwa. Mheshimiwa naomba sana hii nyimbo waifute. Lakini sheria, sheria, hapa Kamanda wangu alisema Mhe. Hamza Hassan Juma, hakutoa kitu kwenye kichwa alinukuu katika Katiba.

Sasa jamani siku zote nikisema nipewe uwaziri, leo hii nafasi hiyo iwazi nipewe mwényewe uwaziri japo miezi miwili. Hii nafasi ipo *open* kabisa kwa mujibu wa kifungu cha 43(5), tayari hakuna Waziri tunangoja nini? (*Makofî*)

Mhe. Dkt Shein nimuombe sana kwa ridhaa yake aniachie uwaziri, kwa sababu sheria ipo na Kanuni na Katiba imeeleza wazi 45(5) iko wazi kabisa, nisinyimwe haki yangu Mheshimiwa, kwa sababu mnapofika pahali watu mkaungana mkatengeneza kitu kinaitwa *agreement*, mikataba kwa mujibu wa sheria au ukatunga Katiba ambayo tunakubaliana kwamba Katiba ndiyo mama wa kuweka sheria ndogo ndogo, unapofika pahali ukavunja wewe sijui tunangojea nini.

Mimi leo nategemea sana Mheshimiwa wangu Dkt. Shein msikivu, nafikiri anasikia sasa hivi basi juu lisitue akanikabidhi ufunguo wangu wa Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano nipewe mimi. (*Makofî*)

Mhe. Spika, uwezo ninao, nilikuwa kwanza Mwenyekiti, nina *experience* nayo hiyo. Nilikuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi, nina *experience* nzuri tu na matunda yangu mumeyaona, kwa nini nisipewe funguo leo, kwa nini na wananchi wangu na wao wakafurahi wa Jimbo la Kitope.

Mhe. Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili, kanichukulie ufunguo wangu haraka sana, kwa sababu wewe ndiye mtendaji Mkuu, kanichukulie ufunguo wangu.

Unajua kuna mambo hayataki tochi, sasa hivi mchana unamurika nini na watu wameshatoka, wako wapi. Ilikuwa mimi leo niende pale nikakae kwenye kitinianze kuhutubia, lakini Kanuni hainuruhusu, ilikuwa nikakae pale nikachukue *practice* ya kuweza kujifundisha kukamata uwaziri kwa muda wa miezi miwili, lakini naheshimu Kanuni, ndiyo maana sikuweza kufika pale mbele. Lakini ninachosema kila siku tunahubiri amani na utilivu. Sasa mimi nashangaa hii amani tunahubiri vipi.

Unajua siku moja Mhe. Spika, juzi nilisikia wenzetu wameongezewa muda wa siku 10 kutokana na hoja zilizokuwa ni nzito za kuweza kujadiliwa. Hebu na sisi tupewe siku tano, hatutaki kumi sisi, ili tumalize kazi. *Wallahi* tumejitolea hatutaki posho na wala msitupe chochote.

Mhe. Hamza Hassan Juma, amemaliza kabisa, siku tano Mheshimiwa kuna tatizo gani. Mhe. Waziri wa Fedha siku tano mpenzi wetu hebu tutilie, usitutilie sana hizo pesa, tutilie kidogo tumalize kazi siku tano tu utupe. Tusiwaachie wananchi wakaamua, tunaanza hapa. Tukimaliza hapa tunawaambia wananchi amueni nyinyi wenywewe na ndiyo ilivyo, tunaanza sisi halafu tunawarushia wananchi wenywewe wanaamua.

Mhe. Spika, sio kitendo cha kibinadamu, kwa sababu wananchi wetu tulikuwa tunapiga zogo sana, kila mtu kasema yake; barabara ya nani, barabara ya wapi, sijui kisima hakitoki maji, tuliwasakama hawa mawaziri muda mchache, tuliwasakama kweli na mimi nilikuwemo.

Ni haramu kubwa leo kusema tusiipitishe, "*Innaa lillaahi wainnaa ilayhi raajiun*" Inasikitisha sana Mheshimiwa, hivi kweli mwanamme unakimbia vita.

Juzi Mhe. Ali Juma Shamuhuna (Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali) jeneralikanipa, halafu mimi ujeneralu ule nikimbie, nigeuke nyuma "mguu mbele mguu nyuma" haiwezekani!

Mhe. Ali Juma Shamuhuna siyo mjinga, kunipigia saluti, kaamini kama huyu jamaa anafaa kuwa jenerali, halafu leo mimi niwe mguu mbele mguu nyuma, haiwezekani hata siku moja, haiwi hiyo.(*Makofi*)

Mhe. Spika, inasikitisha sana; tumeletwa na wananchi tumekula kiapo, tumeshikishwa mas-hafu, halafu leo mtu anasema hapa anatoa madua, tizama yanavyodhuru.

Mimi siku zote nasema jamani usitoe dua kwenye siasa, wewe ndani yako umejikosha? Hebu nambie nani aliyejikosha, wanafanya mas-hara.

Siku moja Mheshimiwa mmoja hapa alitoa madua mimi nikacheka sana. Kumbe ile dua ndani yake inajenga siasa, Mwenyezi Mungu unafikiri hakuoni. Hii! hatari kubwa. Dua imewatoa ndani *Wallahi*, kila unaposoma dua yako jioneshe utakatifu wako.

Mhe. Spika, kwani mimi sijui dua, mimi nina dua nyingi, *Wallahi* nikikutolea dua hapa kawaalize masharifu wa mchangani watakwambia vitu vyangu timesoma huko. Lakini niitoe dua, hebu nambie leo nakwenda kwenye taarabu nikifika pale nitoe dua itafika.

Leo naingia pahali tayari muziki unaimbwaa "mguu mbele mguu nyuma, mguu mbele mguu nyuma" nambie Mheshimiwa dua gani itafika. Tunafanya hatari tusimchokoze Mwenyezi Mungu kunako siasa. Mwenyezi Mungu twende kwenye ibada yake, tukimaliza ibada yake tuseme mambo mengine ya kujenga mambo mengine.

Lakini hivi siyo inasikitisha sana Mheshimiwa. Mimi niwaombe sana waumini wenzetu twendeni katika mustakbali wa kidini, tukiondoka kule ndio uingie kwenye siasa sio dini uitie ndani ya siasa, ni kosa kubwa sana kwa Mwenyezi Mungu, hatufiki pahali.

Leo Mwenyezi Mungu katuletea neema ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa, sasa hebu itizame mwenyewe, zile dua zinatuondoa wenywewe tunangoja nini.

Mhe. Spika, hebu jifikirie unajua kuna tafsiri nyengine ukizisema, nataka Serikali ya Mkataba tafsiri yake unajua wewe. Ndio maana nikasema kuna vitu ambavyo na waje kuchukua hapa, mimi siku zote nawambia hichi kichwa. Mimi nikizungumza jambo nazungumza kitu fasaha. Waziri wa Fedha aliyyowaweka humu *wallahi* nimeyakuta yale niliyosema mimi humu. Nimesema masuala ya afya, leo pesa hizi hapa inatakiwa idhini tumruhusu akatumie, katumie Mhe. Waziri nenda katumie. Kakope, katumie, kongoa kabisa, wapelekee wananchi.

Mhe. Spika, kuna njia kule ya historia ya hayati baba yetu Amani Karume, hebu iangalie kule njia Mheshimiwa aliweka historia Kitope kule. Sasa hizi fedha Mheshimiwa naomba sana zижумлишe na hawa waliotoka, naomba uwapelekee kule wananchi wa Kitope wakajengewe ile njia ya hayati, historia ya hayati mwenyewe alipima kwa kamba wakati ule, pesa ziko *open* hizi hapa hazina wafanyakazi kazichukue. Tumekuruhusu kifungu chako cha 4 kitumie usiwe na wasiwasi wowote, jamadari ninakuamini mimi kabisa. *Wallahi* hapo Mheshimiwa unatikisa kama tunakupunga rubamba anakuja juu, akitoka hapo rubamba wako kichwani kakumbe pesa njoo tuletee kazi Mheshimiwa. Wao hawataki sisi tutatumia!

Mhe. Spika, lakini moja linanicheckesa, juzi nilisikia kanda ya Mheshimiwa wangu mmoja alikuja kule Kipandoni kufanya mkutano. Mheshimiwa huyu alitusaga sana kule, liangalie hili Jimbo la Kitope halina maendeleo halina nini ni mama huyu kasima maneno. Lakini leo waulizeni nataka niwaambie wananchi wa Kipandoni, muulizeni kilichomkimbiza nini humu kuyakataa hayo mafungu, anawatakiak kheri kweli?

Maji atayapata vipi wakati akizuiwa Mhe. Waziri asiende kuomba fedha huko, atapatajate fedha za kuletea maendeleo? Waziri kazikombe pesa mwanangu, *wallahi* utuletee, wenye dhiki sisi tupo, tunaotaka jimbo sisi tupo, kazikombe, unangoja nini? Kuna mambo mengi, juzi Waziri wangu hapa nilimsema Mhe. Mohammed Aboud kuhusu habari ya Maafa yaliyotokezea, leo katizame kule, kifusi kimetandikwa utasema kama kimetiwa lami, ndio haya, walipiga kelele wao njia ile kule juzi maji yalipojaa kule, leo katizame Mhe. Spika, njia lami kabisa, si ndio mafungu yenyehe haya?

Na wale wenzangu walichangia njia ile waliponiona mimi wakajidai kuchangia na wao hivyo hivyo, sawa ndio ilivyo. Sasa leo mmekimbia, ina maana leo tusiitumie ile njia haiwezekani. Hili suala linanisikitisha sana!

Nikiendelea zaidi kuwaonesha, tulizungumzia masuala ya uwanja wa ndege na watu wakachangia vizuri sana, lakini mimi ninajuliza ikiwa leo tunataka kasma hizi ziendelee zifanye kazi vizuri na Waziri tushamkimbia hapa, unajua Mhe. Spika, wananchi hawajui kilichokimbiwa hapa. Suala ambalo la uandikishaji sio pahali pake sasa hivi hapa, hapa anatakiwa Mhe. Waziri atumie mafungu yake ya fedha yale tuliyokuwa tukizuia. Uandikishaji ziko sheria zake za *ku-claim*, muda upo huko nenda ka-*claim* sio ndani hapa, hapa ndani kinachotakiwa maendeleo ambayo tulikuwa tumechangia katika bajeti kuu zote.

Sasa leo unakuja hapa kutoa hoja ya uandikishaji hauendi vizuri, unataka iwe vipi, mguu mbele, mguu nyuma, ndio wenyewe huu Mheshimiwa, kwa sababu hatwendi

hii kitu tafsiri inatakiwa uwe *mind* kweli, uangalie kama ulivytulua hapo Mhe. Spika, sharti ukae ufikiri, kwani Mhe. Spika, unapokaa ukafikiria ukawajua tabia zote za Waheshimiwa wako, kwa sababu gani, unakuwa mtulivu kwenye Kiti chako. Kwa hivyo lazima inakuwa hali halisi.

Mhe. Spika, mimi ili niweze kumalizia kwanza nakubaliana nalo, nimeseme kifungu namba 4 ninakubaliana nacho na ninamruhusu kwa mujibu wa sheria zetu za Baraza, naunga mkono kwa asilimia mia juu ya mia kabisa.

Mhe. Spika, la kumalizia ukiungana na wewe, ukiungana na Mhe. Aboud ukiungana na mawaziri hapa kanichukulieni ufunguo wangu, mnachelewa! Ahsante sana.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: *Bismillahi Rahmani Rahiim.* Mhe. Spika, kwanza ninamshukuru Mwenyezi Mungu kwa uwezo wake kwa kutufikisha hapa leo tukiwa wazima na afya kwa kuja kuipitisha bajeti yetu ambayo tumeijadili tokea tarehe 13/5/2015 mpaka leo tarehe 23/6/2015.

Mhe. Spika, kuna lugha moja inasema hivi *aljununu fununu, al-akilifani wahida*, maana yake ni kwamba akili ni moja lakini wazimu kila mmoja na wake. Sasa tukikaa sisi kujadili watu wendawazimu tutapata tabu.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe huo ni msemo aliokuwa anatumia Dkt. Salmin Amour. (*Makofi*)

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Kwa hivyo Mhe. Spika, kuna wazimu wa kupiga, kuna wazimu wa kuvua nguo, kuna wazimu wa kusema peke yake, kuna wazimu wa kila kitu. Kwa hivyo Mhe. Spika, kinachotakiwa hapa leo kuidhinisha na kukubali kazi tuliofanya tokea tarehe 13/05/2015 mpaka leo. Lakini sasa tutafanya vipi na ile kazi ya ule ugonjwa uliozungumzwa katika lugha ushafanyika, kwa hivyo sisi tuliobakia sasa hivi tuweze kuunga mkono ili matatizo yetu tuliozungumza katika majimbo yetu yakafanyike, lakini tukisema tunakaa hapa tunajadili ile *al-akilifani wahida* hatuiwezi sisi hata kidogo.

Mhe. Spika, mimi mchango wangu katika majimbo yetu Wizara 16 tumezijadili hapa tumezungumza kila matatizo; kuna matatizo ya elimu, maji, umeme, barabara na sote tumekubali pamoja na mawaziri wa pande zote mbili. Sasa leo wenzetu wamekuja hapa wametoka nje na wamekataa, sasa inatumika ile *aljununu fununu, al-akilifani wahida*, ndio inayotumika hivi sasa. (*Makofi*)

Mhe. Spika, mimi ninaikubali na ninaiunga mkono na kuidhinishwa kwa fedha hizi bilioni thalathini na tatu, mia tatu milioni na sitini na laki tatu zifanye kazi, ili

maendeleo yetu yapate kuendelea. Tusinge kufanya kazi, desturi ya mpinzani hawezu kukusifu hata umfanyie jema, na hata mpinzani akikusifu anataka kukuumiza!

Kwa hivyo, mimi ninaunga mkono Mswada huu ufanye kazi ili maendeleo yetu yapate kusonga mbele. Lau kama ingelikuwa mpinzani anamsifu mwenye kuendesha Serikali, basi Marekani wasinge kwa vyama vya upinzani. Kwa sababu kila kitu kipo, sisi tunakwenda kiko, sisi tunakwenda ku-copy Marekani ,China, lakini mote humo mnakuwa na upinzani, kwa sababu mpinzani hawezu akakusifu, na ndugu zetu hawa ni wapinzani hawawezi wakatusifu sisi.

Mhe. Spika, naunga mkono hoja ahsante sana.

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe ninahimiza kwamba jambo hili ni kubwa, jambo hili ni muhimu tuache kutangatanga, kutokatoka nje kwenda hapa na pale, hapana! Tuimalize kazi hii, kwa hivyo tulioko nje tuingie ndani tumalize kazi, nikiona tu *quorum* imetimia namwita Waziri, na wengine nitakuwa ninawaomba radhi sana, kwa sababu hili jambo ni muhimu hili, ndio limemalizia bajeti yote na kuidhinisha matumizi ya Serikali. Kwa hivyo tujitahidi sana, tutulie humu ndani ili tufanye kazi hii tuimalize.

Naomba nimkaribishe sasa Mhe. Viwe Khamis Abdalla, afuate Mhe. Mgeni Hassan Juma na Mhe. Ali Salum Haji anajitayarisha.

Mhe. Viwe Khamis Abdalla: Ninakushukuru Mhe. Spika, na mimi kunipa fursa hii ya kuweza kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Serikali.

Mhe. Spika, nichukue fursa hii nimpongeze Mhe. Waziri wa Fedha na watendaji wake wote, nimpongeze Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuwa mvumilivu kwenye Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Spika, ningekuwa mimi basi nisingeweza kuvumilia kwenye Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa. Serikali hii tulitegemea itatuletea maendeleo zaidi kwenye nchi hii, itatuondoshea vurugu la kisiasa kwenye nchi hii. Itadumisha amani kwenye nchi hii, lakini Mhe. Spika, cha kusikitisha kabisa amani ya nchi hii hao waliotaka Serikali ya Umoja wa Kitaifa ndio wanaotaka kuivunja.

Mhe. Spika, mimi binafsi sishangai kwa kutoka hawa Wawakilishi wa Chama cha CUF kwenye Baraza hili, kwa sababu tumeshazoea tunawaona kila siku wanatoka Bungeni na hapa ndani ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, naona bado haijawa suluhisho kwa kutoka wao tu Wawakilishi wa Chama cha CUF humu Barazani, bado kuna kichwa, hicho kichwa basi nacho kitoke kwenye Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa waende wakafanye kampeni pamoja!

Mhe. Spika, mswada huu wa fedha ndio mswada utaoondosha malalamiko ya wagonjwa wanapokwenda hospitali na malalamiko ya barabara.

Kwanza niipongeze Serikali kwa kuona umuhimu wa kututafutia mradi wa kutengenezwa barabara inayotoka Chake Chake na kwenda Wete. Barabara hii tokea nipate fahamu zangu naiona iko hivi hivi hajabadi, na sasa hivi imezidi barabara hii kuwa chafu, kuwa mbovu kabisa!

Mhe. Spika, niipongeze Serikali kwa kuona umuhimu wa kuishughulikia barabara hii inayotoka Chake Chake kwenda Wete. Mradi wa Barabara inayotoka Ole/Kengeja, barabara hii ni muhimu sana kwa wananchi wa Jimbo la Ole mpaka Kengeja.

Mhe. Spika, hawa wenzetu wakati wa kupitia bajeti kwenye mawizara walikuwa wana hoja nyingi ya kuiponda Serikali hii, ya kuidharau Serikali hii kama haina maendeleo wakati na wao wamo ndani ya Serikali hii hii.

Mhe. Spika, leo wametuhidhirishia kabisa kama Serikali ya Umoja wa Kitaifa hawaitaki tena. Nimuombe Mhe. Hamza, ile hoja binafsi ailete ndani ya Baraza hili, tumechoka!

Vijana wa Zanzibar wanategemea kama sisi viongozi wao ndio tutakaodumisha amani katika nchi hii, wakati sisi ndio tunaosababisha vurugu katika nchi hii, leo wametoka humu wako wapi? Nia yao waende wakafanye fujo na wao huko, hiyo ndio nia yao. Nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar kwa kuisimamia amani hii katika nchi hii.

Mhe. Spika, siku zote mwenye macho haambiwi tazama na siku zote mfa maji haachi kutapatapa, utatapatapa kwenye bahari huko utazunguka mwisho Mwenyezi Mungu atakujaalia uthaokoka au Mwenyezi Mungu atakujaalia atachukua amana yake. Na hawa wenzetu wameshatapatapa siku nyingi kabisa, nia yao wanataka waingie Ikulu, lakini Ikulu haichezewi kwenye majukwaa, na Ikulu haipatikani kwenye majukwaa, Ikulu inapatikana kwa vitendo, nia safi na uongozi bora.

Na hawa wenzetu hawana nia safi, wanakaa huko kwenye Baraza la Mapinduzi wanapanga mambo sisi wenyewe hatu yajui wanakuja humu ndani

wanayakataa kabisa. Wakifika kwenye majukwaa wanasesma aa mimi sishirikishwi natolewa nje, unatolewa nje saa ngapi wakati wewe ndio Kiongozi Mkuu.

Mhe. Spika, Serikali ya Umoja wa Kitaifa narudia pale hatuitaki tumeshaichoka, japo siku tano tuongezee ili tujadili hili jambo la Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Spika, Serikali watuonee huruma wasitunyime uhuru. Baraza lilipangwa mpaka tarehe 30, leo tarehe 30 tayari zishaondoka, japo bure sisi hatuhitaji pesa tupo hapa kwa ajili ya kuwatumikia wananchi wetu waliotuchagua, tuje humu tuwatetee wananchi, na tuko tayari kuwatetea wananchi. Lakini hao wananchi huko Serikali ya Umoja wa Kitaifa hawaitaki kwa vitendo vyao, hawaitaki hasa hata kuiona, na siku zote Mhe. Spika, mpewa hapokonyoki, utazunguka atabakia pale pale, utasoma dua, utashona sanda, utazika, lakini mpewa yuko pale pale!

Mhe. Spika, kuna kitu kinanishangaza kwa upande wa kule Pemba kuna Mfuko huu wa Jimbo. Mfuko wa Jimbo kila baada ya kipindi cha bajeti wanaidhinishiwa shilingi milioni kumi na tano lakini cha kushangaza kule Pemba hakuna maendeleo wanayoyafanya. Maendeleo yote yaliyoko Pemba yanafanywa na Serikali hii iliyopo madarakani, leo mnachukua pesa milioni kumi na tano mnakwenda kuwapa hawa Wawakilishi wa *CUF* wanajenga matawi yao, wanajenga majimbo yao, haina haja tena ya kupewa hizi pesa, ni bora kama Serikali wana pesa wawape mayatima na watu wanaoishi kwenye mazingira magumu.

Serikali isimamie yenyewe maendeleo ya wananchi. Kuna barabara za vijijini Pemba kule juzi nimepiga kelele hapa na Jimbo lile la Ole likuwa na Waziri wa Miundombinu, na kijiji kile Waziri na yeze jimbo lile lote yumo.

Mhe. Spika, juzi nimepiga kelele hapa kutokana na ahadi ya Mhe. Rais, na wizara ile inasimamiwa na mtu anayetoka Chama cha *CUF* mpaka leo ahadi ile iko pale pale. Ahadi ya Rais unaichezea! Rais akitoa tamko tu inatakiwa ahadi itekelezwe, na Rais ndiye mwenye nchi hii, au wanafelisha makusudi ili ioneokane kama Serikali iliyopo haitaki kunini?

Mhe. Spika, mengi tumeshayasema, tunataka vitendo. Hawa wameshajitoa kwenye Baraza hili waondoshwe kwenye Uwaziri, wawajibishwe mara moja, na kichwa chake kiondoke! Maana hiyo nguu mbele nguu nyuma, miguu ishaingia bado kichwa! (*Makofi/Kicheko*)

Mhe. Spika, kwa niaba ya vijana wangu wa Zanzibar wote na Mkoa wa Kaskazini Pemba, naunga mkono Mswada huu wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2015/2016.

Mhe. Spika, naunga mkono. (*Makofî*)

Mhe. Mgeni Hassan Juma: Mhe. Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi kuweza kuchangia katika sheria ya kuidhimisha makisio na matumizi ya shilingi bilioni mia nane na thalathini, mia tatu na sitini milioni na laki tatu kutoka katika Mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali kwa mwaka wa fedha unaoishia siku ya tarehe 30 Juni, 2016 na kuruhusu utoaji na uhaulishaji wa fedha hizo pamoja na mambo yanayohusiana na hayo.

Mhe. Spika, mimi nitangulize kwanza pongezi nyingi sana kwa Wajumbe wote ambaeo wamechangia, na niseme tu kwamba jeshi tunalo, jeshi tunalo na vita tunaviweza! Sasa wakati umefika tuone tutumie mbinu gani ya kuhakikisha kwamba haya mambo sasa tunayaweka sawa.

Mhe. Spika, mzoea vya kunyonga, vya kuchinja haviwezi. Tulikuwa hapa tunakamatana, tunazungumzia amani na utulivu wa Taifa letu, ambalo kila mtu anataka amani na utulivu. Lakini tukiendelea hivi wakati ambapo tumeshakaa sawa vizuri, wenzetu wanaanza kugeuka kama wanavyosema nyimbo yao, mguu mbele, mguu nyuma. Hatuwezi kwenda hivi, amani haitafutwi hivi, utulivu hautafutwi hivi! (*Makofî*)

Mhe. Spika, wakati tuko humu ndani ya Baraza tunaona namna ya wenzetu wanavyolia wivu kwa kuona kwamba tunaendelea. Wanalia wivu kwa sababu wanaona Ilani ya Chama na Mapinduzi imetekelezeka kwa asilimia 90 na wanaona mambo mazuri yanakuja. Sasa wivu huu Mhe. Spika, unaujua wivu, roho mtu inauma, anafanya vitu ambavyo havielekei, kwa sababu ya wivu basi ye ye anaweza kufanya chochote. Lakini mnaona wivu nini? Maendeleo mnayakataa wenywewe, kwa nini muone wivu? (*Makofî*)

Mhe. Spika, niseme tu, nimuombe sana Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar naomba sana Dkt. Ali Mohamed Shein Katiba inakupa uwezo, kifungu cha 43 (5) kinakupa uwezo wa kufanya kazi yako na umetuhidi Mhe. Rais. Kwa hiyo, tunaomba utekeleze, haiwezekani leo mawaziri ambaeo wanatakiwa wasifanye maamuzi yoyote bila kupata muongozo wa Makamu wa Pili wa Rais ye ye ndiye kiongozi wao, lakini leo wanafanya maamuzi ya kutoka wanatoka tu. Sasa Mhe. Spika, mimi nataka kusema hivi wanamgomea nani?

Mwalimu Julius Kambarage Nyerere alitwambia gomeni lakini mkigomea nyinyi Watanzania mniamgomea nani? Maendeleo ya nchi hii yanatuuhaji sote. Sasa wao kama wamechukua mpira wamewewka kwapani, wameondoka, wanataka kuzuia bajeti kazi yote tulioifanya kipindi chote kwamba tusiitekeleze, hapa itatekelezeka, kwa sababu tunaweza hapa itakuwa, na tutaipitisha bajeti na

tutaendelea kuleta maendeleo ya Taifa hili. Kina mama, watoto, vijana, wazee wanaihitaji bajeti hii ianze kufanya kazi, wakiondoka, wakibaki, bado tutaweza kuendeleza Taifa hili. (*Makofî*)

Mhe. Spika, mimi nasikitishwa sana, lakini saa nyengine huwa najiuliza. Unajua kuna nyimbo yao moja huwa inanifurahisha sana, mimi siku zote nikiisikia huwa najiuliza, wanajizomea ooh, ooh, ooh halafu wanauliza chama gani hiki? Wao wenyewe, chama hawakijui, halafu wanajibu, umesikia lini CCM wakafanya hivyo. CCM wakianza kuimba wanaiimba CCM na wanaisifu CCM moja kwa moja, ndio kwa sababu hiyo.

Sasa Mhe. Spika, mimi nasema hivi, nawaomba ndugu zangu walioko nje wote ambao wanapenda maendeleo na Taifa hili warudi, tuupitishe mswada huu, ili sasa tuanze kuzitumia fedha zetu, asotaka akalale mbele ya safari, lakini tutaendelea!

Mhe. Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii, ahsante sana. (*Makofî*)

Mhe. Spika: Nilisema nitaingia kwenye safu ya mawaziri, lakini Waheshimiwa wengine wawili wamehamasika nao wapate kuchangia, na mimi nakubali wachangie. (*Makofî*)

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Spika, na mimi nikushukuru kwa dhati kabisa kwa kunipa fursa hii kuweza kuchangia hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Fedha.

Mhe. Spika, mimi nianze kwa kumshukuru Mhe. Waziri wa Fedha ye ye pamoja na watendaji wake, ambao wanaongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha, Kaka yangu Sheikh Khamis.

Mhe. Spika, kwa nini niseme natoa pongezi? Natoa pongezi za dhati kabisa kwa namna ambavyo wameonesha jitihada zao za ukusanyaji wa mapato katika kipindi hiki cha miaka mitano tunayomalizia, na namna ambavyo wameweza kupunguza mianya ya uvujaji wa mapato.

Mhe. Spika, sote tunafahamu kwamba mwaka jana tulipitisha bajeti yetu ya 708.8 bilioni lakini jitihada zao zimetufikisha mwaka huu tunataraji kuitishia 830 bilioni. Hizi ni jitihada tosha, jitihada ambazo Mhe. Spika inapaswa tuziunge mkono kwa nguvu zote na tuwape matumaini ili hatimaye tupitishe bajeti hii, wananchi wa nchi hii wapate kwenda kufarijika na yale matunda ya nchi yao.

Mhe. Spika, jitihada hizi ndizo zilizowapelekea wenzetu hatimaye kulikimbia Baraza. Mhe. Spika, mpinzani ye yote huwa anataraji serikali iliyoko madarakani ifanye vibaya, lakini kwa miaka minne hii serikali hii imekuwa ikifanya vizuri

mwaka hadi mwaka. Sasa hili limeanza kuwakatisha tamaa, kwa sababu tuna muda mfupi inabidi turudi kwa wananchi kwenda kuwaeleza tumefanya nini ili watupe matumaini tena ili tumalizie nini. Hawana jambo la kwenda kuwadanganya wafuasi wa chama cha upinzani.

Mhe. Spika, hawana jambo kwa sababu ndani ya miaka minne hii tumeshuhudia jitihada za serikali katika kutekeleza miradi mbali mbali ikiwemo barabara, maji safi, hospitali Unguja na Pemba na tayari Mhe. Waziri wa Fedha ameshaanza kutueleza mipango mizuri ya serikali baada ya kuitisha bajeti hii. Sasa hili linawafanya waanze kukata matumaini.

Mhe. Spika, mimi mara nyingi huwa ninasema hapa, na ninapowaambia wanafikiria labda tunakuwa tunawatania. Mheshimiwa kunguru hafugiki, unajitahidi kadri ya kumfunga lakini hiyo ndio kudra ya Mwenyezi Mungu aliyomjaalia kwamba huwezi kumfuga mnyama anayeitwa kunguru.

Sasa sisi wengine Mhe. Spika, hatuoni ajabu hawa kutoka, na tunajua watarudi kwa sababu siku ya kufunga Baraza bwana wao atakuwemo ndani, labda na bwana wao humu ndani asije, tunajua kama itakuwa hajaja na wao ndio watakuwa hawaii. Lakini tuna imani siku ya kufunga Baraza wao watarudi ndani humu kuja kujumuika na sisi kwa sababu hiyo ndio kawaida yao, ndio kunguru alivyo, anaruka huku, anaruka huku matokeo yake anaingia kwenye tundu ananasa na kazi inakuwa imekwisha.

Mhe. Spika, kwa kuendelea mimi nasema tena ninawashangaa tena wanani pa tabu sana, kwa sababu kauli iliyotolewa na Mhe. Juma Duni kabla ya kutoka na kukimbia katika Baraza hili anasema kwamba hakuridhika na suala zima la uandikishaji wa daftari.

Mheshimiwa kama hukuridhika nchi hii inaendeshwa kwa mujibu wa taratibu za sheria na kanuni, Tume ya Uchaguzi ipo katoe malalamiko katika suala zima la uandikishaji. Lakini kubwa zaidi ambalo Mhe. Spika, linanipa mshangao kwamba karibuni ya Wajumbe wa chama cha upinzani ni kutoka Pemba, na Pemba daftari limeshamalizika wamefanya walivyofanya sisi mbona hatukutoka. Sasa kama tatizo la daftari katika Mkoa wa Mjini Magharibi basi walikuwa watoke wawakilishi wa Mkoa wa Mjini Magharibi, kwa sababu wawakilishi wa Pemba daftari wameshalimaliza lote na wameridhika na hali nzuri.

Mhe. Spika, nawaonea pole sana wananchi wanaowatumikia vyama vyaa upinzani. Unapokuwa Mwakilishi maana yake unatumikia wananchi, na unapowatumikia wananchi serikali hii inakuwa inalipa malipo kwa kuwatumikia wananchi wetu. Sasa mimi nataka kuwaauliza hawa ndugu zangu wa Pemba ambao wanatoa ridhaa

ya kura wametoa kura kwa Wawakilishi wao, wakawatumikie Darajani? Maana yake kama kuwatumikia wananchi ndio kwenye chombo hiki, kama kulikuwa kuna matatizo walikuwa waeleze ili tupate kuyajadili na kuyapatia ufumbuzi.

Mhe. Spika, kutoka kwao ni hasara kubwa zaidi, kwani Mhe. Spika bajeti hii kama haikupitishwa maana yake serikali itashindwa kufanya matumizi, na mionganoni mwa matumizi ambayo Mhe. Waziri wa Fedha ameyaandika katika kitabu chake kuna matumizi katika Tume ya Uchaguzi bilioni 7.5 kufanikisha uchaguzi wa nchi hii. Sasa ah wao wanatoka pesa hazijapitishwa huo uchaguzi uko wapi?

Mhe. Spika, asiyejijua hajitambui, maana yake kutoka kwao ni kwamba Mhe. Shein aendelee madarakani mpaka tuchoke. Eeh ilikuwa wakae tupitishe bajeti twende katika uchaguzi, sasa kama hatukupitisha bajeti hii maana yake uchaguzi hakuna.

Kwa hiyo, mimi Mhe. Spika, nataka niwaeleze wananchi wa nchi hii pamoja na wale Wawakilishi walioamua kutoka, ni kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Dkt. Ali Mohamed Shein kuititia tiketi ya Chama cha Mapinduzi niliwaambia kwenye kuchangia vitambulisho wakitaka tunashinda, hawataki tunashinda, na tuna sababu za msingi za kusema hayo. Tumefanya mambo mazuri miaka mitano hii ya Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein, wananchi wameridhika na matunda ya kiongozi wao.

Mhe. Spika, lakini la pili tuna mtaji mkubwa kwa wananchi, tuna mtaji mkubwa kwa Wawakilishi, tuna mtaji mkubwa kwa viongozi wa serikali hii, hili halihitaji tochi.

Mhe. Spika, nataka nieleze machache sana katika kulithibitisha hili, kwamba walitwambia hawa Katiba ya Serikali mbili haiwezekani kuja, matokeo yake tumewapiga bao. Wakatwambia ndani ya Bunge la Katiba kwamba kwa Zanzibar hatuwezi kupata *two thirds* ya Wabunge wa Bunge Maalum la Katiba. Tumepata *two thirds* matokeo yake Katiba iliyopendekezwa tumeipitisha, na leo tunataka tuwaeleze kwa uwezo na nguvu kubwa ya Wajumbe wa CCM bajeti hii tutajadili na hatimaye tutaipitisha kwa nguvu zote. Kwa sababu idadi na nguvu ya Wajumbe wa Chama Tawala tunatosheleza kufanya maamuzi katika Baraza lako.

Mhe. Spika, wao waache waendelee na mambo yao lakini mimi napata mshangao yaani mwanadamu sijui tumtendee jambo gani kadri ambavyo tunajitahidi tulikuwa tuna mambo mengi, Mwenyezi Mungu amrehemu Mhe. Salmin Awadh Salmin ilitaka kuletwala hoja binafsi lakini watu wakasema aah tuwastahamilie wenzetu labda watakuwa waungwana lakini wenzetu ni wanafiki kabisa.

Mhe. Spika, mimi hawa *backbenchers* wenzangu sishangai wakati mwengine, kwa sababu tushawazoea, lakini nawashangaa zaidi hawa mawaziri, unapokaa kitu cha mbele hukai kama wewe mpinzani, unakaa wewe ni serikali. Maana yake unatakiwa uitumikie serikali yako, leo wenzetu wametoka wameviacha viti vitupu. Lakini nataka kushangaa ah, nguruwe haramu mchuzi wake halali, maana yake mawazo yangu Mhe. Spika, walipotoka kuvikataa viti nya serikali nilifikiria wakitoka nje watatafuta tekci na zile gari za serikali wazikatae. Mwenyezi Mungu anasema *almunafikuuna walmunafikati finary jahanam*. Mnafiki mwanaumke na mnafiki mwanaumme Mwenyezi Mungu atawaangamiza katika moto wake wa jahanam, kwa sababu unafiki ndio kama huu ambao wameonesha, kwa sababu wewe unajifanya mserikali kwa yako unayoyataka wewe na chama chako, lakini unapokuja katika masuala ya maslahi ya nchi katika kuitisha bajeti ya nchi hii ili wananchi wa nchi hii wapate kwenda kulitumikia Taifa lao, wagonjwa wa nchi hii wakapate matibabu baada ya kuitisha bajeti, watu ambao wanahitaji huduma mbali mbali wanasubiri ifike Julai 1 tuptishe bajeti ili wakatumie katika mazingira mbali mbali, wewe unaondoka watu wateseke katika nchi hii, kama si unafiki ni kitu gani, Mwenyezi Mungu atawahukumu tuko duniani *Inshaallah*. (*Makofî*)

Mhe. Spika, unafiki huo ndio narudia pale pale, kama wamekataa kukalia viti nya serikali wakatae mambo yote, hebu waandike barua kwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha kwamba wamekataa kiinua mgongo na maposhoto mengine kwa sababu serikali hii haiendeshi mambo vizuri. Eeh, usigomee hili jengine unalitaka, wagome yote, ndio ninaposema hawa watu mheshimiwa wanafiki, lakini tutajitahidi kutoa taaluma, Shekhe wangu pia Abdalla Juma kaingia mitini mimi nashangaa hasa na yeYe ndiye mcha Mungu, Mwenyezi Mungu pia katika aya zake anasema *innallaha ghafuuru rahiim*, hakika ya Mwenyezi Mungu ni mwingu wa kusamehe.

Neno la Mwenyezi Mungu linaitwa *Allah*, lakini hapa Mhe. Spika naomba ninukuu kidogo neno la Mwenyezi Mungu limetiwa *fat-ha* baada ya kuitwa *Allah* imeitwa *inallah maaswaabiriina*, hakika Mwenyezi Mungu yuko pamoja na wanaosubiri. Sababu ya kutiwa *fat-ha* ni kutia nguvu hili neno, wenyewe wanasema *harfi attawkid wannasbi*, unalinasibisha neno la mbele kulibadilisha vile utakavyo.

Sasa tusameheane tunamaliza muda na nina imani na wao Mwenyezi Mungu atawasamehe, wameshafanya dhuulma kubwa sana katika nchi hii. Mwanadamu ili upokee rizki halali maana yake unatakiwa ukitumikie kile kitu ulichokiapia kwa uhalali kabisa, lakini wanachukua rizki halali, wanachukua rizki ambazo sisi tunawapa kwa ajili ya kuwatumikia wananchi, lakini wao wanachukua mishahara na maposhoto kwa kukimbia kuwatumikia wananchi. Hii fedha haiwastahikii kwa mujibu wa aya za *Qur-an*, kwa mujibu wa hadithi za Mtume Muhammad (S.A.W),

wanachokichukua wanachukua haramu, kwa sababu wanachukua bila ya kuwatumikia wananchi wa nchi hii.

Mhe. Spika, hili sisi hatushangai, haya ni mazingira yaliyoandaliwa kwa muda mrefu, hawa watu walikuwa wanatafuta kila namna lakini kila wanalolitafuta kwa sababu ya utiifu wetu wana CCM, kwa sababu ya mambo ambayo sisi wana CCM Mwenyezi Mungu katujaalia tuna subira, tuna hekima, tunajua nini maana ya kuongoza na ndio maana tukawa tunaishi na wenzetu kwa muda mrefu sana. Lakini kama si hekima za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa CCM, ingekuwa zamani tushaondoka, zamani ingekuwa tushapigana.

Matukio mengi yametokezea lakini subira zetu, utiifu wetu, imani yetu kwa serikali na wananchi ndio imetufikisha hapa, na Mwenyezi Mungu *Inshaallah* kwa uwezo wake atatujaalia jahazi hili tutalivusha kwa salama salmini, hatimaye Rais aje alivunje rasmi Baraza hili kwa hekma na salama na amani.

Mhe. Spika, wananchi wa nchi hii wote mashuhuda, na leo nataka niulize katika Baraza hili, hivyo nyinyi hamshangai bajeti hii jinsi ya kuigomea hawa wanafuata mkumbo tu wa mabwana zao? Miezi mitatu hapa Mhe. Ismail Jussa, haingii Barazani, na Mhe. Spika, sijui kama una taarifa ya Mjumbe kutoingia katika Baraza, anachukua haki za Baraza, ndipo niliposema Mwenyezi Mungu atawaangamiza kwa matendo yao.

Mhe. Spika, wengine walisoma madua makubwa hapa, kaka yangu mnadhimu mimi nilifikiri kwa utukufu wa mwezi huu mtukufu wa Ramadhani angetumia hekima za kuangalia aya za Mwenyezi Mungu na hadithi za Mtume Muhammad (*S.A.W*) kuwaelekeza wenzake kukimbia dhulma. Mheshimiwa waende wakafungue na wake zao wanywe maji, hawana sababu ya kufunga.

Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa kusema kwamba sote tunaelewa hii mipango haikuanzia Zanzibar, mipango imeanzia Bara, na hii ndio mikakati ya UKAWA. UKAWA utabakia kwa mabwana zao Dar es Salaam, Zanzibar hakuna upawa, mwiko wala sufuria. Wajumbe wa CCM tunatosha, tuna uwezo wa kutoa maamuzi katika Baraza hili Tukufu.

Mhe. Spika, baada ya dibaji hiyo ndogo na masikitiko kabisa ya kuwaonea huruma ndugu zangu wa chama cha upinzani, kwa namna wanavyokula dhulma, na kwa namna Mwenyezi Mungu alivyowaandalia moto kesho akhera, kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Kwahani naunga mkono hotuba hii. Mhe. Spika, nakushukuru ahsante. (*Makofit*)

Mhe. Amina Iddi Mabrouk: Mhe. Spika, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia kuwepo hapa ndani ya Baraza lako, lakini zaidi kusimama na kuweza kutoa mchango wangu huu mfupi kwa manufaa ya wananchi wetu wa Zanzibar.

Mhe. Spika, niombe radhi kwanza, kwa sababu hali yangu sio nzuri sana leo, kifua kimenishika na ndio maana sauti haiko vizuri, lakini niseme kwamba nimehamasika na ndio maana nimekuletea *ki-note* muda si mrefu.

Nimehamasika kwa namna wenzetu wa Chama cha *CUF* jinsi walivyoamua kutoka ndani ya Baraza hili, lakini mimi niseme kwamba hawakutumia hekima lakini zaidi hawakufanya kitendo cha uungwana.

Mhe. Spika, mimi nime-*notice* kitu leo ndani ya Baraza sijui wenzangu wameki-*notice*? Tokea muda ambao wametoka hawa wenzetu kwa kweli Baraza limechangamka kuliko lilivyochangamka wakiwepo wao. Baraza limehamasika, Waheshimiwa Wawakilishi wa CCM wamechangamka, na hii inaonesha kwamba jeshi tunalo ndani ya Chama cha Mapinduzi, jeshi liko imara kutetea maslahi ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, inaonekana kwamba kuwepo kwao *CUF* wanatudumaza, kuwepo kwao ndani ya Baraza la Wawakilishi wanatufanya tuwe legelege, *tu-relax*. Lakini kubwa zaidi kutoka kwao ndani ya Baraza hili limewadhihirishia wananchi wote wa Zanzibar kwamba Wawakilishi wa Chama cha Mapinduzi wanafaa kutuongoza, na pia wako imara kuhakikisha kwamba wanatuletea maendeleo wananchi wa Zanzibar. (*Makofit*)

Mhe. Spika, kutoka kwa Wawakilishi wa *CUF* kwa kisingizio cha uandikishaji mimi niseme kwamba sio kweli kuwa ni kisingizio cha uandikishaji, kwa sababu kama wana maneno ya kusema walikuwa wawemo humu ndani na waseme kinachowasibu. Lakini ni dhahiri kwamba kutoka kwao wameona ngoma ni nzito, wameona nje kugumu, wameona wananchi wa Zanzibar wamehamasika kuhakikisha kwamba wanakipigia Chama cha Mapinduzi na kitashinda kwa nguvu zote.

Mhe. Spika, mimi niseme kwamba hivi tulivyokuwemo humu ndani kwa kipindi chote hiki cha miaka mitano, wananchi huko kwa taarifa yako walioko nje wanatutathmini, wanatusoma, wanatuangalia kama chama gani kinatufaa kuwapa madaraka.

Kwa hiyo, niseme Mhe. Spika, usione tumo tu, wananchi wanakwenda na pirika zao ukawaona hawana macho, wananchi wa Zanzibar wana akili timamu,

wananchi wanaweza kupima mambo, wananchi wana uwezo wa kujua hili jiwe na hii kokoto.

Mhe. Spika, nikuhakikishie kwamba wananchi wa Zanzibar wameshatupima na washasema wanatuchagua kwa asilimia kubwa kabisa. Pia wamesema kwamba watatuchagua kwa asilimia kubwa kuliko walivyotuchagua miaka iliyopita. Kwa hiyo, niseme wenzetu wametoka kwa sababu hawana la kuwaambia wafuasi wao wa *CUF*, kwa sababu washawadanganya sana, kwamba miaka mitano hii tutashinda, ngoma ikifika CCM inachukua, inaweka, waa.

Miaka mitano mingine wanawaambia *CUF* itashinda, wakati ukifika CCM wanachukua, wanaweka, waa tunaendelea mbele. Nataka niseme na kipindi hiki wakati ukifika wananchi wa Zanzibar watakipigia Chama cha Mapinduzi kwa asilimia kubwa kabisa.

Mhe. Spika, sio hilo tu, hawa wenzetu walijua kwamba Dkt. Ali Mohamed Shein hachukui fomu wakaanza kusema oo anakwenda Bara, sasa mwanamme siku aliyochukua fomu wenzetu walishituka, mwanamme siku aliyojitungaza na kuwaambia wananchi pale Ofisi Kuu ya CCM walilala, waliingia maji na wakaona kwamba sasa tufanyeje, tuanze kuharibu mapema.

Mimi niseme kwamba Mwenyezi Mungu mkubwa, sote tunamtegemea yeye na Mwenyezi Mungu anatujua sisi waja wake nia zetu, na niseme kwamba Mwenyezi Mungu hayuko pamoja na wao na ushahidi upo.

Bunge la Katiba walijilabu kwamba hatutofikia asilimia, matokeo yake wakatoka, walipofika Unguja wakajuta kwa nini wametoka.

Sasa niseme kwamba, Mwenyezi Mungu hayuko pamoja, naona Mwenyezi Mungu anayelitaka yeye ni *Kun-fayakun*; panda, shuka, lakini Mwenyezi Mungu yupo, halali usiku wala mchana, na Mwenyezi Mungu bado anatupenda Chama cha Mapinduzi, na anajua kwamba chama hiki kinawatakia mema wananchi wa Zanzibar, na Mwenyezi Mungu bado anataka Chama cha Mapinduzi kibaki madarakami, na hakuna wa kutuondosha isipokuwa yeye *Subhana Wataala*.

Mhe. Spika, kipindi cha Dkt. Salmin Amour Juma alisema hataki mseto wala ubwabwa, sisi vijana tukasema tutumie hekima Dkt. Amani Abeid Karume akafanya busara, akaona labda wenzetu wamebadilika, labda wenzetu wamekua, labda sasa wamefahamu, lakini kumbe masikini wamesema wenzangu hapa.

Mhe. Spika, mimi nataka niifafanue nyimbo ambayo amesema Mhe. Mgeni Hassan ambayo wanaitumia sana wenzetu. Chama cha Mapinduzi kikianza katika mikutano yao kinaanza, Chama chetu cha Mapinduzi chajenga nchi, CCM eee,

lakini wenzetu *CUF* wanaanza: ooo ooo ooo, wanaulizana Mhe. Spika, chama gani. Sasa mimi nikwambieni wao wenyewe hawajitambui, hawajijui, hawajifahamu wanaulizana chama gani, tena kwa hukoo kama waliosukumwa hivi, Chama cha Wananchi *CUF*. (*Kicheko*)

Mhe. Spika, wewe umeshatembea sana nchi za nje, na sisi tumeshatembea sana umeyaona wapi hayo, chama kinataka madaraka, chama kinajiona ye ye mwamba lakini hawajitambui wala hawajifahamu.

Mhe. Spika, nakuona unaanza kuangalia dakika zako hapo lakini nikwambie kwamba leo tumeemasika, na niseme kwamba bora wasije tena humu kumbe tunaweza, mliokuwa mnadhani hatujui kusema leo tunesema, na hii yote kwa kuhamasika tu, tukihamasishwa tunahamasika!

Mhe. Spika, sikufichi nina hakika wako kwenye televisheni wanatutizama, na kwa kweli wanajua kwamba wanaume wapo leo, wanaume wananguruma ndani ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Spika, kwa kumalizia naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mhe. Salma Mussa Bilali: Mhe. Spika, na mimi kwanza kabisa sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwangi wa rehma kwa kunijaalia leo kuwepo hapa katika Baraza lako Tukufu na kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Makisio na Matumizi ya Mwaka 2015. Pia nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii.

Mhe. Spika, na mimi kwanza sina budi nimshukuru au nimpongeze Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na watendaji wake wote kwa kazi na juhudhi yao kubwa wanayoifanya, na kusababisha pato la serikali ya nchi hii lionezeke kwa asilimia hiyo ambayo imetajwa.

Mhe. Spika, pia napenda niwapongeze mawaziri wote wa CCM pamoja na Wawakilishi wa CCM kwa uamuzi wao wa kuendelea kubaki katika Baraza hili Tukufu, na kuweza kuchangia Mswada huu wa Sheria na bila ya wasiwasi wowote kuupitisha.

Mhe. Spika, nitakuwa sijawatendea haki wanawake wa Zanzibar na wa Mkoa wa Kusini Unguja kama sitalaani vikali kitendo hiki walichofanya wenzetu leo cha kutoka katika Baraza hili Tukufu, na kuacha mambo muhimu sana ya faida kwa wananchi wao ambao wamewachagua, na kutoka kwenda kufanya vurugu nje ya Baraza.

Mhe. Spika, mimi nataka kusema kwamba maendeleo ya nchi hii hayapatikani kwa mgomo, kitendo walichokifanya si cha kiungwana. Kwa sababu humu mna Wizara

ya Biashara, Viwanda na Masoko, Wizara ya Afya, Wizara ya Miundombinu na Mawasiliano na nyengine ambazo wanaziongoza, wao mawaziri ndio waliosimama hapa wakaomba kuidhinishiwa pesa hizi ili wapatiwe katika wizara zao na waweze kupeleka maendeleo kwa wananchi, lakini cha kushangaza ni kwamba leo wametoka katika hatua ya mwisho ya kumalizia suala hili na wameacha kazi hii nzito.

Mhe. Spika, kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu sisi tutachangia, tutaidhinisha na tutapitisha matumizi haya. Hivi bila ya kuidhinisha fedha hizi kuna mambo mengi mno ambayo wenzangu wameshasema, mimi sitosema sana lakini yapo mambo ya maji, afya, elimu na mengi mengineo. Bila ya kuidhinisha haya yatapatikana wapi?

Mhe. Spika, mimi ninarudia tena kulaani kitendo hichi walichokifanya na kusema kwamba si uungwana.

Mhe. Spika, mimi sitokuwa na mengi sana ya kusema, kwa sababu mengi wameshasema wenzangu, isipokuwa nimenyanyuka angalau na mimi kuunga mkono ioneckane kwamba Wawakilishi wa CCM tupo katika Baraza hili na tunaendelea kuchangia na kuupitisha Mswada huu kama ilivyo kawaida. (*Makofii*)

Mhe. Spika, nimesikitishwa sana na kitendo alichosema Ndugu yetu Bhaa (Mhe. Hussein Ibrahim Makungu) hapa, kwamba alimsalimia Babu, lakini Babu akakataa salamu za Mhe. Bhaa. Babu ni mtu mzima, inaonekana Babu ana hekma na busara, halafu Babu huyu ni Muislamu, lakini leo hii Babu anakataa kusalimiwa.

Mhe. Spika, mimi nadhani huyu si Babu, huyu ni Babu wa mchovyo, Babu hasa hawezi kukataa kusalimiwa, na huyu Babu hafai. Wananchi wa Bububu mimi niwaambie huyu Babu hafai, huyu Babu ni wa mchovyo, Babu huyu atatiwa shimonii. Haiwezekani Babu atawekwa Wizara ya Nchi wakati Babu wenywewe hana maadili. (*Makofii*)

Mhe. Spika, mimi pia niunge mkono maelezo au maoni mbali mbali aliyotoa Mhe. Hamza Hassan Juma. Mhe. Rais nadhani anatuona na ameshasikia, ninachoomba kwa Mhe. Rais aondoe upole, atimize ile azma yake ambayo aliisema hivi karibuni, kwamba hatowavumilia wale wote ambaao wanaoleta ishara ya uvunjifu wa amani katika nchi hii. Kitendo walichokifanya leo ndugu zetu ni ishara ya uvunjifu wa amani katika nchi hii. Kwa hivyo Mhe. Rais naomba; Mhe. Makamu wa Pili wa Rais hayupo, Mhe. Waziri wa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais yupo, naomba suala hili lichukuliwe na lifanyiwe kazi mara moja tena. (*Makofii*)

Mhe. Spika, mimi labda niseme kwamba kwa hawa wenzetu, Mwenyezi Mungu hachezewi, na kuna siku hawa wenzetu walisoma dua ya *Istikhara*, lakini

kinachoonekana ni kwamba ile dua na waliyoisali ndiyo inayowadhuru na itaendelea kuwadhuru na itawamumunya mpaka itawamaliza. Mwenyezi Mungu hachezewi na hamfichi mnafiki.

Kama kweli ingelikuwa ile sala na dua inawastahikia wangekwishafanikiwa, lakini dua inawadhu na itawamaliza kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu. (*Makofî*)

Mhe. Spika, kwa niaba ya wanawake wa Zanzibar na wa Mkao wa Kusini Uguju nitakuwa sitotenda haki kama sitaunga mkono Mswada huu kwa asilimia mia moja. Hivyo Mhe. Spika, mimi ninaunga mkono Mswada kwa asilimia mia moja na mengi yameshasemwa na wenzangu ninaunga mkono pia hayo.

Mhe. Spika, ninakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Ahsante. (*Makofî*)

Mhe. Spika: Ahsante sana. Naomba sasa nimkaribishe Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, baadae Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko na atafuata baada ya hapo Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo: Mhe. Spika, ahsante kunipa nafasi na mimi ya kuchangia machache kuhusu Mswada huu ambao upo mbele yetu.

Mhe. Spika, kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia leo hii tutawa tupo hapa kwenye chombo hichi ambacho ni cha Serikali na ni cha Baraza la Wawakilishi.

Kwanza kabisa nianze kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, pia nimpongeze Mhe. Makamu wa Pili wa Rais kwa juhudzi zake anazozifanya kutekeleza majukumu yake ya Serikali, pia nimpongeze Mhe. Waziri wa Fedha, Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha pamoja na Afisa Mdhhamini Pemba wa Wizara hii. (*Makofî*)

Mhe. Spika, mimi nataka nitangulize kwa msemo huu, "Mchimba kisima huingia mwenywewe". Msemo huu unaashiria mambo mengi sana kuhusu wenzetu ambao leo wametoka kwenye hichi chombo ambacho ni cha Serikali na ni chombo cha Kutunga Sheria.

Mhe. Spika, mimi nianze kusema kwamba nikiwa ni Mwakilishi wa Mkao wa Kaskazini Pemba na nikiwa ni Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo Zanzibar. Ninawaomba sana wananchi wa Mkao wa Kaskazini Pemba

wanisikilize kwa utuo kabisa, ili maelezo yangu nitakayoyasema hapa wayafahamu vizuri kwa kina na halafu wayafanyie kazi. (*Makofî*)

Mhe. Spika, mimi Mhe. Rais ameniteua kuwa Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, ninasimama hapa kwa kusema kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetekeleza majukumu yake kwa hali ya juu hasa Kisiwani Pemba.

Mkoa wa Kaskazini tuna Wilaya mbili; kuna Wilaya ya Micheweni na Wilaya ya Wete. Mhe. Rais alipoteua Baraza lake la Mawaziri na Manaibu, kwa kweli alifanya ziara kwenye Kisiwa cha Pemba.

Mhe. Spika, ninayasema haya kwa uhakika, siyasemi kwa kugitagita. Mhe. Rais tulifanya ziara tukaenda Wilaya ya Micheweni kule Kiuyu Maziwa-ng'ombe kwenye maeneo huru yaliopo Micheweni. Mhe. Rais akazungumza na wananchi wa Micheweni. Wananchi wa Micheweni wakasema Mhe. Rais hatutaki utalii, Mhe. Rais akawaauliza kwa sababu gani, Mheshimiwa watakapokuja wazungu watatuchukulia watoto wetu, watatuchukulia wake zetu. Mhe. Rais akawaambia hiyo siyo sababu, niambieni sababu.

Mhe. Rais, pale akawasikiliza wananchi wale wa Micheweni, wakasema Mheshimiwa siyo kama tunaukataa utalii hatuukatai, lakini tunataka tujengewe viwanda.

Mhe. Rais kwa kweli akawakubalia wananchi wale wa Micheweni na akasema basi sisi tutakaa Serikalini ili tuandae mipango madhubuti tuweze kuja kuwajengea viwanda.

Mhe. Spika, kwa kweli bajeti hii juzi ilipopita kuna Mheshimiwa mmoja anatoka Jimbo la Micheweni alisema mambo mengi sana, lakini ninamshangaa akiwa ni Mwakilishi wa Jimbo lakini maendeleo yoyote hana anayoyafanya. Nikiwa ni Naibu Waziri na nikiwa ni Mwakilishi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba kuna mambo mengi ambayo nimeyatekeleza juu ya kuwa Mhe. Mwakilishi yule yupo Micheweni na anaposimama hapa Mheshimiwa yule anajinata amefanya hichi na hichi.

Mhe. Spika, ninataka wanisikie wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba hasa Jimbo la Micheweni, Waheshimiwa Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi munaotokea CCM mujue kwamba muna viongozi ambao ni madhubuti wanaotokea kwenye CCM na wanatekeleza wajibu wao siku hadi siku. (*Makofî*)

Mhe. Spika, kwa kweli Mhe. Waziri jana alipokuwa akifanya majumuisho alisema kama atatembelea maeneo huru, na kuna Waheshimiwa wamesema ili waongozane pamoja, namuomba Mhe. Waziri mimi nikiwa ninatokea kwenye Jimbo la Micheweni nakuomba sana Mhe. Waziri unapofanya ziara kwenye maeneo huru unichukue mimi nikiwa ni Mwakilishi ninayetoka Mkao wa Kaskazini Pemba, na ninaishi kwenye Jimbo la Micheweni maeneo yote ninayajua, na kama tunavyojua wenzetu hawa ni wanafiki, hawasemi kweli.

Juzi tu kulikuwa na mradi wa umeme wa juu Mhe. Spika, wanisikilize kwa kituo watu wa Jimbo la Micheweni, mujue kwamba viongozi hawa ni wanafiki na hawasemi ukweli.

Mhe. Spika, Micheweni kama tunavyojua kuna hali ya mazingira magumu, leo hii viongozi wale ndiyo wanaohamasisha Micheweni kusiwe na maendeleo yoyote, lakini Serikali hii imesimama kidete kupeleka maendeleo kwenye Mkao wa Kaskazini hususan Wilaya ya Micheweni. (*Makofi*)

Mhe. Spika, pia niingie kwenye Mswada huu, juu ya kuwa leo Mswada huu tutaupitisha kwa hekma na busara zetu tukiwa ni Wawakilishi wa Chama cha Mapinduzi. Mhe. Waziri hasa mimi nikupongeze na niwapongeze Mawaziri wa CCM pamoja na Manaibu Mawaziri wa CCM kwa kazi zao wanazozifanya kuanzia mwaka 2010 mpaka tumefika leo hii 2015 tunasimamia Serikali na Mhe. Spika, unatuona juhudhi zetu.

Sasa tuone kwamba wale waliotoka humu kuwa siyo viongozi bora, na ni viongozi ambao wanajali maslahi yao, hawawajali wananchi, na kama wanawajali wananchi Mswada huu leo hii wangekaa wakaweza kuidhinisha au kupokea Mswada huu na tukaweza kuupitisha kwa maendeleo ya jamii pamoja na wananchi kwa ujumla.

Mhe. Spika, wanawake wa Mkao wa Kaskazini nawaomba sana hususan Wilaya ya Micheweni kwenye Jimbo la Micheweni musicague kiongozi ambaye anajitakia yeye mwenyewe tu, muchague kiongozi ambaye anataka maslahi ya wananchi wote. (*Makofi*)

Mhe. Spika, haya yote tunayoyasema hapa ni uhakika, na sasa hivi leo hii ni bajeti ya mwisho, ninawaomba sana akinamama wa Mkao wa Kaskazini Pemba musimame kidete kuipigia kura CCM ili ishinde, ingawaje Pemba hatupati majimbo lakini tuna asilimia kubwa sana ya kura. Ninaomba sana wanachama wa Chama cha Mapinduzi wa Mkao Kaskazini Pemba musimame imara ili kukitetea Chama chetu hichi pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. (*Makofi*)

Mhe. Spika, kwa kusema hayo ninaunga mkono Mswada huu asilimia mia kwa mia, na ninawashukuru sana wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba walionichagua na nikaingia kwenye Baraza hili Tukufu.

Na ninawaomba sana ninawatakia kheri ya Ramadhani na ninawaomba sana Mwenyezi Mungu awajaalie awape hekma na busara, ili kuweza kunirudisha tena kwenye Baraza hili Tukufu nitekeleze majukumu ya Chama cha Mapinduzi pamoja na wananchi wa Mkoa wa Kaskazini Pemba. (*Makofî*)

Mhe. Spika, ninaunga mkono Mswada huu asilimia mia kwa mia na ninakushukuru. (*Makofî*)

Mhe. Spika: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri. Sasa ni zamu yake Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, afuate Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano.

Mhe. Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Spika, ninakushukuru kwa kunipatia na mimi fursa ya kuweza kuzungumza machache ili niweze kuunga mkono Mswada huu wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2015/2016.

Mhe. Spika, kama ilivyo ada tuanze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia sote tukawa wazima na wenye afya na tukaweza kufika hapa kutekeleza majukumu yetu. (*Makofî*)

Mhe. Spika, ninataka nianze kwa kusema kwamba ninaunga mkono Mswada huu wa Sheria ya Kuidhinisha Matumizi ya Fedha hizi Bilioni Mia Nane Thalathini, Milioni Mia Tatu Tisini na Laki Tatu kwa ajili ya matumizi kwa mwaka ujao wa fedha. (*Makofî*)

Mhe. Spika, matumizi ya fedha hizi yanaenda sambamba na kuwatumikia wananchi wa nchi yetu hii ya Zanzibar; kwa maana ya Unguja na Pemba.

Maidhinisho ya fedha hizi Mhe. Spika, inajumuisha pia kiasi kile cha fedha ambacho tumekuja tukawasilisha hapa kama Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ambazo ni kujumuisha ile miradi mitatu muhimu pamoja na shughuli nyengine, kuwajali wajasiriamali lakini pia uendelezwaji wa masuala ya viwanda kwa ajili ya kuwapatia vijana na zaidi wananchi wa nchi hizi ajira.

Mhe. Spika, nimeshangazwa, tumeshituka sote humu kwa nini wenzetu dakika ya mwisho wanasusia jambo hili na haifahamiki kwa nini. Kwa sababu kama mwanzo

tumekwenda vizuri tukapitisha kwa kila Wizara kwa pamoja, leo katika majumuisho basi wanatoka nje. Inatuletea hisia ya mchezo wa kitoto! (*Makofî*)

Mhe. Spika, tunasema ni mchezo wa kitoto kwa sababu watoto wanapocheza akiona kwamba anashindwa, tukitoa mfano labda wa gololi au karata hata nage, akishaona anaelekeea kushindwa basi anavuruga kila kitu anasema sitaki na anatoka. Ndicho walichokifanya leo hapa ndani, wamewadhihirishia wananchi kwamba sera zao na yale wanaojidai kwamba wanataka Serikali ya Umoja wa Kitaifa ilikuwa ni kwa sababu zao binafsi na siyo kwa sababu ya wananchi. (*Makofî*)

Mhe. Spika, ni kwa sababu zao binafsi, na kama walivyotangulia kusema Waheshimiwa hapa wengine na zaidi Mhe. Hamza Hassan Juma basi wangefanya kweli wangerudisha kila kitu, wangeanza na kurudisha magari, wangerudisha funguo za Mawaziri, wakarudisha kwa Mhe. Rais wakamwambia aah! sisi basi. Lakini mbona wametoka hapa na kutoka hapa wameingia kwenye magari yale yale wakaondoka nayo. Mhe. Spika, huu ni mchezo wa kitoto. (*Makofî*)

Mhe. Spika, tunawataka wananchi wawaelewe na wawafahamu hivyo, na kwa kuwa tunaingia kwenye uchaguzi, tuseme kwamba ni dalili za wao kuona kwamba tayari wameshashindwa. Kwa sababu *dalili ya mvua ni mawingu*, na hapa wanaonekana kushindwa.

Mimi ninataka niseme Mhe. Spika, nimebahatika kuwa mionganoni mwa waangalizi wa waandikishaji wa daftari katika Mkoa wa Magharibi.

Jana nilikuja kwa muda mfupi na baadae nikatoka tukawa tunapita katika maeneo tuliyopangwiwa kukagua shughuli za uandikishaji zinavyokwenda.

Mhe. Spika, zinakwenda vizuri sana, na ndio maana tukasema hatuelevi kwa nini Babu hapa ndani akalamika, zimekwenda vizuri kwa muda uliopangwa, wananchi wametoka majumbani kwa amani, utulivu na usalama, wamekwenda wamehakikiwa na walioandikishwa kwa dakika za mwisho wameandikishwa na kurudi majumbani, hakuna aliyeonewa, hakuna aliyeumizwa, hakuna aliyefanywa chochote. (*Makofî*)

Kwa hivyo, wanachokifanya wao hapa ni mchezo wa kitoto Mhe. Spika, na mimi ninasema kwetu sisi umetupatia *credit*. Tunaingia katika uchaguzi huu tunaingia vifua mbele, kwamba sasa dalili za ushindi tumeziona.

Tunakwenda tukiwa na uhakika na Mwenyezi Mungu atatujalia tutashinda na tutashinda kwa kishindo. Kwa sababu yale yote mema na mazuri ambayo Chama

cha Mapinduzi tumeahidi tutayatekeleza kwa wananchi wetu, tumeweza kuyafanikisha kwa asilimia kubwa sana, karibu mia moja kasoro kidogo sana.

Kwa maneno yake mwenyewe Mhe. Rais ninataka nimpongeze hapa kwa kuchukua fomu, na hili ninadhani pia limechangia kiasi kikubwa kuwarudisha nyuma. Kwa sababu hawakutegemea kabisa, na walikuwa wameshasema maneno mengi kwamba Mhe. Rais hatochukua fomu, wanajua huyu ndiyo kiboko yao.

Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein shikilia uzi huo huo, na Mwenyezi Mungu atakujaalia *in shaa Allah* na sisi tupo nyuma, ushindi ni wa kishindo mwaka huu kuliko kipindi kilichopita. (*Makofî*)

Mhe. Spika, tunafahamu Mheshimiwa kwamba ni mstahamilivu, una subra, Mwenyezi Mungu kashushia hekma ya hali ya juu, lakini kwa mtindo huu waliokufanya hapa Mawaziri uliowateua mwenyewe, ipo haja Mhe. Rais kulitafakari upya suala hili la watu hawa kuingia katika Baraza lako la Mapinduzi.

Tunakuomba sana huruma yako kwa hili hebu iweke pembeni, fanya wajibu wako, tekeleza wajibu wako, na sisi tupo bega kwa bega na wewe tunakuunga mkono kwa asilimia mia moja. (*Makofî*)

Mhe. Spika, ninasema mimi ninaiunga mkono hoja hii ya matumizi ya fedha hizi kwa asilimia zote, na katika kulitekeleza hili nimuombe basi Mhe. Waziri wa Fedha alitazame vizuri hili suala la posho za hawa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa upande wa hawa waliogoma hapa. Kiinua mgongo chao, kwa hawa waliogoma wametoka hapa, taratibu zinaelekeza Mhe. Spika, kwamba unapogoma basi ndiyo ijulikane kwamba umegoma usirudi tena, lakini wenzetu hawa sisi tunawafahamu. (*Makofî*)

Mhe. Spika, mwaka ule wa 2002/2003 wakati tunapitisha ile Sheria asilimia 30 ya wanawake kuingia kwenye vvyombo hivi vya sheria, waligoma wakatoka.

Nadhani tuliokuweko wakati ule tutakumbuka, walitoka tena kwa kishindo, lakini baadae tukastaajabu sana tukashangaa kuona walikuja humu kwa nafasi zile zile za asilimia 30, na wakaapishwa hapa wakala viapo na wakawa wamo humu kwa asilimia ambazo wao walizisusia na wakatoka.

Leo hapa limejirudia tena, baada ya kujirudia kule kwenye Bunge la Katiba na hapa limejirudia tena.

Mimi nasema Mhe. Spika, kwa hili hawataki hata kiinua mgongo hawa, hawastahili kupewa. Maana yake ndio wameshapiga mstari wameshatoka, wametafuta sababu, hii sababu sio ya msingi, madaftari yanaendelea kwa amani na

utulivu, na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatuwafikisha tumalize kwa amani na utulivu. (*Makofî*)

Mhe. Spika, mimi nasema jana wakati tunazunguka CCM tumejitokeza vizuri na tumeandikisha vizuri sana, na jana peke yake ingetosha kabisa leo tunakwenda kumaliza kazi tu, ushindi ni lazima kwa Chama cha Mapinduzi Mhe. Spika, na hili wamelifahamu.

Nasema kwamba naiunga mkono hoja hii ya matumizi ya fedha hizi ili tuweze kuendelea kuwatumikia wananchi wetu, ili imani yao juu yetu iendelee kuwepo na naiunga mkono kwa asilimia mia moja.

Nakushukuru sana Mhe. Spika. (*Makofî*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, kabla sijamkaribisha Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, nawaomba sana Waheshimiwa Wajumbe tubaki humu ndani, walioko nje tuingie ndani tumalize kazi hii.

Pili, tujaribu kusema kwa kifupi ili tuhakikishe tunamaliza juu ya wakati. Kimsingi *quorum* inaelekea kutimia. Walioko nje wakiingia ndani tutaifanya hiyo kazi.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, kwa kifupi sana. Walioko nje wapite ndani.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na afya njema.

Pili, naomba nikushukuru wewe binafsi kwa kunijaalia na mimi kunipa nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu katika kuunga mkono mswada huu, kwa ajili ya matumizi na mapato ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka 2015/2016.

Mhe. Spika, kwanza kabisa ningombwa nitoe wito kwa wananchi wote wa Mkoa wa Mjini Magharibi na Mkoa wa Kusini, ambao hawajapata nafasi ya kwenda kuijandikisha wale wenye sifa, basi wajitokeze kwa wingi, ili waorodheshwe katika daftari, na waweze kupata haki yao ya msingi ya kwenda kupiga kura.

Vile vile naomba nitoe wito kwa vyombo vyetu vya ulinzi na usalama, wasichelewe kuchukua hatua za kisheria, kwa ye yeyote ambaye amedhamiria kufanya fujo ama kutaka kuvuruga mchakato mzima unaoendelea wa uandikishaji wananchi wetu katika daftari la kupigia kura.

Mhe. Spika, pia ningeomba serikali kwa kupitia waziri wetu, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, naomba sana ulinzi wa kwa Sheha wa Bububu na Masheha hasa wa Mkoa wa Mjini Magharibi uimarishwe. Tukiimarisha ulinzi kwa Masheha maana yake tunawapa nguvu ya kusimamia majukumu yao kwa mujibu wa sheria zilizopitishwa na Baraza hili Tukufu. (*Makofi*)

Mhe. Spika, tukichelewa kuwaimarishia ulinzi wakijenga hofu basi tunakaribisha vurugu. Mchakato huu ukivurugika, maana yake serikali itakuwa imeshindwa kutimiza wajibu wake, jambo ambalo mimi siamini kama serikali hii makini itashindwa kusimamia wajibu wake wa kisheria na wa kikatiba. Kwa hivyo, naomba sana vyombo vyta ulinzi na usalama visimamie na kutimiza wajibu wao wa kikatiba. (*Makofi*)

Mhe. Spika, jambo ambalo liko wazi, na ninaamini ndio lililowapelekea wenzetu kutoka, ni kuona kila ishara kwamba ushindi wa CCM hauna doa, na kwenye hili wala tusijadiliane. Sisi tupo makini na tutahakikisha kwa nguvu zetu zote, Chama cha Mapinduzi kinaendelea kuungwa mkono na wananchi walio wengi Zanzibar. (*Makofi*)

Mhe. Spika, tutafanya hivyo kwa msingi wa haki, utaratibu na kuwashawishi watu kwa sera zetu nzuri, kama vile ambavyo tumeweza kutekeleza ilani yetu kwa kipindi hiki cha miaka mitano.

Mhe. Spika, wewe ni shahidi ni kwa kiasi gani Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kipindi hiki cha miaka mitano tumeweza kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi kwa vitendo. (*Makofi*)

Mhe. Spika, sote ni mashahidi kiasi ambacho Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweza kuimarisha miundombinu ya sekta za usafiri pamoja na miundombinu ya anga, halikadhalika na miundombinu kwa upande wa barabara.

Matarajio yangu ni kwamba wananchi walio wengi, watakuwa wameona mafanikio makubwa sana yaliyopatikana chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein. Mafanikio haya inawezekana ikawa ndio sababu na nongwa ya kuwapelekea wenzetu hawa kutaka kuvuruga.

Mhe. Spika, lakini kwa bahati nzuri tunapozungumzia maendeleo, maana yake hatubagi mtu katika itikadi yake, yanakwenda sehemu zote za Zanzibar; mjini na vijiji.

Ukuaji wetu wa uchumi kutoka asilimia 5 mpaka asilimia 7, yaani mwaka 2010 mpaka mwaka 2015. Bila shaka kila mmoja wetu atakuwa amenufaika na ukuaji huu.

Mhe. Spika, serikali hii hii imeweza kwa mara ya kwanza kwenda katika *universal pension*, kwa watu wetu wote wenye umri zaidi ya miaka 60. Huku ni kuonesha kwamba serikali hii inamjali hata yule ambaye ameweza kustaafuli, lakini kwa kuthamini kwamba na yeche aliota mchango katika Taifa hili, basi ana haki ya kupata kile ambacho serikali imeweza kuongeza.

Mhe. Spika, naomba nitofautiane kidogo na wenzangu. Mimi sipingi uwepo wa serikali ya *GNU*, wala sitofanya hata siku moja kusema kwamba kusiwepo na serikali ya *GNU*, lakini naomba ama Katiba ama sheria ni lazima kuna mwahali tufanye marekebisho. Utaratibu huu wa *ku-behave* kama hivi ambavyo wenzetu wana-behave, sidhani kama ndio malengo ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Spika, wenzetu wa Zimbambwe waliweza kuweka asilimia maalum inayolazimisha uwepo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Nadhani na sisi Zanzibar tuna sababu sasa za kuangalia vizuri uwepo wa Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa, lakini namna wenzetu wanavyo-behave, sio utaratibu kabisa kama kiongozi wa serikali, kama kiongozi wa kijamii.

Ni wajibu wetu kama Serikali kutengeneza au kuangalia taratibu zetu za kisheria, ili tuweze kuwa na viongozi ambao wanakuja na taswira ile inayotegemewa na wananchi wanaowaongoza. Haiwezekani kiongozi wa serikali, unayelipwa na serikali, unayewatumikia wananchi kwa niaba ya serikali wewe mwenyewe ukawa kiongozi au mtu wa mbele katika kuipinga serikali ambayo wewe unaifanyia kazi. Huu sio utaratibu wa serikali, na siamini kama kuna waziri ye yeyote duniani anayeweza kufanya vituko kama hivi!

Mhe. Spika, tuangalie upya sheria zetu na mienendo ya viongozi hawa wenzetu, ili tuweze kuona wanarudi katika mstari unaokusudiwa.

Mhe. Spika, wenzetu hawa wamezungumza kwa mapana sana juu ya suala zima la *Escrow*, na kusema kwamba upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano, upande wa Tanganyika, upande wa Tanzania Bara unatunyanyasa kwamba sisi hatujahusika katika *Escrow* tunazuiwa misaada.

Mhe. Spika, malalamiko haya hayana msingi, tunaowalalamikia ni wafadhili na wahisani wa maendeleo ni watu ambao wana akili timamu, wana uono wao, wana upeo wao na sababu zilizopelekea kuinyima misaada Tanzania wameziona, na wao walichokiomba ni serikali kuanza kuchukua hatua.

Serikali ya Jamhuri ya Muungano imechukua hatua na wao bila shaka zimewaridhisha, tayari wao wenyewe wameanza kurejesha misaada hiyo. Naamini kwamba doa hili ambalo sisi tumeathirika tuendelee kuvumilia, na huu ndio Muungano wenyewe, tusitegemee Muungano kwamba kila jambo jema lifanywe na wenzetu na sisi tunufaikie, ama kila jema ambalo tutafanya sisi na wenzetu wanufaikie, bila shaka na baya likija likitoka kwao na sisi tutaathirika, na baya likitoka kwetu na wao wataathirika.

Mhe. Spika, sote hapa ni mashahidi Serikali ya Jamhuri ya Muungano kwa maana kwamba upande wa Tanzania Bara, tokea uhuru wa mwaka 1961 imekuwa ni nchi ya kwanza kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, iliyokuwa na sifa ya kupokea wakimbizi. Sisi mwaka 2001 tulizalisha wakimbizi, tena wakimbizi wa kudanganya, wakimbizi wa kuji- *act* tu hao tukaenda Kenya Shimoni tukawatia doa wenzetu, lakini wakalikubali doa lile kwa niaba ya Tanzania, kwamba Tanzania inazalisha wakimbizi bila ya sisi kulalamika na wao wakavumilia.

Sasa na sisi kama kuna janga la watu waliofanya wizi katika *Escrow*, serikali imechukua hatua, tusianze kulifanya hili kuwa ndio ajenda ya kujadili Muungano wetu kwamba kuna kasoro imetokea.

Wajibu wa serikali ni kuchukua hatua pale yanapotokea mapungufu ya kisheria, na tayari Serikali ya Jamhuri imeshachukua hatua.

Mhe. Spika, niwaombe sana wenzetu hawa kugomea kwao ni dhahiri kwamba wanataka hata zile bilioni 7.5 zilizopangwa kwa ajili ya uchaguzi chini ya kifungu cha 5 cha mswada huu maana yake hawazitaki.

Wamegomea fedha hizi kwamba zisipitishwe, maana yake hawataki uchaguzi ukafanyike, sisi tunafanya jambo la heri. Dkt. Shein ataendelea atapiga miaka mitano mingine, na sisi tutaendelea kubaki Barazani hapa tutapiga mitano mingine, lakini sio malengo.

Malengo tunayotaka sisi kila baada ya miaka mitano tupate nafasi ya kwenda kujipima kwa yale ambayo tumeahidi, namna tulivyotekeleza na namna wananchi walivyokubali sera za chama chetu. Kwa hivyo, Mhe. Spika, tuwaombe huko një waliko watuanganlie kwenye TV, tutapitisha mswada huu na fedha hizi zitapatikana, tutakwenda kufanya uchaguzi na CCM itashinda! (*Makofî*)

Mhe. Spika: Jitahidi na muda.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, jengine linalowakera labda ni utulivu na amani ambayo imepatikana vizuri zaidi.

Niwaombe sana, sisi kama Serikali tutahakikisha kwamba maendeleo yetu yanaendelea kupelekwa kwa wananchi wetu.

Mimi mwenyewe ni shahidi, mwaka 2010 katika Jimbo la Chwaka tulikuwa tuna vijiji karibu sita vilikuwa havina maji safi na salama. Hivi sasa tumebakiza vijiji viwili na imani yangu serikali kama alivyotuahidi Mhe. Waziri husika na Mhe. Waziri wa Fedha, kijiji cha mwisho kukamilishiwa mradi wa maji kitakuwa ni kijiji cha Uroa, na ahadi ya serikali kwamba kabla ya mwezi wa Oktoba mwaka huu, basi maji Uroa yatakuwa yamefika, naamini kwamba jambo hili litatekelezwa.

Mhe. Spika: Malizia.

Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano: Mhe. Spika, niliwahi kupata siku moja kuzungumza na viongozi wa dini, na niliwaomba kwamba kama viongozi wa dini watashindwa kutuongoza katika mlango wa amani, maana yake twabaan hawawezi kutuongoza katika mlango wa pepo. Hawa viongozi wa kisiasa kama wameshindwa wenzetu kutuongoza kushindwa kushiriki katika zoezi hili la upitishaji wa mswada huu, bila shaka hawawezi kusimama katika kuwatetea wananchi.

Mhe. Spika, naomba nimalizie kwa kusema kwamba viongozi hawa wamefanya jambo bayu, na sisi kama viongozi wa CCM sote kwa umoja wetu tuwe watulivu, wasikivu na tuhakikishe kuwa mswada huu unapita kwa ajili ya kujenga maslahi na matumizi bora kwa ajili ya kupeleka maendeleo kwa wananchi wetu. Mhe. Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia. (*Makofî*)

Mhe. Spika: Nakushukuru sana Mhe. Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano, nimkaribishe sasa Mhe. Naibu Waziri wa Afya na yeze apate muda mchache sana, ili tumuite Mhe. Waziri hapo baadae ili kufanya majumuisho baada ya mawaziri na wao kuchangia kidogo. Mhe. Naibu Waziri wa Afya.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Spika, kwanza naomba kuchukua fursa hii kumuomba Mwenyezi Mungu, kwa kutujaalia tukiweko sisi tuliokuwemo humu ndani leo hii kuwatumikia wananchi wa Zanzibar, kwa kuitisha mswada huu wa fedha ambazo zitakwenda moja kwa moja kwa wananchi katika hali yao ngumu kuwanunulia dawa, kuwasomesha watoto wa kinyonge, kwenda kwenye skuli za serikali kulipa malipo mbali mbali. (*Makofî*)
Naomba leo Mhe. Spika, kitu chako na Katibu aweke *record* ya historia hii, kwamba fedha hizi zinapitishwa na waliokuwemo humu ndani ya Baraza hili kwenda kwa wananchi moja kwa moja.

Mhe. Spika, fedha hizi hizi ndio zinakwenda kwenye Tume ya Uchaguzi, ndio zinaweka mambo mengine yote sawa ambapo huko tunakotaka kuelekea. Sasa ndugu zetu waliotoka wao pia watahukumiwa na historia hii ya kwamba leo hatumo humu ndani pamoa, katika ule umoja wetu wa kitaifa.

Mhe. Spika, wewe ni shahidi na ni kiongozi mmoja wapo shahidi mkubwa sana, wa jinsi ule mswada uliowasilishwa hapa ndani ya Baraza lako Tukufu la Wawakilishi. Mswada wa kurekebisha Katiba ambao mimi pia mmoja wapo nilibahati kushiriki. Mswada wa kubadilisha vifungu mbali mbali nya kuweza kuleta umoja wa kitaifa.

Mhe. Spika, mara nyangi tukikaa humu ndani tunahisi kwamba wananchi kule nje, labda sisi tumewazidi, laa sivyo. Mimi nasema wananchi wametuzidi sana kwa mambo mengi kule nje, katika kutuhukumu hata kutu-*judge* mawazo yetu na maoni yetu tunayoyatoa humu ndani, na leo wananchi wanaona, wananchi wana akili wanafahamu, na leo wanaona mambo yote yanayofanyika humu ndani tokea asubuhi kutolewa taarifa hapa mpaka hapa tulipo. Mhe. Spika, mimi nataka kusema kwamba huu umoja wetu wa kitaifa umekwenda kwenye *test*, mitihani mbali mbali, na leo huu ni mtihani wake mwengine.

Mwananchi wa kawaida mmojawapo wakati tumekwenda Dodoma tupo kwenye Bunge la Katiba, mwananchi wa kawaida tu, aliniambia Mheshimiwa nyinyi mnakwenda kwenye mtihani wa umoja wa kitaifa wenu. Nikamuuliza mimi kwa nini. Akasema nyinyi Zanzibar mmesharekebisha Katiba yenu mna umoja wa kitaifa. Mbona mkifika Dodoma ule umoja wenu wa kitaifa wa Zanzibar unavunjika humu ndani. Hilo la mwanzo aliniuliza. Kwa hivyo, pale imeonesha dhahiri kwamba wako wale walioamini kidhati na wako wale ambao hawajaamini kidhati katika umoja wa kitaifa huu.

Pili, Mhe. Spika, mimi naomba kumpongeza sana Dkt. Ali Mohamed Shein. Humu ndani wamo wengi waliogombea kupitia Chama changu cha Mapinduzi CCM mwaka 2010 katika kiti cha Urais; yuko Mhe. Ali Juma Shamuhuna aligombea, yuko Mhe. Mohammed bin Aboud na yeze aligombea, yuko Mhe. Haroun Ali Suleiman naye aligombea, yuko Mhe. Shamsi Vuai Nahodha na yeze aligombea. Kama nimemsahau mwengine naomba radhi, nimewataja waliokuwepo humu ndani, maana tunazungumza. Hayupo leo Mhe. Mohammeddraza, lakini hakugombea katika uchaguzi uliopita. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk kasema katia nia yeze ya kugombea.(*Makofifi*)

Mhe. Spika, Mwenyezi Mungu kamjaalia Dkt. Ali Mohamed Shein kupita, na leo Dkt. Ali Mohamed Shein kwa umahiri wake, kwa ujasiri wake, kwa hekima na busara zake wengi wao aliyegombea nao kawachagua mawaziri humu ndani wamo. Niliowataja hao wengi wao ni mawaziri humu ndani. Lau kama *test* hizi

angepata kiongozi mwengine yejote. Hili nasema wazi, na nalitamka wazi, *test hizi za umoja wa kitaifa* huu angepata kiongozi yejote mwengine basi angetetereka, yeje ni mvumilivu na mstahamilivu. (*Makofii*)

Mhe. Spika, leo Rais gani angekubali mawaziri wake ambao anafanya kazi nao katika BLM, katika *Cabinet*, leo wanyanyuke. Huu ni mswada wa serikali Mhe. Spika, sio hoja binafsi, *this is not a private motion or private bill*, huu ni mswada wa Serikali, ni *appropriation bill* ambayo imewasilishwa na Waziri wa Fedha, na inasimamiwa na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

Sasa leo imekuwa serikali kipande au suruali kipande, maana mawaziri husika wa kusimamia *appropriation bill* hii leo hawapo ambayo inapitisha bajeti ya mishahara yao, bajeti ya mafuta yao, bajeti ya wizara zao, bajeti ya Tume ya Uchaguzi ambayo keshokutwa tunakwenda kupiga kura. Bajeti ya hayo malalamiko ya kujandikisha yanayotolewa, madaftari na kadhalika ndio bajeti yake hii. (*Makofii*)

Sasa leo haya tutafanyaje Mhe. Spika. Mimi baadae Mhe. Spika, nitakuomba muongozo wako kwa masuala yafuatayo.

Mhe. Issa Haji Ussi Gavu Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano katika mchango wake hapa alisema, tumeunda umoja wa kitaifa, lakini baada ya pale hatukuweka *rule of the game*. Nakumbuka fika mimi kwamba iliundwa kamati ya watu sita humu ndani ikiongozwa na Mhe. Ali Mzee Ali, wajumbe wake wengine wamo humu Barazani leo na wengine hawamo. Alikuwepo Mhe. Haji Omar Kheri, alikuwepo Mhe. Naibu Spika, katika kamati hiyo na walifanya kazi kubwa sana. (*Makofii*)

Mhe. Spika, leo mimi nakuomba hawa baada ya kuleta ile ripoti yao na kuwasilisha kwako, kulikuwa kuna mambo waliyapanga mule ndani, nadhani mambo kama 20 hivi.

Mhe. Spika, wewe nakumbuka ultwambia humu ndani ya Baraza, katika *Hansard* ya mwisho kabisa wakati kinafungwa kikao, mwaka 2010 kama sijakosea ilikuwa katika jengo hili hili, ndio kikao cha mwanzo kilifanyika katika jengo hili. Ulisema yatawasilishwa kwa serikali ili mambo haya yasimamiwe na kutekelezwa.

Miongoni mwa yale mambo zimo sheria ambazo zinabana na zinauongoza umoja wa kitaifa huu ufanye kazi vipi.

Mhe. Spika, nitakuomba tena suala hili ulikumbushie na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atakapomjaalia Mhe. Dkt. Ali Mohammed Shein, atakapokuja kulivunja

baraza hili rasmi, naomba Mungu siku hiyo alitolee tamko kwa sababu wananchi wamekaa tayari wanataka kusikia tamko lake. Wananchi hawaridhishwi na haya mambo tunayofanya humu ndani, hawaridhishwi leo wananchi, ndio watakaohukumu kesho kutwa kwenye sanduku la kura, wanaona *appropriation bill* ya Serikali watu hawapo, juzi umekuja Mswada wananchi wengi wameelimika, juzi ulikuja mswada hapa binafsi *private motion* wa Mhe. Hamad Masoud, kuhusu vitambulisho, kuhusu kadi, kuhusu mambo ya daftari, namshukuru sana Mhe. Haji Omar Kheri, siku ile Mungu amempa nguvu vitambulisho vyote vimeletwa hapa mbele vimewekwa mbele na vidhibiti vyote hapa.

Kwa hivyo, Mheshimiwa, nitakuomba sana muongozo wako katika ku-set up rules of the game tunafanyaje, je, tutaendelea hivi hivi hawa watakuwa wanatoka au hawatoki, leo wangetoka *back bencher* mimi nisingesema lolote, ni haki yao kutoka lakini katika *appropriation bill* ya Serikali kutoka Mawaziri from the cabinet; hili haliwezi kufahamishika kwa wananchi. Wala wananchi hawawezi kufahamu maana *backbencher* ana haki yeye, anawakilisha jimbo lake.

Mhe. Spika, nikimalizia kuchangia mimi namuomba tena Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aendelea kuwa mvumilivu, Mwenyezi Mungu kamjaalia kapasi mitihani yake yote hiyo ya heka heka mpaka tumefika leo. Huu ni mtihani ambao wanapewa wa mwisho, ambao Mungu atamjaalia naye atafanikiwa. Atafanikiwa kwanza kwa kupata kura nyingi, kwa sababu wananchi leo wanaona juzi amechukua fomu Afisi Kuu pale ya Chama cha Mapinduzi, kwa hivi hizi ni ishara njema ya kwamba atapata kura nyingi sana kwa sababu leo wananchi huko nje...

Maana tuna wananchi aina tatu; wa kwanza ni yule mwenye chama ama anapenda chama hiki au anapenda chama hiki. Mwengine ni mshabiki, lakini wa tatu ni yule mwananchi wa kawaida ambaye hana chama chochote lakini *ana-judge* ni mpiga kura halali wa nchi hii ambaye atatoa hukumu kwa kuona haya yanayoendelea.

Jengine Mhe. Spika, nawaomba sana wananchi wa Jimbo langu la Kiembesamaki kesho ndio utaratibu rasmi wa kuandikisha kwa wale wote waliokuwa hawajaandikishwa unaanza katika eneo letu hili. Nawaomba wananchi wote pamoja na wanachama wa chama cha Mapinduzi waliokuwa hawajajitekeza kwenda kuandikisha, wajitokeze kwa wingi ili wapate haki yao ya kupiga kura hasa wale waliokuwa hawajapata nafasi ya kujiandikisha, ili wawewe kupiga kura na kuhukumu kwa hali hii tunayoendelea nayo.

Mhe. Spika, kwa kumalizia kabisa naomba tena kuunga mkono Mswada huu wa Shs. bilioni mia nane na thalathini na tatu na mia tatu ambao leo huu ndio utakuwa mshahara wa wafanyakazi wote wa Serikali. Nawaomba wafanyakazi wa Serikali

leo wote watakaopata mishahara kutoka *appropriation bill* hii tunayoipitisha hapa wawapigie kura waliokuwemo humu ndani, kwa sababu mishahara yao leo, mapato ya wazazi watoto wao wanaosoma skuli zote, wanaokwenda kutumia huduma za afya, kutibiwa katika mahospitali yote, leo pesa zao zinapitishwa na hawa waliokuwemo humu ndani. Historia iwahukumu hawa waliokuwemo humu ndani kufanya jambo hili jema na naamini wananchi watakaofaidika kwa njia moja au nyengine na bajeti hii ya Serikali leo, watawapa shukurani zao waliokuwemo humu ndani wote kwa pamoa.

Mhe. Spika, mwisho kabisa nasema tena kwamba jambo hili la umoja wa kitaifa halikuwa rahisi, tuweke nia thabiti kama tunataka umoja wa kitaifa, tuweke nia thabiti ya umoja wa kitaifa, wakati wa kura za maoni wakati ule haikuwa rahisi na leo ikija kuamuliwa kupigwa kura za maoni tena sijui itakuwaje. Kwa hivyo nawaomba ndugu zangu wote waliokuwa wametoka nje ya Baraza hili wasikose nafasi nyengine ya kihistoria ambayo Mhe. Rais atakuja hapa kuhutubia na kuja kutufungia Baraza. Wasikose nafasi hiyo, huyu ni Rais ambaye amewateua wao kuwa Viongozi, Mawaziri na Manaibu Waziri wa Serikali hii ya Umoja wa Kitaifa na haikuwa rahisi jambo hili kufika hapa tulipofika leo. Wengi walipata tabu, wengi walihukumiwa, wengi walipata madhila mbali mbali mpaka hapa tulipofika, leo tusichezee demokrasia, tusichezee amani, tusichezee utulivu wetu tuliokuwa nao humu.

Mhe. Spika, nakushukuru sana naunga mkono Mswada huu na Mungu akitujaalia wewe na hekima zako na busara zako utatuongoza katika ule muongozo nilioomba. Ahsante sana Mhe. Spika. (*Makofi*)

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Utumishi: Mhe. Spika, awali ya yote na mimi nimshukuru Mwenyezi Mungu *subuhanahu wataala* kwa kutujaalia kuendelea salama usalimini kwa mfungo wa Mwezi wa Ramadhan.

La pili, nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii na mimi kuchangia Mswada huu muhimu sana wa Serikali. Kwanza kabisa naomba kwa niaba ya Wananchi wote wa Jimbo la Mkunduchi, jimbo mama la CCM kwamba tunaunga mkono kwa asilimia mia moja Mswada huu wa matumizi.

Mhe. Spika, nikushukuru sana na wewe kwa jinsi unavyotuongoza katika Baraza hili tukufu, hotuba yako ya asubuhi leo ilikuwa ni dira katika kuchangia michango yetu ya hivi sasa.

Nimshukuru sana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kazi nzuri anazoendelea kufanya na *inshaallah* Mwenyezi Mungu akitujaalia katika miaka mitano inayokuja atazidi kutufanya kazi vizuri zaidi, *inshallah* na

sisi tutaendelea kumsaidia. Ameonesha uwezo na Mwenyezi Mungu amemjaalia na kipaji cha kutuongoza sisi na *Inshaallah* Mungu atamjaalia atafanikiwa.

Mhe. Spika, wengi wamezungumza hapa leo Waheshimiwa kule ZANTEL au sijui taasisi gani ambayo inasema; *now we talking, I don't TIGO eeh*, sasa watu wanazungumza humu ndani leo wamejitutumua kweli kweli, mimi nadhani haijawahi kutokea hata mara moja Mswada wote kuchangiwa na watu wengi na wazito kama leo Mheshimiwa kwa uchungu kabisa, na kila mmoja kazungumza kwa ustadi wake. Leo tumeona dalili humu ndani, kuna mashehe humu wameibuka, sasa sijui kama wameibuka kwa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani au vipi, lakini Muwakilishi wangu leo wa Matemwe katoa vitu.

Mheshimiwa wa Kwhani leo katoa vitu pale na waheshimiwa wengine hata Mheshimiwa Makame Mshimba nae katoa vitu, Mhe. Amani nae kwa leo alhamdullillahi nae kajitahidi, sasa kumbe mambo yapo.

Mimi nimesimama baada ya kuunga mkono Mswada huu juu ya matumizi ya Serikali. Nimesikitika sana na kitendo cha Waziri mwenzetu kufanya kitendo kama kile, labda kwa sababu pengine hajui taratibu za kiserikali au vipi, lakini si vyema sisi Mawaziri tukawa mstari wa mbele katika masuala kama haya, nadhani ingependeza sana tukawa mfano sisi siku zote kwa *back bencher*, haipendezi na wananchi wameona na wananchi wa Makunduchi wameona vile vile, Zanzibar wote na Makunduchi wameona.

Siku moja ulifanyika mkutano wa hadhara kule Makunduchi wa chama hicho, sasa siku ya pili nikaja Barazani hapa kuna Mheshimiwa mmoja akanambia rafiki yangu CCM *bye bye* Makunduchi, nikamwambia haya lakini nadhani unaota Mheshimiwa, Makunduchi kumehamasika sana sana, tena sasa, hivi na si Makunduchi tu, Zanzibar yote wamehamasika, wanachama wetu wa Chama cha Mapinduzi. Sasa hivi mikutano inayofanyika kule unaona fika kwamba wananchi wamehamasika kupindukia na *Inshaallah* wanasubiri kwa hamu siku ya kwenda kupiga kura tukijaaliwa, na nimekuwa nashiriki kikamilifu katika futari ambazo wananchi wanaziandaa kule.

Hivi sasa na vijana wamehamasika kweli kweli na wanangojea tarehe kwenda kuandikisha kwenye daftari hili kupigia kura. Kule mambo ni mazuri na *Inshaallah* Mwenyezi Mungu atatujaalia tutamaliza kwa salama na amani, lakini Jimbo la Makunduchi na Majimbo mengine kwa Mkao wa Kusini na majimbo mengine *Inshaalah* ni imara na *Inshaallah* tukijaaliwa tutashinda.

Mhe. Spika, leo kazi yetu ingekuwa ata si kubwa lakini hotuba za Ijumaa zile na mimi najaribu kidogo hotuba za Ijumaa hutolewa, siku nyengine ziko

zilizoandaliwa kwa ratiba, lakini wakati mwengine hotuba za Ijumaa hutolewa kwa mujibu wa matokeo yanayotokea katika nchi. Sasa leo hapa Barazani imekuwa hili suala ambalo limetokezea humu ndani la jamaa hawa kutoka, ndio imekuwa sasa ndio ajenda yetu kubwa na sisi, lakini si jambo la busara la kufanya kama hivyo kutoka humu ndani. Tungekaa hapa, tukasikiliza, tukapitisha bajeti hii muhimu kwa Serikali yetu, ili tuweze kufanya matumizi yetu vizuri. Kwa sababu unaposusia kupitisha matumizi haya kwa kweli tunafanya makosa, mambo yote ambayo tutayatumia katika Serikali yetu katika bajeti inayokuja tunayapitisha leo. Sasa wewe umeondoka, je, wale wananchi watakuhamu vi?

Mhe. Spika, kama nilivyokuomba mimi nilikuwa na machache sana lakini naomba sana tuwe waangalifu katika masuala kama hayo. Mawaziri tujitahidi tuwe mstari wa mbele sisi kuonesha mfano siku zote, na tumuunge mkono Rais wetu ambae kwa kweli anatusaidia sana katika kila hali. Mhe. Spika, naungamkono hoja. (*Makofit*)

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa Idara Maalum za SMZ:
Mhe. Spika, awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu adhuhuri hii ya leo, kunipa nafasi kuwa mionganoni mwa wachangiaji kwa kuchangia Mswada huu wa kuidhinisha matumizi ya Serikali.

Pili, nikupongeze wewe. Tatu, kwa namna ya pekee nimpongeze Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa busara zake na hekima za kuiongoza nchi yetu. Nne, pia niwapongeze wajumbe wenzangu wote wa Baraza la Wawakilishi kupidia Chama dume Chama cha CCM ambao kwa umahiri wao wameweza kutoa maoni yao juu Mswada huu wa kuidhinisha matumizi ya Serikali kwa mwaka 2015/2016.

Mhe. Spika, naomba kwa unyenyekevu mkubwa katika bajeti zote sikupata fursa ya kuweza kuchangia, kwa hivyo, leo naomba uturuhusu na tuko tayari kuongeza muda lakini tumalize kiu ya wananchi wa Zanzibar waliotuleta humu ndani. Kwa hivyo, nitakuomba sana Mhe. Spika, usinambie muda wako umemaliza, kwa sababu baraza hili tokea imeanza bajeti Wawakilishi wa Chama cha CUF wanaishutumu na kuitupia madongo Wizara ambayo nimepewa dhamana ya kuiongoza, hata hapa walipotoka wamekwenda kukutana wameitisha mukutano na waandishi wa habari wanaendelea kuishutumu Wizara ya Tawala za Mikoa na idara Maalum za SMZ.

Hata Waziri asiyejjua kama Waziri alipotoa hoja alitaja Wizara ya Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara maalum za SMZ, ni shtuma na yeze alidhani kugombania jimbo ni *free lunch*; kugombania jimbo sio *free lunch*, kwamba alidhani Bububu kuna *free lunch*. Kugombania jimbo kwende kwenye uchaguzi

lazima chama chochote kile cha siasa kijiandae kufanya kazi, kuwatendea wananchi mambo mazuri na kutekeleza ilani na sera yao. Sasa Chama cha Mapinduzi kimetekeleza kwa vitendo ilani yake ya mwaka 2015.

Kwa hivyo, kwa kutegemea kwamba Chama cha Mapinduzi kitekeleze sera yake na ilani yake halafu CUF mpate *free lunch* katika nchi hii ya Zanzibar hakuna *free lunch*, *CCM* tumefanya kazi, Serikali inayoongozwa na CCM imefanya kazi ya kutekeleza ilani ya uchaguzi. Na mimi ili nisije nikasahau kwa niaba ya wananchi wenzangu wa Jimbo la Tumbatu, naunga mkono Matumizi haya ya Serikali kwa mwaka 2015/2016 kwa asilimia mia moja. Nina sababu zangu kwa nini naunga mkono na Wananchi wa Tumbatu wanajua kwa nini naunga mkono. Hivi sasa *jet ambayo* Dkt. Shein aliahidi inaendelea kujengwa, kwa maana ya gati imetokana na fedha tulizoidhinisha mwaka 2014/2015. Kama mimi ningekuwa mjinga, mpumbavu nisinge idhinisha bajeti iliyopita, bandari ile ingejengwa vipi?

Kuna ahadi ya Mhe. Rais ya kumalizia mradi wa maji Tumbatu, hivi sasa unaendelea kutekelezwa jumla ya milioni mia tatu ishirini na nane zimetolewa kupidia bajeti ambayo tunaimalizia. Kama mimi nisingeidhinisha fedha hizi zingekujaje Tumbatu kutekeleza mradi wa maji. Kwa hivyo, kwa msingi huo ndio maana bajeti hii ya mwaka 2015/2016 naidhinisha na naidhinisha kwa sababu najua kwamba kwenye fedha za maendeleo, Serikali imetenga jumla ya bilioni mia tatu tisini na nane, mia tisa na hamsini na sita milioni kwa ajili ya *development budget*.

Katika bajeti hiyo kuna mchango wa Serikali ya Zanzibar wa bilioni 51.88 imo ndani ya matumizi haya, itakuwa ni vichekezo vikubwa sana mimi nisipoidhinisha na ni vichekesho vikubwa sana kwa wale waliotoka ndani ya Baraza hili; nasema hivyo kwa sababu nikijua kuna bandari itakayojengwa Mkokotoni kupidia mkopo wa *ADB* na mchango wa Serikali ni huu hapa, sina sababu ya matumizi haya nisiaidhinishe. Kuna barabara ya Pale/Kiongele ambayo itaingia kwenye *component* hii itajengwa, sina sababu ya kukataa kupitisha bajeti hii. Kuna barabara ya Mtambile/Muwanda ambayo itajengwa na mambo mengi mengineyo ambayo yatafanyika baada ya idhini itakayotolewa na kuunga mkono mimi Haji Omar Kheir, kama muwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Tumbatu ndipo matumizi hayo yaweze kuidhinishwa.

Sasa wale waliokuwa wakipiga kelele wanataka barabara, wanaotaka maji leo hii wametoka nje hivi kweli hawa wanawatakia mema wananchi, hawawatakii mema wananchi. Nawaomba wananchi muwakatae kwenye uchaguzi mkuu utakaokuja mwaka huu 2015.

Mhe. Spika, Wawakilishi wengi walitoka ndani ya Baraza hili ni kutoka kisiwa cha pili cha Pemba. Serikali ilifanya juhudhi ya kuandaa mradi wa undwaji wa meli ya abiria, kuna dola 6.1 milioni za Kimarekani zinatakiwa zilipwe kupitia bajeti hii. Wawakilishi wenu wananchi wa Pemba wametoka kuna sababu ya kuwachagua? Hakuna sababu ya kuwachagua, wao wanapiga kelele. (*Makofî*)

Juzi hapa nilikuwa nikiwasikiliza Wawakilishi wanasema Meli ya *M.V. Maendeleo* imezima moto wananchi heka heka. Hawa ni mamba, wanatafuna huku wanatoka machozi, kama kweli mnawapenda wananchi wa Pemba mngekaa mkaidhinisha bajeti dola 6.1 milioni tukaidhinisha kwa pamoja, ili serikali ikamalizia malipo wananchi wa Pemba wakapata kupanda meli. (*Makofî*)

Mlikuwa mukiteeta nini, bajeti zote mumetetea ilipokuja miundombinu mumesema, ilipokuja Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali mumembana waziri kuhusu madeski wakati wa ripoti za kamati mumembana waziri ametoa ufanuzi. Serikali imeweka mipango madhubuti ya kutengeneza madeski, ili wanafunzi waweze kukaa vizuri. Nyinyi mnazuia hamtaki kutoa. Wananchi msiwape kura mwezi wa Oktoba ukifika.

Mhe. Spika, Mhe. Abdi Mosi Kombo, alimnukuu Dkt. Salmin Amour Juma "*Aljununu fununu*", asiyejua maana usimwambie maana. Sasa wenzetu hawajui maana na wangkuwa makini kweli, wangetutega tu wakati tunapitisha vifungu hapa wakapiga buti, lakini tunashukuru Mwenyezi Mungu mkubwa bwana. Kwa sababu Mwenyezi Mungu hapendi maovu yao ndio maana wametoka na sisi leo mswada huu tukaupitisha.

Yote ni ukubwa wa Mwenyezi Mungu, anajua nia yao ni nini na anajua sisi nia yetu nini. Nia yetu ni kuwatetea wananchi wa Zanzibar, wametoka basi sisi tutapitisha Mhe. Spika wala usiwe na wasiwasi. Hata kama tutaongeza muda, robo saa hivi, lakini mswada huu leo utapita.

Mhe. Spika, nimeombwa kama Waziri wa Nchi, (OR), Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kuhusu suala la ulinzi wa Sheha wa Bububu. Anasema masheha wote wako salama na anayetaka kwenda kucheza ende akacheze kwa Sheha wa Bububu. Kama hawamjui yule hata hahitaji ulinzi, ye ye mwenyewe ni mwali mu wa hayo mambo. Siwatishi lakini nawatahadharisha. Sheha wa Bububu wamuelewe ni nani sitaki kuendelea zaidi.

Mhe. Spika, kama alivyosema Rais wetu mpendwa Dkt. Ali Mohammed Shein kwenye uwanja wa Kibanda Maiti, Uwanja wa Demokrasia kwamba kama kuna mwaka utafanyika uchaguzi ulio huru na haki ni mwaka huu wa 2015. Kama kuna mwaka utakaofanyika uchaguzi wa amani na utulivu ni mwaka huu 2015.

Anayejitayarisha kufanya fujo ahame, anayejiandaa kufanya fujo atafute pa kwenda, Zanzibar hakuna nafasi ya kufanya fujo.

Serikali ya wananchi wa Zanzibar inayoongozwa na Chama cha Mapinduzi imetengeneza taratibu nzuri za kutunga sheria kupitia Baraza hili tukufu, sheria hizo tumezitunga wote. Serikali inazisimamia na sote hatuna budi tuzifuate.

Sheria inayoongoza uchaguzi ni Sheria ya Uchaguzi, sheria inayoongoza upatikanaji wa *Zan-ID* ni Sheria ya *Zan-ID*, sheria ya ugawaji wa mipaka ya utawala ni sheria tulizopitisha hapa, sisi wote hakuna aliyeipinga. Tutafanya uchaguzi kupitia sheria ya uchaguzi ulio huru na haki na tutasimamia taratibu na kanuni za ulinzi na usalama kwa mujibu wa sheria ya nchi.

Sisi tumeona kwamba wanataka kuanzia hapa. Nataka kuwambia hapa sipo pa kuanzia, hawawezi kturejesha tulikotoka, hawawezi. Baadhi ya Wajumbe wamesema kwamba tuliwahi kutengeneza wakimbizi wa bandia kule Shimonii. Kama hilo ndilo lengo lao haitatokea hiyo kitu. Tunasema tena uchaguzi utafanyika, wao walipita wakijilabu, wakijigamba kwamba mwaka huu wao wanaingia Ikulu, walidhani Ikulu ni mchezo.

Sasa wanalamika wananchi wanajiandikisha wengi. Ah! kwani nyinyi mlitaka wananchi wasijiandikishe. Wananchi kujeandikisha ambao wana haki ya kujeandikisha ni wajibu wao na ni wajibu wa serikali kusimamia wananchi wenye haki ya kujeandikisha kuingia kwenye daftari, waingie kwenye daftari la kupiga kura. Asiye haki haingii, mwenye haki ataingia.

Tume ya Uchaguzi imeandikisha wapiga kura ambao hawaajaingia kwenye daftari Pemba, mbona hawakutoka humu ndani. Hivi *issue* ya vitambulisho kwani imekuja leo, wakati unaandikishwa Pemba si ilikuwepo mbona hawakutoka. Lakini baada ya kuona raia wema, wananchi wana-CCM walikuwa hawajafikia umri kipindi kilichopita, wapo kwa wingi wanajiandikisha wameanza kuingia homa, ingieni!

Mhe. Spika, nasema mimi najua wanaendelea kushutumu Wizara yangu, lakini mimi nimepewa dhamana ya kusimamia Wizara hii ya Tawala za Mikoa na Idara Maalum na sisimamii kwa mabavu, nasimamia kwa mujibu wa sheria ambazo nimekuja nazo hapa, Baraza hili imezipitisha ndizo ambazo mimi nazisimamia. Sina sababu ya kutokuzisimamia sheria hizo.

Mhe. Spika, baada ya kusema hayo kwa mara nyengine tena naunga mkono Mswada huu kwa niaba ya wananchi wenzangu wa jimbo la Tumbatu kwa asilimia 100, ahsante sana. (*Makofii*)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: "Waatasimu bihablillahi jamiaah wala tafaraq" (*Makofi*)

Hayo ni maneo ya Mwenyezi Mungu amewaasa watu wake, "Kwamba shikamaneni katika kamba ya Mwenyezi Mungu wala msifarikiane." Hili ndilo niloliliona hapa linatendeka leo. Tumeshikamana kweli kweli na wale waliofarikiana wametoka, wamekwenda zao, wataita waandishi wa habari. Waite redio, wataita televisheni, watatukana lakini humu hawamo wameshatoka. Wamekataa mwezi wa Ramadhanii huu maneno ya Mwenyezi Mungu ya kwamba tushikamane wala tusifarikiane. *Inshallah* tutashikamana tutamaliza kwa amani na utulivu.

Mhe. Spika, baada ya utangulizi huo nikupongeze wewe sana kwa hotuba yako ya leo asubuhi. Mwenyewe ulisema ungelijua ungeliiandika na ikawa ndefu, ikawa nzito, lakini umeshtukiziwa hali ile, je, hapo ungeiandika ingekuwa vipi? Tunakushukuru.

Pia, nimshukuru Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein, kwa utulivu wake kwa subra zake, kwa umahiri wake wa kuiendesha nchi yetu kwa salama na amani. Namshukuru baada ya watu kumwendea na kusema mzee kachukue fomu ya Uraisi, alikwenda moja kwa moja, kwenda kuchukua fomu ya Uraisi. Katika hilo namshukuru na nampongeza sana, Mwenyezi Mungu *Inshaallah* atamjaalia kama walivyotangulia wenzangu hapa kumuombea dua kwamba apite na yeje atapita.

Nampongeza sana Mhe. Hamza Hassan Juma, kwa maneno aliyojasema; mazito sana, ya busara na ya muala. Nampongeza sana na kila alilolisema naliunga mkono.

Namshukuru Waziri wa Fedha sana sana kwa umahiri wake kutupeleka hapa tulipofika. Mhe. Waziri wa Fedha alipokwisha usoma Mswada wake kwa mara ya mwanzo kabla hawa jamaa hawajatoka. Sasa tunaendelea na shughuli zetu na katika mshikamano wetu aliotwambia Mwenyezi Mungu, tushikamane kila mijumbe aliyesimama hapa akazungumza na alizungumza kwa umahiri sana, kwa umakini sana, bila ya shaka yoyote Mswada huu utapita. (*Makofi*)

Mimi kwa niaba ya wananchi wa Donge wapiga kura wangu naunga mkono Mswada huu kwa asilimia mia moja, tuupitisheni ili Waziri wa Fedha aweze kuruhusika kuzitumia fedha hizi kikatiba na kisheria. Mimi kama alivyojsema ndugu yangu Haji Omar Kheri, sina sababu ya kuukataa Mswada huu. Wenzetu wameukataa maana hawapo, wanaotaka kujengewa barabara, kujengewa bandari wameukataa. Maana kuna watu walisema tukajenge bandari ya Wete, wanaotaka kujengewa *airport* wameukataa. *Airport* hii waliikataa zamani wakaja na msemo wao basi tukawekeni vibatari pale *airport* viwake, ili ndege zituwe usiku.

Mwenyezi Mungu siku zote hamfichi mnafiki. Maana ule ulikuwa ni unafiki si kutujejea, lakini ni unafiki. Kwa nini?

Tukampa Wizara ya Mawasiliano na Miundombinu, wewe uwe Waziri chukua Wizara hii ya Mawasiliano na Miundombinu. Hatukuona taa, wala mshumaa, wala kibatari, mpaka kaondoka. Tumempa Waziri kama yeze nafasi hii sasa hivi, tumelijadili katika Baraza hili hili suala la Uwanja wa Ndege wa Pemba. Alituletea mipango yake hapa wakati anazungumza bajeti yake na anaomba fedha akafanye hiyo kazi.

Alitueleza mengi na tukasema bajeti hii tutaitipisha sio kama ile ya mwaka jana. Hii tutaitipisha tukajenge kiwanja cha Ndege Pemba, bajeti tukaipitisha. Leo Waziri huyu huyu anayetaka kwenda kujenga Kiwanja cha Ndege Pemba, kaikataa bajeti hii, "*thuma amanu thuma kafaru, thuma sdadu kufra.*" (*Makofii*)

Sasa hivi nasema hivi, kesho nasema vile na zaidi na kesho kutwa nasema zaidi ya zile. Sijui tukamate lipi? Tukajenge uwanja, au tukatae kujenga uwanja kama alivyokataa Waziri tuliyompa akatujengee uwanja. Waziri wa Fedha usiikatae, kwa umahiri wako na umakini wako usiikatae. Tutaitipisha Mswada huu, tutakuruhusu kama kwenda kukopa kakope, kama kuzitumia fedha hizi zitumie, lakini kiwanja cha ndege Pemba kijengwe. Tukitaka kumsuta mnafiki tusimzomee, lifanye lile la kheri lake yeze linalomuhusu. Baadaye tutaalizana sasa je, tumejenga hatukujenga? (*Makofii*)

Mhe. Spika, pale Donge pana skuli kubwa ya ghorofa imejengwa na wananchi siyo serikali. Rais wetu mpendwa wakati wa kampeni aliahidi wananchi hapa mlipofika nakushukuruni si padogo pakubwa, serikali yenu itaimaliza. Mkinipa kura ya kuwa Rais nitaimaliza. Nilikuwa namkumbusha Shekhe Mwinyi hapa, wewe ndiyo mratibu wa ahadi za Rais, mara mbili, tatu.

Mimi nimeshakwenda kwa Rais kumkumbusha na mwenyewe kasema kalifanyeni, limalizeni hili. *Alhamdulilahi* tukalimaliza mpaka sasa tumeiyezeka, ukipita nzuri, kazi ndogo tu iliyobakia. Shekhe nakuletea leo leo, makisio ya pale tulipobakisha ili umkumbushe Mtukufu Rais tuimalize. (*Makofii*)

Mimi Waziri wa Elimu, nina madawati na watoto kila siku wanazaliwa na tumesema elimu ni bure. Kila anayezaliwa anastahiki kupata elimu, atapata kikalio, atapata mabanda ya skuli ya kukaa. Tumezungumza mbinu kadhaa wa kadhaa za kutafuta pesa za kujenga madawati. Nimeleta hesababu kamilii hapa, pesa ngapi tumechukua, madawati mangapi tumefanya na tumeyasambaza wapi. Ikaundwa Kamati hapa ya kuchunguza kule tulipoyasambaza ndipo na yapo kwa bahati mbaya Kamati bado haijarejesha ripoti. Lakini mimi ninayo taarifa, wamekwenda

wameyakuta madawati yapo Pemba na Unguja, Kusini, Kaskazini, Mashariki na Magharibi. Hatujakamilisha yale tunayoyahitaja yote lakini mipango inaendelea.

Nimeshakaa na Waziri wa Fedha, tumezungumza mipango madhubuti sasa hivi tutaishirikisha mpaka Tanzania Bara kwa sababu elimu ya juu ni jambo la muungano. Tukimaliza bajeti tu, tunakaa tunazungumza na wenzetu tunapanga namna gani ya kuzitafuta hizi pesa. Nina shughuli za madawati, nina shughuli za maabara, sasa ukinambia nitoke nje nisiunge mkono mswada huu pesa hizi tutazipata wapi. Watoto wa wananchi wanyonge na maskini tutawasomesha nini, tutawasomesha wapi?

Mhe. Spika, nina skuli zisizopungua 250 na ushei zilizojengwa na wananchi hazijamalizika, kama mswada huu wa *appropriation bill* haukupita hapa tunamwambia Waziri wa Fedha pesa usizitumie, tunamwambia Waziri wa Fedha usende kukopa, tunamwambia Waziri wa Fedha hatutaki maendeleo, tumekesha hapa siku nenda, siku rudi kujadili bajeti zetu kuhusu mipango ya maendeleo na mipango mengineyo. Leo tumeshamaliza mjadala wa *sector ministry*, leo tunakuja kupitisha *appropriation bill* ili tumpe waziri nafasi kisheria, sasa kuzitumia hizi pesa tulizopitisha. Sasa mimi nashindwa kuifahamu tafsiri hii ya watu kutoka nje, kugomea huu mkutano wetu wa kupitisha hii *bill*, ninashindwa kufahamu.

Mhe. Spika, kwenye Bunge la Katiba Dodoma tuliyaona hayo hayo, yalipotokea ghafla tukapata mshtuko kidogo, lakini Mwenyekiti wa Bunge la Katiba akishauriana na Katibu wa Bunge la Katiba, yupo hapa, huyo hapo, tuendelee au tusiendelee, tutapata *quorum* au hatupati? Wakahesabu, wakapanga *quorum* imetimia, hatukulivunja Bunge la Katiba, tukaendelea nalo. Tukajadili shughuli zote baadae Katiba ya mpito tukaipeleka kwa mwenyewe Rais, tukamkabidhi. Sasa tunataka kuipeleka kwa wananchi waipigie kura ya maoni.

Tungeshtuka tukatoka na sisi nje au tukasimamisha Bunge la Katiba wakati tushapokea pesa nydingi sana tushazitumia kama walivyotumia wenzetu walipopokea wenzetu hawa, wamezipokea pesa nydingi si kidogo, wengine wakafanya mgomo baridi humu ndani hawaingii hawataki, *quorum* haitimii mpaka *Alhamdulillahi*, tumelimaliza. Leo dakika ya mwisho sehemu ya kumalizia *totally wanatugomea wana-walk out*.

Mhe. Spika, narejea tena kusema kwa hiari yao na kwa ushauri wao wenyewe wametupa nafasi tufanye yetu na *Alhamdulillahi* tumeyafanya.

Mwenzangu mmoja hapa alisema, wewe ukisusa wenzio wala. Nataka nimuongezee sio ukisusa wenzetu wala aa, tunakula kwa matonge, tumekula kweli kweli sio mchezo, tumeyafuata maagizo ya Mwenyezi Mungu kwamba tukamatane tusihitilafiane. Tumekamatana kweli na kwa usemi wako tumekula kweli

kweli, sasa tunangojea tunawe tukishapiga *fat-ha*, kura zimeshatimia tunapitisha *bill* yetu hii Waziri wa Fedha unakwenda kuzitumia pesa, ili tumalize shughuli zetu za mkutano. (*Makofî*)

Mhe. Spika, ninakushukuru sana sana kwa kunipa nafasi hii na mimi ingawa kwa muda mrefu kidogo nimekuwa mkimya mkimya, lakini sina budi kwa leo lazima niingie katika mchango wa mswada huu *Alhamdulillahi*, umenipa nafasi ninakushukuru sana. Naunga mkono mimi pamoja na wananchi wangu wa Donge, pamoja na wazanzibari wote asilimia 100. Ahsante sana. (*Makofî*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa kabla hatujaendelea na shughuli hii nataka niwaambie jambo moja muhimu sana. Kazi hii tunayoifanya sasa hivi ni moja kati ya kazi muhimu sana ambayo ili tuweze kuendesha Serikali ni lazima mswada huu upitishwe. Kutopitishwa kwa mswada huu maana yake Serikali haitaweza kufanya kazi na utaratibu itabidi ni Mhe. Rais, kutumia mamlaka yake ya kuidhinisha malipo ya mishahara ya wafanyakazi na mambo mengine hayataweza kufanyika.

Sasa *crisis* hii maana hii ni *crisis*, kama haukupita hii ni *crisis*, ni *crisis* kwa sababu kama jambo hili halikupita kama mlivyokwisha eleza hapa hata uchaguzi mkuu utashindikana kuuendesha, jambo ambalo ni la kidemokrasia.

Muda wetu unakaribia kwisha na hili ni suala la dharura kubwa, wajumbe wetu bado wengine wako nje najua wanakwenda kusali, sasa kwa kutumia kanuni ya 158 kuhusu mambo ambayo hayakuwekewa utaratibu lakini dharura imetutokezea kwa sababu kama wajumbe wengine wako nje, wajumbe waliopo hatuwezi kutoa hoja tukaamua ndio maana yake.

Sasa dharura aina kama hii pengine ingehitaji kutoa hoja na suala hili la *ku-manage* muda Spika, anatumia nafasi hii. Kanuni imeelekeza katika mikutano ya bajeti uchangiaji ni dakika 30 na mjumbe anaweza akaongeza dakika kumi ndivyo ilivyo kwenye kanuni. Lakini tunapeana dakika 20 kwa sababu ya kuzingatia muda na hali ya mambo hiyo ni *discretion* ya Spika yule anayekuwa kitini hapa. Wakati mwengine tunapeana dakika kumi, ni *discretion* ya Spika mambo yanakwenda.

Na kwa kuwa sasa muda unakaribia kumalizika kwa kutumia kifungu hiki kwa dharura hii tuliyonayo, Spika anatumia *discretion* tuendelee na shughuli hii mpaka tumalize. Maana hili ni jambo kubwa, ni jambo muhimu na ni lazima liende kwa mujibu wa taratibu. Kwa hivyo, shughuli zinaendelea mpaka tumalize. (*Makofî*)

Baada ya machache hayo basi nimuombe Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, kwanza nikupongeze kwa maelezo yako uliomalizia hivi punde na inaonesha wazi imani yako kubwa uliyonayo kwa wananchi wa Zanzibar na nchi yetu kwa jumla. Mwenyezi Mungu azidi kukuongezea na atazidi kukupa mafanikio na baraka nyingi katika maisha yako. Aidha, nichukuwe fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uwezo wa kuweza kuendesha mambo yetu kwa salama na naamini tutamaliza kwa salama.

Mhe. Spika, na waheshimiwa wajumbe naomba pia kuchukua fursa hii kumpongeza sana sana Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwanza kwa uongozi wake mahiri, busara na uvumilivu mkubwa alionao, lakini kwa nia yake thabit ya kuridhia bajeti hii kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa Zanzibar, tunampongeza sana.

Aidha, nimpongeze sana rafiki yangu ndugu yangu Mhe. Waziri wa Fedha na watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa namna walivyotayarisha bajeti hii makini sana yenye nia njema ya kuwahudumia wazanzibari wote. Lakini pongezi maalum zende kwa wawakili wote wa CCM waliomo ndani ya Baraza hili, wamefanya kazi kubwa na nzuri ambayo kwa nia na dhamira ya kuiokoa nchi yetu.

Wenzetu waliotoka walifanya kwa makusudi, walidhani tutashindwa kupitisha bajeti yetu, bajeti yetu tutaipitisha ili yende ikahudumie wananchi, ili yende ikafanye maendeleo ya nchi yetu. Ni jambo la kustaabisha sana Mhe. Spika, kama walivyosema wenzangu kumuona Waziri ambaye alikuwa ni sehemu ya kutengeneza bajeti hii leo anakuwa anawashawishi wenzake kususia bajeti hii.

Ni miujiza, aibu, unafiki. Wazee wetu walitwambia hao sio lakini tukasema aa, wenzetu tufanye nao kazi, matokeo yake leo wananchi wote wa Zanzibar wamewaona watu hawa walivyokuwa hawana busara za uongozi, hawana imani na wananchi wa nchi hii na hawayataki mema maendeleo ya nchi yetu. Maana bila ya bajeti hatuwezi kutoa huduma muhimu.

Mhe. Spika, bajeti hii imekuja hapa ikieleza mambo mengi muhimu ambayo tunatakiwa tuwafanyie wananchi wetu nitataja kwa kiasi. Moja ni kuipandisha hadhi hospitali ya Mnazimmoja ili iweze kutoa huduma bora kwa ajili ya wananchi wetu. Kuvipandisha hadhi vituo vya huduma za afya, ujenzi wa Abdalla Mzee hospitali ya Pemba, mradi mkuu wa kuoanisha huduma za afya na uzazi ya mama na mtoto, mradi mkuu wa kudhibiti maradhi ya ukimwi, kifua kikuu na ukoma, uimarishaji wa miundombinu ya maji, mradi wa uimarishaji wa elimu, mradi wa hifadhi ya haki za watoto, Mradi wa Ujenzi wa Kiwanja cha Ndege Pemba, Mradi wa barabara mbali mbali za Pemba, Mradi wa Uimarishaji Uvuvi Nchini,

Uimarishaji Kilimo, Ufugaji, Kujenga Mazingira mazuri ya Biashara, Kuendeleza Barabara zikiwemo za Wete/Chake, Ole/Kengeja na nyengine na nyengine.

Leo kwenye mambo mema kama haya ya maendeleo ya nchi yetu wanatokea wenzetu kususia bajeti ili mambo hayo yasiwafikie wananchi. Itastaajabisha sana, kuona bado wananchi wakaweza hata kura moja CUF, kwa mambo haya.

Mimi ninaamini kwa haya waliyoyaona hapa basi wananchi wa Pemba nao watatanabahi kuona hakuna chama ambacho kilio tayari kuwahudumia zaidi ya Chama cha Mapinduzi. Na kwa sababu tuko tayari kuwahudumia wananchi na ndio maana tumebak humu ndani, kwa hivyo hapana shaka yoyote Chama cha Mapinduzi kitashinda kwa ushindi mkubwa sana. Na wao kama wanachukia kwa sababu ya ushindi wa CCM, mimi ninawaambia kabisa kwamba ushindi wa CCM ni mkubwa sana.

Mhe. Haji, anasema waache wavimbe mpaka wapasuke lakini huo ndio ukweli ni ukweli kwa sababu ya *record* nzuri ya utekelezaji wa ilani yetu, busara za viongozi, imani ya viongozi wa chama hiki kwa wananchi wa nchi yetu na ndio maana nasema bila ya CCM nchi yetu itayumba.

Kwa hivyo, CCM itaendelea kuwepo na itaendelea kuongoza nchi hii milele na milele na wala hao wengine hawapo, unakaa unakataa bajeti ambayo wewe ni sehemu ya kufanya bajeti hiyo, halafu unatoka, mtu mzima una maarifa gani ya namna hiyo?

Mwenzetu mmoja hapa alisema usisusie kupitisha bajeti basi susia na kuacha mshahara, posho, gari na kadhalika. Maana ndio hii bajeti inayotusababisha tufanye hayo. Kwa hivyo, kwa vyovoyote vile sisi tulimo humu ndani wana CCM kwa sababu ya nia njema ya kutaka maendeleo ya nchi yetu tunabaki, tutateteta wananchi wa nchi hii, tutawahudumia wananchi wa nchi hii na kila zuri tutalifanya ili kuhakikisha wananchi wetu wanapata maisha yaliyo bora zaidi.

Wamepiga kelele sana wakisema masuala ya gasi na mafuta leo katika bajeti hii matayarisho hayo yamo, unasusia maana yake nini? Si wanawachezea wenzetu wanawavalisha kilemba cha ukoka. Maana kama kweli ulikuwa na hamu unataka kweli tuyachimbe mafuta, unataka kweli tuchimbe *gas* wangebaki tupitishe bajeti hii. Unataka kweli wananchi wetu wapate huduma za afya, wangebaki kupitisha bajeti hii.

Kwa hiyo, wananchi hicho ni kitandawili mkione wenzetu hawa namna gani walivyo wakorofu na siku nydingi wameanza haya, lakini chote hicho ni choyo na nia mbaya kwa nchi yetu. Sisi tunataka tuwahakikishie kwamba kila jema

tutalifanya, ili tuendelee kutoa huduma bora kwa ajili ya wananchi wetu, wapate maendeleo makubwa na waweze kushiriki katika kujenga nchi yao. Tena kwa visiwa vyetu vyote viwili vya Unguja na Pemba, ili hali za wananchi wetu zinawirike.

Mheshimiwa ndugu yangu Ibrahim Bhaa, alisema hapa kauli za Rais wetu zinaashiria umoja, amani na utulivu wa nchi, lakini kauli za viongozi wengine wa Chama cha *CUF* zinaashiria ugomvi, chuki na tofauti mambo ambayo yamepitwa na wakati kwa muda mrefu.

Nimestaajabu sana kwamba Muislamu kama rafiki yangu Juma Duni unapewa mkono na Muislamu mwenzako unakataa, ni jambo la ajabu kubwa sana. Wewe unamkatalia Bhaa kukupa mkono, Jimbo la Bububu litashinda CCM na mwakilishi wetu panapouhai atakuwa ni ndugu Ibrahim. Umekwenda mwenyewe kujitia demani hakuna aliyekwambia, tutakuchezesha mchakamchaka Sheikh Juma, utaona.

Kwa hivyo, kataa kutoa mkono, kataa kutoa uso, lile jimbo tutachukua tu. (*Makofî*)

Na rafiki yangu Mazrui tumekuazima Jimbo la Mtoni mara hii tunalichukua, hasa mnapoona wana CCM na wananchi wanaotaka amani wanajitokeza kwa wingi kuandikisha kwa nia ya kutafuta uongozi bora. Mlipojitoa hapa mmejiharibia zaidi. Alisema Mhe. Haji Omar Kheir, tulifanya uandikishaji Pemba hakukua na vurugu wala hakuna mwakilishi wa Unguja wa CCM aliyetoka hapa akenda Pemba kufanya vurugu. Lakini leo wametoka wawakilishi wa Pemba na viongozi wengine wamekuja kwenye majimbo ya Unguja kufanya vurugu, kuharibu uandikishaji, jambo hilo halitowezekana.

Suala la uandikishaji lipo kisheria na mimi nataka niwapongeze sana Masheha kwa kazi nzuri wanayoifanya, waendelee kufanya kazi hiyo na wasiwe na wasi wasi kama alivyosema Mhe. Haji Omar Kheir, ulinzi upo na uwezo wa kuwalinda tunao. Na ndugu zangu wa *CUF* siasa sio ugomvi wala chuki jenga hoja watu wakusikie, kama umeishiwa shukuru Mungu.

Sasa mnakuja hapa mnafanya zogo, vurugu na kitu kinakwenda kwa mujibu wa Katiba na Sheria. Zoezi la uandikishaji litaendelea na tutamaliza kwa salama na hizo nia zenu mbaya hazitofika mahali.

Mhe. Spika, tumekuja hapa wamekimbia kuchukua fedha za *CDF* Mfuko wa Jimbo, nataka niwaambie wananchi wa Pemba na wananchi wa Unguja kwamba kila aliyechukua fedha ya *CDF* za Mfuko wa Jimbo ni kwa ajili ya maendeleo ya wananchi. Kwa hivyo, zichungeni, zitizameni vizuri ni fedha zenu kwa hiyo

waliozichukua na wakatoka humu ndani wananchi mutanabahi kwamba fedha hizo ni za maendeleo yenu, zitizameni. Zichungeni ili zifanye mambo ya maendeleo katika nchi yetu.

Mhe. Spika, natuwakatae wote wale amba wana nia mbaya, wana nia ya nchi yetu kuifanya isitawalike, wana nia ya kufanya vurugu, ili tukae kwa hali ya amani na utulivu katika nchi yetu.

Ni wananchi ndio wenyewe usukani wa maamuzi mukiwakataa tatizo litaondoka tusiwape nguvu ya kusababisha vurugu, ya kusababisha kutokee matatizo katika nchi yetu. Lakini watu hawa tumewazoea kila jambo la kheri wanalikataa, walishawahidi kususia hili Baraza la Wawakilishi, wameshasusia Bunge la Katiba, wameshasusia mambo mengi ya msingi. Kwa hivyo, wanaporudia kususia ni mambo yao na ni kawaida yao, sisi wenyewe nia njema tufanye mambo yetu ili tufikie mafanikio.

Na mimi nataka niwahakikishie wananchi wote wa Unguja na Pemba kwamba tutaandikisha kwa salama, amani na utulivu mkubwa. Tutafanya uchaguzi huru na wa haki na kila mwenye haki ya kuandikishwa ataandikishwa na asiyekuwa na haki ya kuandikishwa haandikishwi. (*Makofî*)

Mhe. Spika, na kwa sababu *quorum* ishatimia mimi nataka niseme naunga mkono kwa asilimia mia moja Mswada huu wa Sheria wa Kuidhinisha Fedha na Matumizi, ili tuweze kuwashudumia wananchi wa Zanzibar.

Baraza lako hili la leo Mhe. Spika, liwekwe katika historia kwamba majamadari wamekaa wakapitisha bajeti yetu kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wa Zanzibar.

Mhe. Spika, nakushukuru na nawashukuru Wazanzibari wote kwa kutusikiliza na tunawahakikishia mambo yatakwenda vizuri. Ahsanteni sana. (*Makofî*)

Mhe. Spika: Katibu ananipa idadi ya wajumbe hivi sasa ili kuthibitisha hiyo *quorum*, maana mambo haya yanakwenda kwa mujibu wa taratibu. Waheshimiwa Wajumbe, nina furaha sana kwa mshikamano wenu idadi ya wajumbe sasa tunaweza tukaamua mambo, maana mambo haya yanakwenda kwa mujibu wa taratibu na nilisema mapema kwamba nina imani na ninalewa, na ninakubali kwamba nyinyi mnao uwezo kwa kuzingatia umuhimu wa shughuli iliyopo leo hivi sasa, iliyopo mezani. Mheshimiwa amekuja kwa ungo kutoka Dar es Salaam ambapo alikuwa anafanya majukumu mazito aliyopewa na serikali hii, kwa kuwashudumia wananchi. Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kwanza kuwapongeza sana, sana Waheshimiwa Wajumbe na nidhamu hii ndio inayohitajika kuendesha

chombo hiki. Sasa tubakie watulivu na sasa nimkaribishe Mhe. Waziri wa Fedha. (*Makofî*)

Waheshimiwa hakuna kutoka nje, kuna kuingia ndani tu, basi.

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, kwanza na mimi nataka niwashukuru wajumbe wote kwa kazi nzuri waliyoifanya na michango yao na mimi binafsi imenipa faraja. Nataka niwaeleze tu kwamba huo ndio uzalendo na upenzi wa nchi yao.

Mhe. Spika, kabla sijawataja wale ambao waliochangia naomba niseme nukta moja ambayo ni muhimu sana, hii itakuwa ni funzo na ni somo kwa kila mmoja wetu aliyemo ndani, aliyeo nje na wale ambao wanaotarajiwa kuingia mwezi wa Novemba.

Waheshimiwa Wajumbe, nilikushukuruni sana jana kwa kunipa fursa na ruhsa ya kukusanya mapato. Mliniruhusu kwa kupitia *finance bill* kwa kunambia Waziri wa Fedha sasa tunakuruhusu kakusanye mapato, lakini leo nilishangaa sana kuona ruhusa ambayo mlionipa ya kukusanya mapato baadhi wamekataa ruhusa ya kutumia.

Ruhusa ya kukusanya mlinipa lakini baadhi wamekataa kunipa ruhusa ya kutumia kwa kweli nilishangaa sana. Nilishangaa hasa nilipowaona ndugu zangu mawaziri ambao kama ilivyo na mionganî mwetu tumepanga bajeti kwa pamoja, tumezungumza kwa pamoja, tumeridhiana kwa pamoja, leo wameshindwa kuwa wastahamilivu na kuipa mamlaka na nguvu serikali yetu kuweza kuwatumikia wananchi.

Mhe. Spika, lakini nataka niwashukuru sana Wawakilishi wa Chama cha Mapinduzi mapenzi yenu kwa wananchi wenu wamekuoneni Unguja na Pemba na dua zilizosomwa na baadhi ya wajumbe wetu kwa Ramadhani ya leo Mwenyezi Mungu atazipa barka *Inshaallah* na mtakuja kuona barka yake. Ni ushindi wa Chama cha Mapinduzi uliomkubwa.

Mimi sikushangaa kwa sababu baadhi yao wengine wameshadondoka wale, sikushangaa sisi tutarudishwa na wananchi wetu na *inshaallah* tutashinda. (*Makofî*)

Mhe. Spika, mimi sio Shekhe, sio Mufti lakini na mimi namuombea sana dua Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ashinde kwa kishindo, arudi na awateue mawaziri majamadari waweze kupambana na wenzetu hawa.

Sisi tutapambana nao kwa maendeleo, wala hatuna vishindo tutatekeleza maendeleo, tutawatumikia wananchi wetu kwa faida ya nchi yetu na hayo ndio mapambano tutakayopeleka kwa wananchi wetu.

Nilisema mwanzo kama Sheha mmoja wanaingia mitini tuna masheha mia tatu na zaidi, na mimi kama alivyosema Mhe. Mohammed Aboud Jimbo la Bububu walisahau, hilo ni jimbo na ni ngome ya Chama cha Mapinduzi. Na ninaelewa kwamba wana misakamo sasa hivi wanamsakama Waziri wetu wa Tawala za Mikoa wamuache kama alivyo, wamsakame Waziri wao wa Miundombinu aliyetoa hoja ya kuwatoa wenzake nje. (*Makofî*)

Ndugu zangu wa Chama cha Mapinduzi, wawakilishi leo mmeridhia kupitisha bajeti hii ina maeneo mazito makubwa sana.

Kwanza kutoka kwao nadhani walisahau kwamba kuna shilingi bilioni 7.5 kwa ajili ya uchaguzi. Kusingweza kufanyika uchaguzi Chama cha Mapinduzi kingeendelea tu kutawala na Dkt. Shein angeendelea kuwa Rais. Sasa hawa ndugu zangu jamani mimi sitaki niwaambie hawakwenda shule, lakini nataka niseme kwamba wamekwenda shule lakini hawakufahamu kitu. (*Makofî*)

Kuna shilingi bilioni 8.5 mafao yao wenyewe, sasa haya mnataka kuniambia Waziri wa Fedha msiponipa nguvu za kutumia hizi pesa na haya yatakaa kibindoni. Kumbukeni mumeshanipa nguvu ya kukusanya, mimi nitakusanya nitaweka kibindoni.

Kuna shilingi bilioni 16.76 za kuendesha Baraza la Wawakilishi kuanzia tarehe 1 Julai, sasa sijui walikusidia nini. Kuna miradi chungumzima Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ameshaitaja.

Mhe. Spika, sasa nataka niseme wale ambao wamechangia kwa leo niwashukuru halafu tupitishe vifungu:

1. Mhe. Mahamoud Mohammed Mussa
2. Mhe. Hamza Hassan Juma
3. Mhe. Wanu Hafidh Ameir
4. Mhe. Mussa Ali Hassan
5. Mhe. Panya Ali Abdalla
6. Mhe. Shadya Mohammed Suleiman
7. Mhe. Nassor Salim Ali
8. Mhe. Mlinde Mbarouk Juma
9. Mhe. Marina Joel Thomas
10. Mhe. Fatma Mbarouk Said

11. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
12. Mhe. Makame Mshimba Mbarouk
13. Mhe. Abdi Mossi Kombo
14. Mhe. Viwe Khamis Abdalla
15. Mhe. Mgeni Hassan Juma
16. Mhe. Ali Salim Haji
17. Mhe. Amina Iddi Mabrouk
18. Mhe. Salma Mussa Bilali
19. Mhe. Bihindi Hamad Khamis
20. Mhe. Thuwayba Edington Kissasi
21. Mhe. Issa Haji Gavu
22. Mhe. Mahamoud Thabit Kombo
23. Mhe. Haroun Ali Suleiman
24. Mhe. Haji Omar Kheir
25. Mhe. Ali Juma Shamuhuna
26. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed

Mhe. Spika, huu ni mswada na yote ambayo wenzangu wamezungumzia katika mswada huu Mhe. Mwanasheria Mkuu ameyajumuisha na ninadhani wenzetu walidhani hatuwezi. Na Mhe. Spika, si kawaida katika Baraza hili watu kuimba lakini leo naomba kuimba kama ni *reference* tu, watu wameimba imba kidogo na mimi nakuomba uniruhusu kidogo tu nikumbushe. (wimbo unaimbwaa), *Walisema hatuwezi... (Makofit)*

Mhe. Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kutoa hoja. (*Makofit*)

Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Mhe. Waziri wa Fedha, nakushukuru sana kwa majumuisho ulyofanya na hatimae ukatoa hoja ikaungwa mkono na wote waliomo ndani, kilichobaki ni kuitisha utaratibu. Wale wanaokubaliana na hoja ya mswada huu wanyanyue mikono. Wanaokataa, Wajumbe wote waliomo ndani 41 wameukubali.

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

(*Hoja iliamuliwa na kuafikiwa*)

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, sasa naomba kutoa taarifa kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Kutunga Sheria ili kuupitia mswada huu kifungu baada ya kifungu.

KAMATI YA KUTUNGA SHERIA

Mswada wa Sheria ya Makisio na Matumizi ya Mwaka 2015

Kifungu 1	Jina fupi
Kifungu 2	Tafsiri
Kifungu 3	Utoaji wa Shilingi 830,360,300,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali
Kifungu 4	Makisio ya fedha zilizokubalika
Kifungu 5	Uwezo wa waziri wa kukopa
Kifungu 6	Uwezo wa waziri wa maombi ya ziada
Kifungu 7	Marejesho ya mkopo na riba
Kifungu 8	Kukubaliwa kwa mipango ya maendeleo
Kifungu 9	Kukubaliwa kwa fedha zilizopitishwa kwa matumizi ya maendeleo

(Baraza lilirudia)

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, ilivyokuwa Kamati ya Kutunga Sheria imeupitia Mswada wa Sheria ya Kuidhinisha Makisio na Matumizi ya Shilingi 830,360,300,000 kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha unaoishia siku ya tarehe 30 Juni, 2016 na kuruhusu utoaji wa uhaulishaji wa fedha hizo pamoja na mambo mengineyo yanayohusiana na hayo, kifungu kwa kifungu na kuukubali bila ya marekebisho sasa naliomba Baraza lako tukufu liukubali.

Naomba kutoa hoja.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Hoja imetolewa niwahoji wale wanaokubaliana na mswada huu wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofî*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja ilihamuliwa na kuafikiwa)

Mswada wa Sheria ya Makisio na Matumizi ya Mwaka 2015

(Kusomwa kwa mara ya tatu)

Mhe. Waziri wa Fedha: Mhe. Spika, naomba kutoa hoja kuwa Mswada wa Sheria ya Makisio na Matumizi ya Mwaka 2015 usomwe kwa mara ya tatu.

Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Ikulu na Utawala Bora: Mhe. Spika, naafiki.

Mhe. Spika: Niwahoji Waheshimiwa Wajumbe wanaokubaliana na Mswada katika kusomwa mara ya tatu wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofifi*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

(*Hoja iliamuliwa na kuafikiwa*)

(*Mswada wa Sheria ya Serikali ulisomwa mara ya tatu na kupidishwa*)

Mhe. Spika: Waheshimiwa Wajumbe, nielezee tena furaha yangu. Furaha yangu kwenu Waheshimiwa Wajumbe wa CCM mliyomo humu ndani ambaa mmekuwa na imani kubwa ya kupidisha Bajeti ya Serikali ambayo mmeipitisha leo rasmi, ili serikali hatimaye iweze kufanya kazi yake baada ya mswada huu kupata saini ya Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ya kuwahudumia wananchi.

Kazi hiyo mumeifanya nyinyi na wananchi nataka waelewe kwamba kazi hii imefanya na Wawakilishi wa CCM sio wengine. Kwa sababu jambo hili la mwisho ndio jambo lililokusanya kazi yote tulioifanya kuanzia tarehe 13 Mei, 2015 tungefeli hii ile yote ingekuwa ajuari. Lakini mmeifanya vizuri, kwa utulivu, kwa mashirikiano na kwa kweli kumbe wakati umefika sasa tukashikamana zaidi wajumbe tulioipo mpaka tumalize shughuli hizi, lakini mshikamano wa aina hii hii tuupeleke kwa wananchi mpaka kufikia hatma ya kumaliza kazi moja kubwa ya kutimiza demokrasia hapo tarehe 25 Oktoba, 2015. Hilo ni muhimu sana na kwa kweli mshikamano wenu utasaidia sana kufanikisha demokrasia hiyo iende vizuri.

Waheshimiwa Wajumbe, tulikuwa na kikao leo cha Kamati ya Uongozi, lakini kwa kazi kubwa mliyoifanya kikao kile kimeakhirika na kitafanyika kesho mara baada ya kupokea taarifa ya serikali katika ukumbi huu.

Kamati ya Uongozi ilikuwa inafanya kazi moja kubwa muhimu sana marekebisho ya kanuni zetu za kuendeshea chombo hiki, moja wapo ikiwa ni suala la nidhamu ya mahudhurio kama mtaona inafaa pengine kutakuwa na mambo mengine mtayohisi yanafaa tuingize kwenye kanuni hiyo. Hiyo itakuwa ni kazi ya Kamati ya Uongozi ya kesho.

Utaratibu wetu shughuli za kanuni hasa zinafanya na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala; kutohana na ufinyu wa muda na kwa sababu rasimu ya marekebisho ya kanuni hizo tutawahi kupidisha katika mkutano huu, ili wajumbe tutakaojaaliwa

kurudi tena tuwe na kitu kipyta kitakachoendesha vizuri zaidi shughuli zetu, basi hiyo Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala tunaialika katika Kamati ya Uongozi tufanye kazi pamoja, ili hatimae tuje tipeane *briefing* ya lile ambalo tumekubaliana na kuja kufanya *exemption* ya marekebisho ya kanuni hizo.

Kwa hiyo, Waheshimiwa Wajumbe, narudia kuwashukuru tena kwa mashirikiano makubwa tuliyofanya kiasi cha kwamba kazi ya leo hii kubwa muhimu kuimaliza wakati huu. Baada ya hayo Waheshimiwa Wajumbe, sasa nakiakhirisha kikao hiki hadi kesho siku ya Jumatano tarehe 24/6/2015 saa 3:00 za asubuhi.

(Saa 8:37 kikao kiliakhirishwa hadi tarehe 24/06/2015 saa 3:00 asubuhi)